**Watoto** kortini tuhuma kughushi saini warithi mali



UKURASA 7

**Mwanamke** auawa kikatili kwa madai ya ugomvi wa mali

UKURASA 8


ama
AFYA NA MAZINGIRA
Mtafiti aanika Ziwa Victoria limejaa tani 150 za plastiki, nywele za saluni
OFISINI KWA MWANAHABARI...
Simulizi 'msimamo' na 'uwazi' zilivyo silaha kuishinda rushwa ngono kazini
•Uamuzi menejimenti ni sheria tosha kumaliza

UKURASA 11


# Nipashe

Alhamisi Julai 29, 2021 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580656

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US


# UAMUZI MGUMU

**SAMIA** atoa sababu 6 kupata chanjo ya corona, dozi zaidi zaja, Askofu akemea wanaopinga...

*Endelea ukurasa 2*



Rais Samia Suluhu Hassan, akipatiwa chanjo ya Covid-19, baada ya kuizindua katika viwanja vya Ikulu, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: IKULU**

# Shahidi aangua kilio, adai Sabaya alitishia kumuua

UKURASA 3



Mhandisi Mkazi wa Mradi wa Uzalishaji Umeme wa Maji wa Julius Nyerere, John Mageni (kushoto), akitoa maelezo ya utekelezaji wa mradi kwa Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi Benki ya CRDB, Dk. Ally Laay (wapili kulia) na Mkurugenzi Mtendaji wa Benki hiyo, Abdulmajid Nsekela (wanne kulia), wakati wajumbe wa bodi hiyo, walipoutembelea katika bonde la Mto Rufiji, mkoani Pwani juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

UKURASA WA 2

## CHANJO NYINGINE NNE CORONA ZAJA NCHINI

SERIKALI inatarajia kuingiza aina nyingine nne za chanjo ya UVIKO-19 ili kukabiliana na maambukizi ya ugonjwa huo nchini. Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Dorothy Gwajima...

UKURASA WA 8

## NYOKA ASABABISHA MWALIMU MKUU KUIKIMBIA NYUMBA

MWALIMU Mkuu wa Shule ya Sekondari ya Dk. John Magufuli katika Kata ya Kamsekwa, wilayani Kaliua mkoani Tabora, amekimbia nyumba aliyojengewa na shule kwa hofu ya kuwapo nyoka aina ya kobogo. Mwenyekiti wa Serikali...

# Makundi hatarishi homa ya ini yatajwa

UKURASA 7

**MICHEZO** **SIMBA, MANARA WAACHANA RASMI** UK.24 **MAONI, KATUNI** UK.6

# Chanjo nyingine nne corona zaja nchini

**Na Waandishi Wetu**

SERIKALI inatarajia kuingiza aina nyingine nne za chanjo ya UVIKO-19 ili kukabiliana na maambukizi ya ugonjwa huo nchini.

Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Dorothy Gwajima, alibainisha hayo jana Ikulu jijini Dar es Salaam wakati wa uzinduzi wa chanjo ya corona kitaifa. Dk. Dorothy alitaja aina za chanjo hizo zitakazoletwa nchini baada ya kuingizwa kwa chanjo aina ya Johnson &Johnson, ni Moderna, Pfizer-BioNtech, Sinopharm na Sinovac.

Alisema serikali imeamua kuleta aina nyingi za chanjo ili kila mwananchi apate chanjo inayoendana na afya yake. "Hakuna dawa isiyokuwa na madhara lakini kuna faida zake, ndiyo dawa ziko hivyo na jinsi ya 'kumanage' na daktari kukuona wewe nisikupe hii, nikupe mbadala. "Ndiyo maana chanjo zitakuja nyingi, aina tano ili wananchi wafanye uamuzi na nyingine nyingi ambazo kamati yangu itaendelea kuzipitia, wazisome tuone huyu ana-fit hapa.

"Ili kufikia malengo tuliojiwekea, tumejipanga na wataalamu wetu kujibu hoja zote zinazotolewa mitandaoni, tunajibu kisayansi hoja kwa hoja na watu waulize maswali tuyajibu," alisema.

Akizungumzia taarifa za upotashaji kuwa chanjo hiyo ya Johnson & Johnson ilisitishwa kutolewa kwa wananchi wa Marekani, alisema walisitisha Aprili kwa sababu za kujiridhisha na upungufu uliojitokeza lakini zinaendelea kutumiwa na kwamba watu zaidi ya milioni nane wameshachanja.

Alisema suala la kutia saini makubaliano ya kuchanja ni kawaida kwa operesheni za chanjo duniani kote. "Kwenye nchi zilizochanja vizuri, zinaonyesha kuwa wagonjwa wanaolazwa wamepungua kwa kiasi kikubwa na zile ambazo watu wake wamechanja wachache, mfano nchi za Afrika uchanjaji upo asilimia mbili maambukizi yanaendelea kuongezeka, lazima tupigwe tu," alisema.

Waziri huyo alisema wakati wa kuchanja kuna madhara madogo kama ilivyo kwa dawa zote za binadamu zilivyo na madhara. "Kuna madhara kama kusikia kizunguzungu, kichefuchefu unatakiwa kupumzika na kunywa maji mengi na kazi iendelee," alisema.

Alisema chanjo bilioni 3.6 zimeshatolewa kwa wananchi duniani kote na zimesaidia kupunguza makali ya ugonjwa huo, kupunguza wagonjwa wanaolazwa, vifo na ufanisi wa kudhibiti virusi.

Alisema Rais Samia ameapa kutumikia taifa na yeye ameapa, hivyo haiwezekani kuleta chanjo ambayo inawadhuru Watanzania.

Katika hatua nyingine, Chama cha ACT-Wazalendo kimeitaka serikali kutoa elimu ya kina juu ya umuhimu wa chanjo ya corona iliyoletwa nchini ili kuepusha upotoshaji kuhusu chanjo hiyo unaoenezwa na baadhi ya watu nchini na kusababisha hofu miongoni mwa wananchi. Naibu Katibu Idara ya Habari na Mawasiliano ya Ngome ya Vijana wa ACT-Wazalendo, Julius Masabo, aliwaambia waandishi wa habari mkoani Dar es Salaam jana kuwa ni muhimu serikali kutoa elimu kuhusu chanjo ya corona ili kuepusha upotoshaji.

"Hizi kauli za kuwapotosha watu wasiende kuchanja zinatokana na ukosefu wa elimu kuhusu njia za kisayansi za kupambana na ugonjwa huu," alisema.

Aliongeza kuwa serikali inapaswa kuhakikisha upatikanaji wa chanjo unakuwa wa uhakika nchini ili kuwafikia wananchi wengi zaidi. Alisema chama chao pia kinaona kuna haja serikali kuwekeza katika utafiti wa chanjo ili ijitegemee katika chanjo yake binafsi kwa kushirikiana na nchi zenye ujuzi na utaalamu wa juu katika masuala ya utafiti ili kupunguza utegemezi kwa mataifa mengine. Julai 24, mwaka huu, serikali ilipokea dozi 1,058,400 za chanjo ya UVIKO-19 kutoka Serikali ya Marekani kupitia mpango wa Covax, unaolenga kusaidia nchi zinazoendelea katika kukabiliana na janga hilo.

■**Imendaliwa na Mary Geofrey, Haika Christopher na Sechellah Nakamba (SJMC).**

# Samia asema ni uamuzi mgumu

**Na Mary Geofrey**

RAIS Samia Suluhu Hassan, amewaongoza viongozi mbalimbali wa serikali, vyombo vya ulinzi na usalama na dini kupata chanjo ya UVIKO-19 huku akiweka bayana kuwa amefikia uamuzi mgumu kwake kupata chanjo hiyo.

Mkuu wa nchi huyo ametaja vigezo sita alivyovizingatia kufikia uamuzi wake wa kuchanja.

Amesema hawezi kuhatarisha maisha yake huku akijua anaongoza kundi kubwa la watu wanaomtegemea akiwa kama Rais, Amiri Jeshi Mkuu, mchungaji wa Watanzania, mama wa watoto wanne, mke na bibi wa wajukuu kadhaa.

Rais Samia alichoma chanjo hiyo aina ya Johnson & Johnson kwenye bega lake la kushoto jana majira ya saa 5:36 asubuhi Ikulu jijini Dar es Salaam mbele ya viongozi mbalimbali wa serikali, huku tukio hilo likirushwa mubashara na vyombo vya habari.

"Nategemewa kama mama wa watoto wanne, kama bibi wa wajukuu kadhaa, kama mke, kama Rais, kama Amiri Jeshi Mkuu lakini nimetoka kuonyesha umma wanaonifuata nyuma na nikijua kwamba Rais ni mchungaji, nina watu wengi ninaowachunga na wao wananitizama nyuma, kwa hiyo nisingetoka kujihatarishia kifo," alisema Rais Samia.

Alisisitiza kuwa amekubali kwa hiari yake kuchanja, akitambua kuwa alishachanja chanjo tano ndani ya mwili ambazo ameendelea kuishi nazo kwa miaka 61 bila madhara yoyote.

"Tanzania hatuishi peke yetu, tunaishi na mataifa mengine, hivyo hatuwezi kuishi kwa kujitenga na dunia inavyoenda," alisema Rais Samia.

Alisema haoni hatari ya kuchanja ilhali wanasayansi wa nje na ndani ya nchi wameshajiridhisha kuwa chanjo hiyo ni salama.

Hata hivyo, Rais Samia aliwataka Watanzania watakaochanja, wasijiachie kwa sababu wako karibu na watu ambao hawajachanja.

"Lakini niwahakikishieni Watanzania tutafanya jitihada na wale wote ambao wapo tayari kuchanja tutahakikisha chanjo zinapatikana," alisema Rais Samia.

Alisema kwa Watanzania ambao familia zao hazijakumbwa na ugonjwa huo, ni rahisi kupinga chanjo hiyo lakini kwa wale waliogusw a wanatamani kuchanjwa haraka.

"Nenda Kilimanjaro, Arusha, Mwanza na Kagera ukakutane na koo za waliogusw a na janga hili, wanatamani hata leo hii wangechanja," alisisitiza.

Rais Samia aliwaomba Watanzania wasivunjane moyo bali waendelee kutiana moyo katika kukabiliana na janga hilo lililoikumba dunia.

Alisema mbali na kuanza uchanjaji rasmi jana nchini, lipo kundi la watu wengi ambao wameshachanja katika nchi mbalimbali duniani kwa sababu wangeshindwa kuendelea na biashara zao na ndiyo sababu serikali imeamua kuleta chanjo hiyo.

Alisema zipo jumuiya za mataifa mbalimbali ziliomba kuleta chanjo za nchi zao na waliruhusiwa kuzileta na ndiyo sababu serikali imeona umuhimu wa kuleta chanjo hiyo.

Alisema kwa kushirikiana na Umoja wa Afrika (AU), nchi wanachama wanajipanga kukabiliana na janga hilo na kununua chanjo zao na kuuzia nchi nyingine.

Alisema tayari serikali imeshaagiza chanjo tangu juzi kutoka AU ambazo zinazalishwa Afrika Kusini.

"Naendelea kusisitiza kuwa chanjo ni hiari ya mtu lakini pia ni imani ya mtu," alisisitiza Rais Samia.

Alisema wakati akiwa mdogo, wazee walikuwa wanapinga watoto kuchanja kwa madai watapata madhara lakini walichanja kwa lazima na ingawa madhara yalikuwapo, lakini walibaki salama.

Rais Samia pia alilitaka Shirika la Utangazaji (TBC) kuendelea kuucheza wimbo wa uhamasishaji ulioimbwa na wasanii jana mbele yake ili kuendelea kutoa elimu kwa jamii kuhusu chanjo.

Mbali na Rais Samia, viongozi wengine waliochanjwa jana ni pamoja na Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, Jaji Mkuu, Prof. Ibrahim Juma, Katibu Mkuu Kiongozi, Hussen Katanga, viongozi wa vyombo vya ulinzi na usalama na viongozi wa dini.



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa akipatiwa chanjo ya Covid-19, katika Viwanja vya Ikulu, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: IKULU**

# Askofu awakemea wanaopinga chanjo

**Na Hamisi Nasri, MASASI**

ASKOFU wa Kanisa la Anglikana Dayosisi ya Masasi mkoani Mtwara, Dk. James Almasi, amekemea baadhi ya viongozi wa dini wanaotoa kauli za kupinga chanjo ya corona.

Licha ya kukemea, amesema wamekosa ajenda ya msingi kuhusu maendeleo ya taifa lao na kwamba watu hao wana dhamira ya kuhujumu mipango ya maendeleo inayotekelezwa na serikali.

Aliyasema hayo jana mjini hapa alipokuwa akizungumza na Nipashe katika mahojiano maalumu ofisi kwake juu ya hatua za kujikinga na virusi vya ugonjwa wa corona sambamba na kutekeleza mwongozo wa serikali uliotolewa hivi karibuni.

Dk. Almasi alisema corona ni ugonjwa hatari ambao umeendelea kuathiri mataifa mengi duniani ikiwa ni pamoja na kushusha uchumi wa dunia, hivyo mpango wa serikali ya Tanzania kuleta chanjo milioni moja na kuwahamasisha wananchi kujitokeza kuchanjwa kwa hiari ni jambo jema linalolenga kuokoa maisha ya wananchi.

Alisema Tanzania ni kama nchi zingine, hivyo inapaswa kuchukua hatua mbalimbali za kujikinga na corona ili kunusuru wananchi wake na kuhakikisha wanakuwa na afya bora.

Kiongozi huyo wa kiroho alisema baadhi ya viongozi wa dini ambao wamejitokeza na kauli za kupinga chanjo pamoja na kushawishi wananchi wasijitokeze kuchanjwa kwa madai kuwa chanjo hizo hazina uhakika kama zimefanyiwa utafiti wa kutosha, wana nia ya kuhujumu maendeleo ya nchi.

Alisema Watanzania wasikubali kupoteza muda wao wa kufanya kazi za maendeleo na kukaa kuanza kujadili suala la chanjo kuwa hazijafanyiwa utafiti wa kutosha na kwamba hakuna sababu ya kuchanja hadi pale watakapohakikishiwa kuwa zimefanyiwa utafiti na hazitakuwa na madhara.

Dk. Almasi aliwaonya baadhi ya viongozi wa dini nchini wanaotumia sehemu ya ibada kugeuza kuwa uwanja wa mkutano wa adhara na kuzungumza na siasa au kupinga maendeleo ya nchi badala ya kutumia sehemu hizo kumwomba Mungu aendelee kuliokoa taifa.

Askofu Almasi alisema Watanzania wajitokeza kwa wingi kuchanja na kuondoa hofu ambayo wanapewa na baadhi ya watu kuwa chanjo hizo huenda zikawa na madhara makubwa baadaye baada ya mtu kuchanja.

# Shahidi adai Sabaya alitishia kumuua

**Na Allan Isack,** ARUSHA

SHAHIDI wa sita wa upande wa Jamhuri, Bakari Raibu Msangi(38), ameangua kilio mahakamani wakati akiendelea kutoa ushahidi wake, akidai kuwa aliyekuwa Mkuu wa Wilaya ya Hai, Lengai Ole Sabaya (34), alimpa kipigo kizito na kumshikia bastola akitishia kumuua.

Shahidi huyo, ambaye ni Diwani wa Sombetini jijini Arusha kupitia Chama Cha Mapinduzi (CCM), alitoa madai hayo jana mbele ya Hakimu Mkazi Mwandamizi, Odira Amworo.

Pia alieleza alivyowekwa chini ya ulinzi, kuteswa, kupigwa na kuporwa simu na Sh.390,000 na Ole Sabaya akishirikiana na walinzi wake.

Mbali na Ole Sabaya washtakiwa wenzake ni Sylvester Nyegu (26) na Daniel Mbura (38) ambao wote wanakabiliwa na mashtaka matatu ya unyang'anyi wa kutumia silaha.

Akihojiwa na Wakili Mkuu wa Serikali, Tumaini Kweka, shahidi huyo alidai kuwa baada ya kipigo kizito alitolewa dukani na kupelekwa kwenye gari la Sabaya na alipongia ndani ya gari, alifungwa pingu mikononi na miguuni.

"Niliingizwa kwenye gari la Sabaya nikiwa chini ya ulinzi nimefungwa pingu. Nilikuwa mimi, dereva wa gari hilo na mlinzi mmoja," alidai na kuongeza kuwa mmoja wa walinzi wa Sabaya alimwuliza anafahamu ni kitu gani alichokosea.

"Nilimwambia mnachokifanya ni kama utekaji nyara na huyo mlinzi aliniambia kwa nini nimekwenda kuingilia dili ya General Sabaya na alisema salama yangu ni hadi hapo nitakapomwonyesha alipokuwa mmiliki wa duka, Mohamed Saad.

"Mlinzi aliniambia kwamba hata udiwani wangu utakuwa matatani huku akisema hata Mkuu wa Wilaya ya Arusha, Kenani Kihongosi pia aliniambia kwamba alishawahi kumweka ndani ndugu yangu Meya wa Manispaa ya Moshi," alidai.

Shahidi huyo pia alidai kwamba Sabaya alitoa bastola tena kumtishia kwa madai kwamba alikuwa anafuatilia mambo yake,

"Nilimwambia Sabaya umeshanitesha vya kutosha na kunidhalilisha naomba niache. Aliniambia kwa nini nafuatilia mambo yake na alisema bila kumwonyesha alipokuwa Mohamed Saad na Ally Saad na sehemu wanapobadilishia dola hawezi kuniachia.

"Baada ya hapo, Sabaya alifungua sanduku dogo la kuweka vitu kwenye gari akanionyesha koleo, pingu na vitu vingine akaniambia vitu hivyo vitaniishia kwenye mwili wangu.

"Sabaya alimwambia dereva wake mwambie huyu, katika nchi mimi pekee ndiye kiongozi naweza kuzungumza na Hayati Rais John Magufuli huku akijipiga kifua,"alidai.

Baada ya hapo, alidai kuwa magari yaliondoka eneo hilo na alimwambia kuna baadhi ya nyumba za Mohamed Saad na Ally Saad anazifahamu, hivyo zile ambazo hazifahamu akamwonyeshe.

"Baada ya kufika kwenye duka la Hajirini, gari liliwashwa tukaondoka eneo la Kwa Benson na tulipofika eneo la Amana Bank akaniuliza nafahamu nyumba yao inayoitwa Muhajirin iliyoko karibu na standi kuu ya mabasi ya Arusha nilimjibu ndiyo.

"Tulipotoka hapo, tulielekea eneo la Kaloleni na aliniuliza tena jengo la Said Kondo ni la kina Mohamed Saad na Ally Saad nikamwambia hapana na baada ya hapo aliniambia niwapeleke anapoishi Ally Saad na tulipofika walipaki gari."

Msangi alidai walipofika sehemu anapoishi Ally Saad, Sabaya aliagiza walinzi wake wamfungue pingu ya miguuni na walimshusha kwenye gari wakaenda getini kwa mhusika.

"Walinishusha kwenye gari Sabaya aliniambia niende kwenye geti la Ally na nifanye niwezavyo ili wafungue mlango lakini niligonga sana hawakufungua na mmoja wa walinzi walisogea karibu yangu baada ya kuona mlango haufunguliwi akaanza kusukuma geti hilo.

"Aliniambia nikishindwa kuhakikisha geti linafunguliwa bahati yangu itakuwa mbaya kwa kuwa watanifanya kitu kibaya na wakati tukio hilo likiendelea ilikuwa majira ya saa nne usiku," alidai.

Baada ya mizunguko ya kutafuta nyumba za watu hao kukamilika, alidai kuwa Sabaya aliagiza gari kuwashwa walipofika eneo la Kaloleni, Sabaya aliangalia simu yake na kuanza kufurahia.

"Alianza kushangilia kwa kusema safi sana huyu Salumu Hamduni, RPC Arusha sasa amehamishwa aende makao makuu akapumzike pamoja na askari polisi wengine aliohamishwa nao akiwamo Wambura. Sabaya pale ndani ya gari alisema kwamba yeye ndiye alitoa maelekezo hayo kwa Rais Magufuli watu hao wahamishwe," alidai.

Shahidi huyo alidai baada ya kutoka eneo la Kaloleni, walielekea pembeni ya geti la kuingilia Hospitali ya Mount, Sabaya na mlinzi wake mmoja walishuka kwenda kuonana na mtu mmoja waliokuwa wakimsubiri.

"Baada ya sisi kufika polisi niliona gari lingine likiingia hapo, walishushwa watu wawili Hajirini na Numan, mimi nikiwa kwenye gari la Sabaya aliniambia hawawezi kunishusha kituoni watacheza na mimi hadi hapo nitakapowaonyesha watu wanaowahitaji. "Baada ya kutoka kituoni hapo aliniambia niwapeleke hadi nyumbani kwa Mohamed Saad Hajirini na walipofike eneo hilo, waliwakuta walinzi wawili na akamwita mmoja akajitambulisha kuwa ni DC wa Hai na alimueleza kwamba alikwenda hapo kwa kazi maalumu aliyotumwa na Rais John Magufuli, hivyo aliowaomba kumpa ushirikiano kwa kuwa anataka kumuona Mohamed Saad Hajirini,

"Walinzi waliwapeleka hadi nyumbani kwa mhusika. Walipofika huko nilisikia kama mlango ukivunjwa na wanawake waliokuwa wanaishi eneo hilo walianza kupiga ukunga na baada ya muda Sabaya na walinzi wake, walishuka ngazi za ghorofa kuondoka eneo hilo.

"Tulipotoka hapo tulielekea eneo la Sakina Tulia Lodge, kwa kuwa kuna watu Sabaya alikuwa anakwenda kuwaona. General alipokuwa anazungumza na watu hao, Mkuu wa Kituo cha Polisi Wilaya ya Hai pia nikiwa ndani ya gari nilimwona yule dada aliyekwenda dukani kununua bidhaa alizotaka kulipia kwa dola akienda kuonana na Sabaya. Mmoja wa walinzi(Andrew), na dereva walinipa simu yangu nikampigia simu mke wangu kumueleza juu ya tukio hilo,

---

**Bank of India (Tanzania) Ltd.**

*Relationship beyond banking*

**Fully owned subsidiary of Bank of India (Public Sector Bank)**

## UONESHAJI WA TAARIFA ZA FEDHA KWA UMMA

### IMETOLEWA CHINI YA KANUNI YA 7 NA YA 8 YA KANUNI ZA MABENKI NA TAASISI ZA FEDHA (UONESHAJI) YA MWAKA 2014

**WARAKA MIZANIA KWA TAREHE 30 JUNI 2021**
(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | Robo Mwaka ya sasa 30-Jun-21 | Robo Mwaka iliyopita 31-Mar-21 |
|---|---|---|---|
| A. | **MALI** | | |
| 1 | Fedha Taslimu | 1,251 | 778 |
| 2 | Salio Katika Benki Kuu ya Tanzania | 18,179 | 14,823 |
| 3 | Uwekezaji Katika Amana za Serikali | 47,181 | 48,793 |
| 4 | Salio Katika Benki Nyingine na Taasisi za Fedha | 1,901 | 977 |
| 5 | Hundi na Miamala ya Kushughulikiwa | - | - |
| 6 | Miamala Baina ya Matawi | - | - |
| 7 | Bili Zilizoafikiwa | - | - |
| 8 | Dhima za Wateja Zilizokubalika | - | - |
| 9 | Mikopo Iliyotolewa kwa Benki Nyingine | 19,271 | 19,846 |
| 10 | Uwekezaji Katika Amana Nyingine | - | - |
| 11 | Mikopo Halisi Iliyopo | 71,137 | 72,504 |
| 12 | Mali Nyingine | 1,976 | 3,024 |
| 13 | Uwekezaji wa Hisa | - | - |
| 14 | Akaunti za udhamini | - | - |
| 15 | Mali Zisizohamishika, Mitambo na Vifaa | 1,717 | 2,081 |
| 16 | **JUMLA YA MALI** | **162,613** | **162,826** |
| B. | **B. DHIMA** | | |
| 17 | Amana za Benki nyingine na Taasisi za Fedha | 52,673 | 53,146 |
| 18 | Amana za Wateja | 70,042 | 69,231 |
| 19 | Dhamana ya Malipo kwa Fedha Taslimu | - | - |
| 20 | Amana Maalumu | - | - |
| 21 | Maagizo ya Malipo/Fedha za Kuhamisha | 65 | 89 |
| 22 | Hundi na Hawala za Kibenki Zilizotolewa | 25 | 25 |
| 23 | Limbiko la Kodi na Gharama Zitakazolipwa | 2,543 | 2,340 |
| 24 | Dhima la Tozo kwa Ajili ya Usuluhishi Baina ya Benki na Mteja | - | - |
| 25 | Miamala Isiyoshughulikiwa Baina ya Matawi | - | - |
| 26 | Mapato yaliyoingia ya Kipindi Kijacho na Tozo Nyingine Zitakazolipwa Baadae | - | - |
| 27 | Dhima Nyingine | 1,119 | 1,477 |
| 28 | Madeni | - | - |
| 29 | **JUMLA YA DHIMA** | **126,467** | **126,308** |
| 30 | **MALI/(DHIMA) HALISI *(16 kutoa 29)*** | **36,146** | **36,518** |
| C. | **FEDHA ZA WANAHISA** | | |
| 31 | Mtaji wa Hisa Uliolipwa | 21,500 | 21,500 |
| 32 | Akiba ya Mtaji | 2,222 | 2,570 |
| 33 | Mapato Yaliyobakizwa | 12,269 | 11,908 |
| 34 | Faida (Hasara) ya Kipindi Husika | 155 | 540 |
| 35 | Akaunti Nyingine za Mtaji | - | - |
| 36 | Stahiki ya Wenyehisa Chache | - | - |
| 37 | **JUMLA YA FEDHA ZA WANAHISA** | **36,146** | **36,518** |
| 38 | Dhima Zisizo Dhahiri | 8,467 | 8,764 |
| 39 | Mikopo Chechefu | 2,607 | 2,609 |
| 40 | Tengo kwa Ajili ya Mikopo Chechefu | 586 | 220 |
| 41 | Mali Nyingine Chechefu | - | - |
| D. | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA HALI YA KIFEDHA** | | |
| (i) | Uwiano wa Fedha za Wanahisa na Jumla ya Mali | 22.23% | 22.43% |
| (ii) | Uwiano wa Mikopo Chechefu na Jumla ya Mikopo Ghafi | 3.63% | 3.59% |
| (iii) | Uwiano wa Mikopo Ghafi na Jumla ya Amana | 58.45% | 59.43% |
| (iv) | Uwiano wa Mikopo Halisi na Jumla ya Mali | 43.75% | 44.53% |
| (v) | Uwiano wa Mali Zinazozalisha na Jumla ya Mali | 84.97% | 86.82% |
| (vi) | Ongezeko la Amana | 0.28% | 0.71% |
| (vii) | Ongezeko la Mali | -0.13% | 0.60% |

**TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 30 JUNI 2021**
(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | Robo ya Mwaka wa sasa 30-Jun-21 | Robo ya mwaka Linganishi (Mwaka Uliopita) 30-Jun-20 | Limbikizo la Mwaka wa sasa 30-Jun-21 | Limbikizo la Mwaka Linganishi (Mwaka Uliopita) 30-Jun-20 |
|---|---|---|---|---|
| 1 Mapato ya Riba | 2,528 | 3,102 | 5,602 | 6,210 |
| 2 Gharama za Riba | 1,149 | 1,221 | 2,380 | 2,493 |
| 3 **Mapato Halisi ya Riba (1kutoa 2)** | **1,379** | **1,881** | **3,222** | **3,717** |
| 4 Madeni Viza Yaliyofutwa | - | 7 | - | 7 |
| 5 Punguzo/Ongezeko la tengo katika Mikopo | 367 | 376 | 391 | 679 |
| 6 **Mapato Yasiyo ya Riba:** | **143** | **126** | **260** | **299** |
| 6.1 Faida /(Hasara) Zitokanazo na Miamala ya Fedha za | 45 | 52 | 85 | 109 |
| 6.2 Ada na Kamisheni | 98 | 74 | 175 | 190 |
| 6.3 Gawio | - | - | - | - |
| 6.4 Mapato Mengine | - | - | - | - |
| 7 **Gharama Zisizo za Riba:** | **1,322** | **1,024** | **2,498** | **2,188** |
| 7.1 Mishahara na Mafao | 504 | 430 | 991 | 861 |
| 7.2 Ada na Kamisheni | - | - | - | - |
| 7.3 Gharama Nyingine | 818 | 594 | 1,507 | 1,327 |
| 8 **Faida /(Hasara) ya Uendeshaji** | **(167)** | **600** | **593** | **1,142** |
| 9 Tengo la Kodi ya Mapato | 219 | 269 | 438 | 537 |
| 10 **Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato** | **(386)** | **331** | **155** | **605** |
| 11 **Mapato Mengine Yaliyojumuishwa (bainisha)** | - | - | - | - |
| 12 **Jumla ya Faida (Hasara) iliyojumuishwa kwa robo ya** | **(386)** | **331** | **155** | **605** |
| 13 Idadi ya Waajiriwa | 30 | 29 | 30 | 29 |
| 14 Mapato kwa Hisa | (72) | 62 | 14 | 56 |
| 15 Idadi ya Matawi | 2 | 2 | 2 | 2 |
| **BAADHI YA VIASHIRIO VYA UFANISI** | | | | |
| (i) Uwiano wa Faida Kabla ya Kodi na Wastani wa Mali | -0.41% | 1.55% | 0.73% | 1.49% |
| (ii) Wanahisa | -4.25% | 3.69% | 0.84% | 3.38% |
| (iii) Uwiano wa Matumizi Yasiyo ya Riba na Mapato Ghafi | 49.49% | 31.72% | 42.61% | 33.62% |
| (iv) Zinazozalisha | 4.04% | 5.83% | 4.70% | 5.71% |

**TAARIFA YA MABADILIKO YA MTAJI KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 30 JUNI 2021**

| | Mtaji wa Hisa | Malipo Juu ya bei ya Hisa | Mapato Yaliyobakizwa | Ziada ya Kisheria | Tengo la Ziada ya Jumla | Mengineyo (Bainisha) | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Robo mwaka ya sasa 2021** | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa robo mwaka 01.04.2021** | **21,500** | - | **12,447** | **2,571** | - | - | **36,518** |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | (386) | - | - | - | **(386)** |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Ziada ya Kisheria | - | - | 348 | (348) | - | - | - |
| Tengo la Ziada ya Jumla | - | - | - | - | - | - | - |
| Mikopo iliyofutwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Mengineyo | | | 15 | | | | **15** |
| **Salio la mwisho wa robo mwaka 30.06.2021** | **21,500** | - | **12,424** | **2,222** | - | - | **36,146** |
| **Robo Mwaka iliyopita 2020** | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa robo mwaka 01.01.2021** | **21,500** | - | **12,012** | **2,479** | - | - | **35,991** |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | 540 | - | - | - | **540** |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Ziada ya Kisheria | - | - | (92) | 92 | - | - | - |
| Tengo la Ziada ya Jumla | - | - | - | - | - | - | - |
| Mikopo iliyofutwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Mengineyo | - | - | (13) | - | - | - | **(13)** |
| **Salio la mwisho wa robo mwaka 31.03.2021** | **21,500** | - | **12,447** | **2,571** | - | - | **36,518** |

**TAARIFA YA MTIRIRIKO WA FEDHA KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 30 JUNI 2021**
(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | Robo Mwaka ya sasa 30-Jun-21 | Robo Mwaka iliyopita 31-Mar-21 | Limbikizo la Mwaka wa sasa 30-Jun-21 | Limbikizo la Mwaka Linganishi (Mwaka Uliopita) 30-Jun-20 |
|---|---|---|---|---|---|
| I: | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uendeshaji:** | | | | |
| | Mapato/(Hasara) Halisi | (167) | 759 | 593 | 1,142 |
| | Marekebisho kwa Ajili ya: | - | - | - | - |
| | - Hasara Katika Mali | 605 | 208 | 740 | 797 |
| | - Badiliko Halisi Katika Mikopo | 2,432 | (961) | 2,903 | (2,770) |
| | - Faida/Hasara Kwenye Mauzo ya Mali | - | - | - | - |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Amana | 338 | 868 | 1,206 | 7,050 |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Amana za Muda Mfupi Zilizoafikiwa | (1,603) | 1,069 | (534) | (1,969) |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Dhima Nyingine | 92 | (421) | (205) | (1,090) |
| | -Mabadiliko Halisi Katika Mali Nyingine | 3,411 | 2,032 | 3,960 | 155 |
| | - Kodi Iliyolipwa | (219) | (219) | (438) | (886) |
| | - Mengineyo (bainisha) | - | - | - | - |
| | ***Fedha Halisi zilizotolewa (zilizotumika) kwa shughuli za*** | ***4,890*** | ***3,335*** | ***8,225*** | ***2,429*** |
| II: | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uwekezaji:** | | | | |
| | Gawio Lililopokewa | - | - | - | - |
| | Ununuzi wa Mali za Kudumu | (167) | (3) | (170) | (5) |
| | Mapato Kutokana na Mauzo ya Mali za Kudumu | - | - | - | - |
| | Ununuzi wa Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | - | - | - |
| | Mapato Kutokana na Mauzo ya Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | - | - | - |
| | Mengineyo (bainisha) | - | - | - | - |
| | ***Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Uwekezaji*** | ***(167)*** | ***(3)*** | ***(170)*** | ***(5)*** |
| III: | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Kifedha:** | | | | |
| | Ulipaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - | - | - |
| | Mapato Kutokana na Utoaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - | - | - |
| | Mapato Kutokana na Utoaji wa Mtaji wa Hisa | - | - | - | - |
| | Gawio Lililolipwa kwa Fedha Taslimu | - | - | - | - |
| | Mabadiliko Halisi Katika Madeni Mengine | - | - | - | - |
| | Mengineyo (bainisha) | - | - | - | - |
| | ***Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Kifedha*** | - | - | - | - |
| IV: | **Fedha Taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu:** | | | | |
| | **Ongezeko / Punguzo Halisi Katika Fedha taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu** | **4,723** | **3,332** | **8,055** | **2,424** |
| | Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwanzoni mwa Robo Mwaka | 35,872 | 32,540 | 32,540 | 23,432 |
| | **Robo Mwaka** | **40,595** | **35,872** | **40,595** | **25,856** |

**BAADHI YA MAELEZO KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 30 JUNI 2021**

Katika kuandaa taarifa za hizi za fedha, sera za uandaaji ni zilezile zilizotumika wakati wa uandaaji wa Taarifa za Fedha zilizokaguliwa za mwaka uliopita.

| Jina na Cheo | Saini | Tarehe |
|---|---|---|
| Mr. Ashwani Kumar Negi<br>Mkurugenzi Mkuu | | 20.07.2021 |
| Mr. Heriabdiel Ayoh<br>Meneja Usimamizi | | 20.07.2021 |
| Mr. Allen Richard<br>Mkaguzi Mkuu wa Ndani | | 20.07.2021 |

Sisi, tuliotajwa hapo chini, wajumbe wa bodi ya wakurugenzi, tunathibitisha usahihi wa taarifa za hapo juu, tunatamka kwamba tumezitathmini taarifa hizi, na kwa uelewa na imani yetu kubwa zimeandaliwa kulingana na Viwango vya Kimataifa vya Uwasilishaji wa Taarifa za Fedha na matakwa ya Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha ya mwaka 2006, na zinaonesha hali halisi.

| Jina | Saini | Tarehe |
|---|---|---|
| 1. Mr. Suitbert Kageuka - Mkurugenzi | | 20.07.2021 |
| 2. Dr. Paul Kato - Mkurugenzi | | 20.07.2021 |

216379301

# TANGAZO

# UONESHAJI WA TAARIFA ZA FEDHA KWA UMMA

**Imetolewa chini ya kanuni ya 7 na ya 8 ya Kanuni za Mabenki na Taasisi za Fedha (Uoneshaji) ya Mwaka 2014**

AKIBA COMMERCIAL BANK PLC
*benki kwa maendeleo yako*

## AKIBA COMMERCIAL BANK PLC
## WARAKA MIZANIA KWA TAREHE 30.06.2021
(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | Robo Mwaka Mwaka wa sasa 30-Jun-21 | Robo Mwaka Mwaka uliopita 31-Mar-21 |
|---|---|---|---|
| **A.** | **MALI** | | |
| 1 | Fedha Taslimu | 13,251 | 9,949 |
| 2 | Salio Katika Benki Kuu ya Tanzania | 21,904 | 29,636 |
| 3 | Uwekezaji Katika Amana za Serikali | 29,000 | 25,850 |
| 4 | Salio Katika Benki Nyingine na Taasisi za Fedha | 3,999 | 84 |
| 5 | Hundi na Miamala ya Kushughulikiwa | 88 | 46 |
| 6 | Miamala Baina ya Matawi | 18 | 17 |
| 7 | Bili Zilizoafikiwa | 0 | 0 |
| 8 | Dhima za Wateja Zilizokubalika | 0 | 0 |
| 9 | Mikopo Iliyotolewa kwa Benki Nyingine | 0 | 0 |
| 10 | Uwekezaji Katika Amana Nyingine | 0 | 0 |
| 11 | Mikopo Halisi Iliyopo | 73,106 | 73,572 |
| 12 | Mali Nyingine | 12,905 | 11,844 |
| 13 | Uwekezaji wa Hisa | 39 | 39 |
| 14 | Akaunti za udhamini | 0 | 0 |
| 15 | Mali Zisizohamishika, Mitambo na Vifaa | 18,135 | 18,766 |
| **16** | **JUMLA YA MALI** | **172,443** | **169,803** |
| **B.** | **DHIMA** | | |
| 17 | Amana za Benki nyingine na Taasisi za Fedha | 606 | 909 |
| 18 | Amana za Wateja | 121,946 | 118,324 |
| 19 | Dhamana ya Malipo kwa Fedha Taslimu | 0 | 0 |
| 20 | Amana Maalumu | 25 | 0 |
| 21 | Maagizo ya Malipo/Fedha za Kuhamisha | 0 | 0 |
| 22 | Hundi na Hawala za Kibenki Zilizotolewa | 1 | 1 |
| 23 | Limbiko la Kodi na Gharama Zitakazolipwa | 3,757 | 3,047 |
| 24 | Dhima la Tozo kwa Ajili ya Usuluhishi Baina ya Benki na Mteja | 0 | 0 |
| 25 | Miamala Isiyoshughulikiwa Baina ya Matawi | 0 | 0 |
| 26 | Mapato yaliyoingia ya Kipindi Kijacho na Tozo Nyingine Zitakazol | 8,500 | 8,220 |
| 27 | Dhima Nyingine | 12,750 | 12,748 |
| 28 | Madeni | 690 | 679 |
| **29** | **JUMLA YA DHIMA** | **148,276** | **143,928** |
| **30** | **MALI/(DHIMA) HALISI** *(16 kutoa 29)* | **24,167** | **25,875** |
| **C.** | **FEDHA ZA WANAHISA** | | |
| 31 | Mtaji wa Hisa Uliolipwa | 22,411 | 22,543 |
| 32 | Akiba ya Mtaji | 0 | 0 |
| 33 | Mapato Yaliyobakizwa | (6,852) | (5,634) |
| 34 | Faida (Hasara) ya Kipindi Husika | (4,298) | (2,604) |
| 35 | Akaunti Nyingine za Mtaji | 12,906 | 11,571 |
| 36 | Stahiki ya Wenyehisa Chache | 0 | 0 |
| **37** | **JUMLA YA FEDHA ZA WANAHISA** | **24,167** | **25,875** |
| 38 | Dhima Zisizo Dhahiri | 61 | 83 |
| 39 | Mikopo Chechefu | 15,996 | 15,488 |
| 40 | Tengo kwa Ajili ya Mikopo Chechefu | 8,904 | 8,352 |
| 41 | Mali Nyingine Chechefu | 73 | 73 |
| **D.** | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA HALI YA KIFEDHA** | | |
| (i) | Uwiano wa Fedha za Wanahisa na Jumla ya Mali | 14.0% | 15.2% |
| (ii) | Uwiano wa Mikopo Chechefu na Jumla ya Mikopo Ghafi | 19.0% | 18.6% |
| (iii) | Uwiano wa Mikopo Ghafi na Jumla ya Amana | 66.8% | 68.5% |
| (iv) | Uwiano wa Mikopo Halisi na Jumla ya Mali Halisi | 48.7% | 49.1% |
| (v) | Uwiano wa Mali Zinazozalisha na Jumla ya Mali | 61.5% | 58.6% |
| (vi) | Ongezeko la Amana | 2.8% | -0.5% |
| (vii) | Ongezeko la Mali | 1.6% | 0.0% |

## AKIBA COMMERCIAL BANK PLC
## TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI
## KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 30.06.2021
(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | Robo ya Mwaka sasa 30-Jun-21 | Robo ya mwaka Linganishi 30-Jun-20 | Limbikizo la Mwaka wa sasa 30-Jun-21 | Limbikizo la Mwaka Linganishi 30-Jun-20 |
|---|---|---|---|---|
| 1 Mapato ya Riba | 5,796 | 5,835 | 11,815 | 12,385 |
| 2 Gharama za Riba | (2,177) | (2,026) | (4,349) | (3,709) |
| 3 **Mapato Halisi ya Riba (1kutoa 2)** | **3,619** | **3,809** | **7,467** | **8,677** |
| 4 Madeni Viza Yaliyofutwa | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 5 Punguzo/Ongezeko la tengo katika Mikopo | (552) | (2,251) | (1,989) | (2,374) |
| 6 **Mapato Yasiyo ya Riba**: | **1,401** | **1,153** | **2,553** | **2,470** |
| 6.1 Faida /(Hasara) Zitokanazo na Miamala ya Fedha za Kigeni | 89 | 61 | 153 | 134 |
| 6.2 Ada na Kamisheni | 924 | 803 | 1,693 | 1,801 |
| 6.3 Gawio | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 6.4 Mapato Mengine | 388 | 289 | 708 | 535 |
| 7 **Gharama Zisizo za Riba:** | **(6,163)** | **(6,037)** | **(12,329)** | **(12,476)** |
| 7.1 Mishahara na Mafao | (3,052) | (3,267) | (6,155) | (6,582) |
| 7.2 Ada na Kamisheni | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 7.3 Gharama Nyingine | (3,111) | (2,769) | (6,174) | (5,894) |
| 8 **Faida /(Hasara) ya Uendeshaji** | **(1,694)** | **(3,326)** | **(4,298)** | **(3,704)** |
| 9 Tengo la Kodi ya Mapato | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 10 **Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato** | **(1,694)** | **(3,326)** | **(4,298)** | **(3,704)** |
| 11 **Mapato Mengine Yaliyojumuishwa (bainisha)** | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 12 **Jumla ya Faida (Hasara) iliyojumuishwa kwa mwaka** | **(1,694)** | **(3,326)** | **(4,298)** | **(3,704)** |
| 13 Idadi ya Waajiriwa | 414 | 420 | 414 | 450 |
| 14 Mapato kwa Hisa | (76) | (303) | (192) | (337) |
| 15 **Idadi ya Matawi** | **18** | **18** | **18** | **18** |
| **BAADHI YA VIASHIRIO VYA UFANISI** | | | | |
| (i) Uwiano wa Faida Kabla ya Kodi na Wastani wa Mali | -4.0% | -8% | -5.0% | -5% |
| (ii) Uwiano wa Faida baada ya Kodi na Wastani wa Fedha za Wanahisa | -27.1% | -69% | -34.4% | -39% |
| (iii) Uwiano wa Matumizi Yasiyo ya Riba na Mapato Ghafi | 122.8% | 122% | 123.0% | 112% |
| (iv) Uwiano wa Mapato Halisi ya Riba na Wastani wa Mali Zinazozalisha | 14.1% | 15% | 14.5% | 17% |

## TAARIFA YA MTIRIRIKO WA FEDHA
## KWA ROBO/MWAKA ULIOISHIA 30.06.2021
(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | Robo Mwaka ya sasa 30-Jun-21 | Robo Mwaka iliyopita 31-Mar-21 | Limbikizo la Mwaka wa sasa 30-Jun-21 | Limbikizo la Mwaka Linganishi 30-Jun-20 |
|---|---|---|---|---|
| **I: Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uendeshaji:** | | | | |
| Mapato/(Hasara) Halisi | (1,694) | (2,604) | (4,298) | (3,704) |
| Marekebisho kwa Ajili ya: | 0 | 0 | 0 | 0 |
| - Hasara Katika Mali | 596 | 630 | 1,226 | 1,468 |
| - Badiliko Halisi Katika Mikopo | 465 | 4,132 | 4,597 | 9,350 |
| - Faida/Hasara Kwenye Mauzo ya Mali | 0 | 0 | 0 | 0 |
| - Mabadiliko Halisi Katika Amana | 3,344 | (581) | 2,763 | 1,152 |
| - Mabadiliko Halisi Katika Amana za Muda Mfupi Zilizoafikiwa | (3,150) | (3,080) | (6,230) | 3,670 |
| - Mabadiliko Halisi Katika Dhima Nyingine | 1,337 | (960) | 3,967 | (10,932) |
| -Mabadiliko Halisi Katika Mali Nyingine | (1,060) | (535) | (1,595) | (1,688) |
| - Kodi Iliyolipwa | (124) | 0 | (124) | (416) |
| - Mengineyo (bainisha) | (222) | (127) | (349) | 1,496 |
| ***Fedha Halisi zilizotolewa (zilizotumika) kwa shughuli za uendeshaji*** | **(509)** | **(3,125)** | **(43)** | **396** |
| **II: Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uwekezaji:** | | | | |
| Gawio Lililopokewa | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Ununuzi wa Mali za Kudumu | (121) | (76) | (198) | (69) |
| Mapato Kutokana na Mauzo ya Mali za Kudumu | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Ununuzi wa Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Mapato Kutokana na Mauzo ya Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Mengineyo (bainisha) | 0 | 0 | 0 | (0) |
| ***Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Uwekezaji*** | **(121)** | **(76)** | **(198)** | **(69)** |
| **III: Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Kifedha:** | | | | |
| Ulipaji wa Madeni ya Muda Mrefu | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Mapato Kutokana na Utoaji wa Madeni ya Muda Mrefu | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Mapato Kutokana na Utoaji wa Mtaji wa Hisa | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Gawio Lililolipwa kwa Fedha Taslimu | (0) | 0 | (0) | (2) |
| Mabadiliko Halisi Katika Madeni Mengine | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Mengineyo (bainisha) | (65) | (390) | (455) | (1,701) |
| **Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Kifedha** | **(65)** | **(390)** | **(455)** | **(1,703)** |
| **IV: Fedha Taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu:** | | | | |
| Ongezeko / Punguzo Halisi Katika Fedha taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu | (696) | (3,591) | (696) | (1,376) |
| Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwanzoni mwa Robo Mwaka/Mwaka | 32,668 | 36,259 | 32,668 | 18,624 |
| **Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwishoni mwa Robo Mwaka/Mwaka** | **31,972** | **32,668** | **31,972** | **17,248** |

## AKIBA COMMERCIAL BANK PLC
## TAARIFA YA MABADILIKO YA MTAJI KWA KIPINDI KINACHOISHIA 30.06.2021

| | Mtaji wa Hisa | Malipo juu ya bei ya hisa | Mapato Yaliyobakizwa | Ziada ya Kisheria | Tengo la Ziada ya Jumla | Mengineyo | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Mwaka wa sasa** | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa mwaka 01.01.2021** | **10,984,416** | **2,431,917** | **(5,626,989)** | **3,683,694** | **0** | **16,992,072** | **28,465,109** |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | 0 | 0 | (4,298,492) | 0 | 0 | 0 | **(4,298,492)** |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | **0** |
| Miamala na wanahisa | 11,426,798 | 5,565,274 | 0 | 0 | 0 | (16,992,072) | **(0)** |
| Gawio lililolipwa | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | **0** |
| Ziada ya Kisheria | 0 | 0 | (1,225,352) | 1,225,352 | 0 | 0 | **(0)** |
| Tengo la Ziada ya Jumla | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | **0** |
| Mengineyo | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | **0** |
| **Salio la mwisho wa mwaka 30.06.2021** | **22,411,214** | **7,997,190** | **(11,150,833)** | **4,909,046** | **0** | **(0)** | **24,166,617** |
| **Mwaka Uliopita** | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa mwaka 01.01.2020** | **10,984,416** | **2,431,917** | **4,687,639** | **3,286,944** | **0** | **0** | **21,390,916** |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapa | 0 | 0 | (3,703,790) | 0 | 0 | 0 | **(3,703,790)** |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | **0** |
| Miamala na wanahisa | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | **0** |
| Gawio lililolipwa | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | **0** |
| Ziada ya Kisheria | 0 | 0 | (1,514,439) | 1,514,439 | 0 | 0 | **(0)** |
| Tengo la Ziada ya Jumla | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | **0** |
| Mengineyo | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | **0** |
| **Salio la mwisho wa mwaka 30.06.2020** | **10,984,416** | **2,431,917** | **(530,589)** | **4,801,382** | **0** | **0** | **17,687,126** |

## BAADHI YA MAELEZO KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 30.06.2021

Katika kuanda taarifa za hizi za fedha, sera za uandaaji ni zilizile zilizotumika wakati wa uandaaji wa Taarifa za Fedha zilizokaguliwa za mwaka uliopita. Kwa robo mwaka iliyoishia Juni 30, 2021 Bank iliadhibiwa kwa kiasi cha shilling Milioni 10 kwa kutotekeleza miongozo iliyowekwa na Bank kuu ya Tanzania.

**Jina na Cheo** — **Saini** — **Tarehe**

Juliana Swai
**(Kaimu Mtendaji Mkuu)**

Bertha Simon
**(Mkuu wa Fedha)**

Chemo Mutani
**(Mkaguzi Mkuu wa Ndani)**

Sisi, tuliotajwa hapo chini, wajumbe wa bodi ya wakurugenzi, tunathibitisha usahihi wa taarifa za hapo juu, tunatamka kwamba tumezitathmini taarifa hizi, na kwa uelewa na imani yetu kubwa zimeandaliwa kulingana na Viwango vya Kimataifa vya Uwasilishaji wa Taarifa za Fedha na matakwa ya Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha ya mwaka 2006, na zinaonesha hali halisi.

**Jina** — **Saini** — **Tarehe**

1. Ernest Massawe
2. Dr. Josephat Daniel Lotto

216380201




# TANGAZO



# TAARIFA ZA FEDHA KWA UMMA - NMB BANK PLC

Imetolewa chini ya kanuni ya 7 na ya 8 ya Kanuni za Mabenki na Taasisi za Fedha (Uoneshaji) ya Mwaka 2014

NMB Karibu yako

**Trilioni 4.2** Mikopo Halisi Iliyopo **+11% YoY**

**Trilioni 5.8** Amana za Wateja **+8% YoY**

Jumla ya Mali **Trilioni 7.6** **+6% YoY**

Uwiano wa Mikopo Chechefu na Jumla ya Mikopo Ghafi **4.3%**

**Faida** kabla ya Kodi ya Mapato **Bilioni 192** **+44% YoY**

**Faida** Baada ya Kodi ya Mapato **Bilioni 134** **+43% YoY**

Uwiano wa Matumizi yasiyo ya Riba na Mapato Ghafi **47%**

*YoY - Linganishi mwaka kwa mwaka

## WARAKA MIZANIA KWA TAREHE 30 JUNI 2021

(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | KUNDI | | BENKI | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | Robo Mwaka ya sasa 30.06.2021 | Robo Mwaka iliyopita 31.03.2021 | Robo Mwaka ya sasa 30.06.2021 | Robo Mwaka iliyopita 31.03.2021 |
| **A.** | **MALI** | | | | |
| 1 | Fedha Taslimu | 405,346 | 470,009 | 405,346 | 470,009 |
| 2 | Salio Katika Benki Kuu ya Tanzania | 1,008,328 | 529,551 | 1,008,328 | 529,551 |
| 3 | Uwekezaji Katika Amana za Serikali | 1,345,548 | 1,207,987 | 1,345,548 | 1,207,987 |
| 4 | Salio Katika Benki Nyingine na Taasisi za Fedha | 157,223 | 142,592 | 157,223 | 142,592 |
| 5 | Hundi na Miamala ya Kushughulikiwa | 10,259 | 3,956 | 10,259 | 3,956 |
| 6 | Miamala Baina ya Matawi | 1,045 | 2,384 | 1,045 | 2,384 |
| 7 | Bili Zilizoafikiwa | - | - | - | - |
| 8 | Dhima za Wateja Zilizokubalika | - | - | - | - |
| 9 | Mikopo Iliyotolewa kwa Benki Nyingine | 47,642 | 46,514 | 47,642 | 46,514 |
| 10 | Uwekezaji Katika Amana Nyingine | - | - | - | - |
| 11 | Mikopo Halisi Iliyopo | 4,229,306 | 4,130,048 | 4,229,706 | 4,130,448 |
| 12 | Mali Nyingine | 205,543 | 200,389 | 283,074 | 274,379 |
| 13 | Uwekezaji wa Hisa | 2,920 | 2,920 | 2,920 | 2,920 |
| 14 | Akaunti za udhamini | - | - | - | - |
| 15 | Mali Zisizohamishika, Mitambo na Vifaa | 198,949 | 207,893 | 165,781 | 174,232 |
| **16** | **JUMLA YA MALI** | **7,612,109** | **6,944,243** | **7,656,872** | **6,984,972** |
| **B.** | **DHIMA** | | | | |
| 17 | Amana za Benki nyingine na Taasisi za Fedha | 57,203 | 57,131 | 57,203 | 57,131 |
| 18 | Amana za Wateja | 5,843,527 | 5,188,989 | 5,845,671 | 5,192,578 |
| 19 | Dhamana ya Malipo kwa Fedha Taslimu | 80,489 | 30,874 | 80,489 | 30,874 |
| 20 | Amana Maalumu | 12,113 | 6,301 | 12,113 | 6,301 |
| 21 | Maagizo ya Malipo/Fedha za Kuhamisha | - | - | - | - |
| 22 | Hundi na Hawala za Kibenki Zilizotolewa | 2,118 | 2,121 | 2,118 | 2,121 |
| 23 | Limbiko la Kodi na Gharama Zitakazolipwa | 61,277 | 57,879 | 60,663 | 57,723 |
| 24 | Dhima la Tozo kwa Ajili ya Usuluhishi Baina ya Benki na Mteja | - | - | - | - |
| 25 | Miamala Isiyoshughulikiwa Baina ya Matawi | - | - | - | - |
| 26 | Mapato yaliyoingia ya Kipindi Kijacho na Tozo Nyingine Zitakazolipwa Baadaye | 37,994 | 37,470 | 37,994 | 37,470 |
| 27 | Dhima Nyingine | 66,175 | 64,660 | 112,482 | 103,870 |
| 28 | Madeni | 253,337 | 302,620 | 253,337 | 302,620 |
| **29** | **JUMLA YA DHIMA** | **6,414,233** | **5,748,045** | **6,462,070** | **5,790,688** |
| **30** | **MALI/(DHIMA) HALISI (16 kutoa 29)** | **1,197,876** | **1,196,198** | **1,194,802** | **1,194,284** |
| **C.** | **FEDHA ZA WANAHISA** | | | | |
| 31 | Mtaji wa Hisa Uliolipwa | 20,000 | 20,000 | 20,000 | 20,000 |
| 32 | Akiba ya Mtaji | - | - | - | - |
| 33 | Mapato Yaliyobakizwa | 1,037,941 | 1,106,441 | 1,040,642 | 1,109,142 |
| 34 | Faida (Hasara) ya Kipindi Husika | 135,503 | 65,387 | 133,640 | 64,684 |
| 35 | Akaunti Nyingine za Mtaji | 520 | 458 | 520 | 458 |
| 36 | Stahiki ya Wenyehisa Chache | 3,912 | 3,912 | - | - |
| **37** | **JUMLA YA FEDHA ZA WANAHISA** | **1,197,876** | **1,196,198** | **1,194,802** | **1,194,284** |
| 38 | Dhima Zisizo Dhahiri | 770,686 | 654,587 | 770,686 | 654,587 |
| 39 | Mikopo Chechefu | 191,412 | 216,506 | 191,412 | 216,506 |
| 40 | Tengo kwa Ajili ya Mikopo Chechefu | 214,660 | 209,527 | 214,660 | 209,527 |
| 41 | Mali Nyingine Chechefu | 12,974 | 9,058 | 12,974 | 9,058 |
| **D.** | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA HALI YA KIFEDHA** | | | | |
| (i) | Uwiano wa Fedha za Wanahisa na Jumla ya Mali | 16% | 17% | 16% | 17% |
| (ii) | Uwiano wa Mikopo Chechefu na Jumla ya Mikopo Ghafi | 4.3% | 5.0% | 4.3% | 5.0% |
| (iii) | Uwiano wa Mikopo Ghafi na Jumla ya Amana | 74% | 82% | 74% | 82% |
| (iv) | Uwiano wa Mikopo Halisi na Jumla ya Mali Halisi | 56% | 59% | 55% | 59% |
| (v) | Uwiano wa Mali Zinazozalisha na Jumla ya Mali | 75% | 79% | 75% | 79% |
| (vi) | Ongezeko la Amana | 13% | -3% | 13% | -3% |
| (vii) | Ongezeko la Mali | 10% | -2% | 10% | -2% |

## TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 30 JUNI 2021

(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | KUNDI | | BENKI | | KUNDI | | BENKI | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Robo ya Mwaka sasa 30.06.2021 | Robo ya mwaka Linganishi (Mwaka Uliopita) 30.06.2020 | Robo ya Mwaka sasa 30.06.2021 | Robo ya mwaka Linganishi (Mwaka Uliopita) 30.06.2020 | Limbikizo la Mwaka wa sasa 30.06.2021 | Limbikizo la Mwaka Linganishi (Mwaka Uliopita) 30.06.2020 | Limbikizo la Mwaka wa sasa 30.06.2021 | Limbikizo la Mwaka Linganishi (Mwaka Uliopita) 30.06.2020 |
| 1 | Mapato ya Riba | 196,030 | 168,635 | 196,030 | 168,735 | 386,799 | 334,657 | 386,799 | 334,888 |
| 2 | Gharama za Riba | (30,497) | (34,317) | (30,497) | (34,317) | (63,356) | (66,914) | (63,356) | (66,914) |
| **3** | **Mapato Halisi ya Riba (1kutoa 2)** | **165,533** | **134,318** | **165,533** | **134,418** | **323,443** | **267,743** | **323,443** | **267,974** |
| 4 | Madeni Viza Yaliyofutwa | - | - | - | - | - | - | - | - |
| 5 | Punguzo/Ongezeko la tengo katika Mikopo | (30,169) | (26,598) | (30,169) | (26,598) | (53,039) | (48,445) | (53,039) | (48,445) |
| **6** | **Mapato Yasiyo ya Riba:** | **74,228** | **59,274** | **74,228** | **59,274** | **139,915** | **119,046** | **139,915** | **119,046** |
| | 6.1 Faida /(Hasara) Zitokanazo na Miamala ya Fedha za Kigeni | 7,293 | 5,655 | 7,293 | 5,655 | 12,867 | 11,472 | 12,867 | 11,472 |
| | 6.2 Ada na Kamisheni | 60,166 | 51,116 | 60,166 | 51,116 | 115,987 | 101,287 | 115,987 | 101,287 |
| | 6.3 Gawio | - | 17 | - | 17 | - | 17 | - | 17 |
| | 6.4 Mapato Mengine | 6,769 | 2,486 | 6,769 | 2,486 | 11,061 | 6,270 | 11,061 | 6,270 |
| **7** | **Gharama Zisizo za Riba:** | **(109,339)** | **(101,944)** | **(110,500)** | **(103,028)** | **(216,373)** | **(202,400)** | **(218,236)** | **(204,907)** |
| | 7.1 Mishahara na Mafao | (57,127) | (50,834) | (57,127) | (50,834) | (113,590) | (101,351) | (113,590) | (101,351) |
| | 7.2 Ada na Kamisheni | (3,613) | (1,092) | (3,613) | (1,092) | (7,161) | (3,571) | (7,161) | (3,571) |
| | 7.3 Gharama Nyingine | (48,599) | (50,018) | (49,760) | (51,102) | (95,622) | (97,478) | (97,485) | (99,985) |
| **8** | **Faida /(Hasara) ya Uendeshaji** | **100,253** | **65,050** | **99,092** | **64,066** | **193,946** | **135,944** | **192,083** | **133,668** |
| 9 | Tengo la Kodi ya Mapato | (30,137) | (19,220) | (30,137) | (19,220) | (58,443) | (40,100) | (58,443) | (40,100) |
| **10** | **Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato** | **70,116** | **45,830** | **68,955** | **44,846** | **135,503** | **95,844** | **133,640** | **93,568** |
| 11 | **Mapato Mengine Yaliyojumuishwa** | | | | | | | | |
| | **Faida/(Hasara) uthamanishaji Dhamana za Kuuzwa** | **62** | **(955)** | **62** | **(955)** | **(272)** | **(932)** | **(272)** | **(932)** |
| | **Jumla ya Faida (Hasara) iliyojumuishwa kwa mwaka** | **70,178** | **44,875** | **69,017** | **43,891** | **135,231** | **94,912** | **133,368** | **92,636** |
| 12 | Idadi ya Waajiriwa | 3,473 | 3,445 | 3,473 | 3,445 | 3,473 | 3,445 | 3,473 | 3,445 |
| 13 | Mapato kwa Hisa | 140 | 92 | 138 | 90 | 271 | 192 | 267 | 187 |
| 14 | Idadi ya Matawi | 225 | 226 | 226 | 226 | 226 | 226 | 226 | 226 |
| | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA UFANISI** | | | | | | | | |
| (i) | Uwiano wa Faida Kabla ya Kodi na Wastani wa Mali | 4% | 3% | 4% | 3% | 4% | 3% | 4% | 3% |
| (ii) | Uwiano wa Faida baada ya Kodi na Wastani wa Fedha za Wanahisa | 23% | 18% | 23% | 17% | 23% | 19% | 22% | 18% |
| (iii) | Uwiano wa Matumizi Yasiyo ya Riba na Mapato Ghafi | 46% | 53% | 46% | 53% | 47% | 52% | 47% | 53% |
| (iv) | Uwiano wa Mapato Halisi ya Riba na Wastani wa Mali Zinazozalisha | 11% | 11% | 12% | 11% | 11% | 11% | 12% | 11% |

## TAARIFA YA MTIRIRIKO WA FEDHA KWA ROBO/MWAKA ULIOISHIA 30 JUNI 2021

(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | KUNDI | | BENKI | | KUNDI | | BENKI | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Robo Mwaka ya sasa 30.06.2021 | Robo Mwaka iliyopita 31.03.2021 | Robo Mwaka ya sasa 30.06.2021 | Robo Mwaka iliyopita 31.03.2021 | Limbikizo la Mwaka wa sasa 30.06.2021 | Limbikizo la Mwaka Linganishi (Mwaka Uliopita) 30.06.2020 | Limbikizo la Mwaka wa sasa 30.06.2021 | Limbikizo la Mwaka Linganishi (Mwaka Uliopita) 30.06.2020 |
| **I: Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uendeshaji:** | | | | | | | | |
| Mapato/(Hasara) Halisi | 100,253 | 93,693 | 99,092 | 92,990 | 193,946 | 135,942 | 192,082 | 133,667 |
| Marekebisho kwa Ajili ya: | | | | | | | | |
| - Hasara Katika Mali | 10,038 | 9,869 | 9,545 | 9,377 | 19,907 | 24,019 | 18,922 | 23,034 |
| - Badiliko Halisi Katika Mikopo | (100,386) | (67,773) | (100,386) | (67,702) | (168,159) | (232,589) | (168,088) | (229,950) |
| - Faida/Hasara Kwenye Mauzo ya Mali | - | - | - | - | - | - | - | - |
| - Mabadiliko Halisi Katika Amana | 710,037 | (173,379) | 708,592 | (169,795) | 536,658 | 617,723 | 538,797 | 614,873 |
| - Mabadiliko Halisi Katika Amana za Muda Mfupi Zilizoafikiwa | - | - | - | - | - | - | - | - |
| - Mabadiliko Halisi Katika Dhima Nyingine | 5,434 | (36,762) | 12,074 | (38,675) | (31,328) | 14,758 | (26,601) | 11,477 |
| -Mabadiliko Halisi Katika Mali Nyingine | (11,876) | 3,728 | (15,417) | 3,181 | (8,148) | (52,876) | (12,236) | (46,124) |
| - Kodi Iliyolipwa | (29,475) | (26,436) | (29,475) | (26,436) | (55,911) | (62,111) | (55,911) | (62,111) |
| - Mengineyo (bainisha) | (31,866) | 9,296 | (31,866) | 9,296 | (22,570) | 32,037 | (22,570) | 32,037 |
| **Fedha Halisi zilizotolewa (zilizotumika) kwa shughuli za uendeshaji** | **652,159** | **(187,764)** | **652,159** | **(187,764)** | **464,395** | **476,903** | **464,395** | **476,903** |
| **II. Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uwekezaji:** | | | | | | | | |
| Gawio Lililopokewa | - | - | - | - | - | - | - | - |
| Ununuzi wa Mali za Kudumu | (1,756) | (3,919) | (1,756) | (3,919) | (5,675) | (9,011) | (5,675) | (9,011) |
| Mapato Kutokana na Mauzo ya Mali za Kudumu | - | - | - | - | - | - | - | - |
| Ununuzi wa Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | - | - | - | - | - | - | - |
| Mapato Kutokana na Mauzo ya Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | - | - | - | - | - | - | - |
| Mengineyo (bainisha) | (137,499) | 95,934 | (137,499) | 95,934 | (41,565) | (206,986) | (41,565) | (206,986) |
| **Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Uwekezaji** | **(139,255)** | **92,015** | **(139,255)** | **92,015** | **(47,240)** | **(215,997)** | **(47,240)** | **(215,997)** |
| **III: Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Kifedha:** | | | | | | | | |
| Ulipaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - | - | - | - | - | - | - |
| Mapato Kutokana na Utoaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - | - | - | - | - | - | - |
| Mapato Kutokana na Utoaji wa Mtaji wa Hisa | - | - | - | - | - | - | - | - |
| Gawio Lililolipwa kwa Fedha Taslimu | (68,500) | - | (68,500) | - | (68,500) | (48,000) | (68,500) | (48,000) |
| Mabadiliko Halisi Katika Madeni Mengine | (49,283) | (21,120) | (49,283) | (21,120) | (70,403) | 27,997 | (70,403) | 27,997 |
| Mengineyo (bainisha) | - | - | - | - | - | - | - | - |
| **Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Kifedha** | **(117,783)** | **(21,120)** | **(117,783)** | **(21,120)** | **(138,903)** | **(20,003)** | **(138,903)** | **(20,003)** |
| **IV: Fedha Taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu:** | | | | | | | | |
| **Ongezeko/Punguzo Halisi Katika Fedha taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu** | **395,121** | **(116,869)** | **395,121** | **(116,869)** | **278,252** | **240,903** | **278,252** | **240,903** |
| Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwanzoni mwa Robo Mwaka/Mwaka | 790,160 | 907,029 | 790,160 | 907,029 | 907,029 | 1,213,370 | 907,029 | 1,213,370 |
| **Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwishoni mwa Robo Mwaka/Mwaka** | **1,185,281** | **790,160** | **1,185,281** | **790,160** | **1,185,281** | **1,454,273** | **1,185,281** | **1,454,273** |

## TAARIFA YA KUNDI YA MABADILIKO YA MTAJI KWA KIPINDI KINACHOISHIA 30 JUNI 2021

(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | Mtaji wa Hisa | Malipo juu ya bei ya hisa | Mapato Yaliyobakizwa | Ziada ya Kisheria | Tengo la Ziada ya Jumla | Mengineyo (Uthamanishaji Amana za Kuuzwa) | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Mwaka wa sasa 2021** | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa mwaka** | **20,000** | - | **1,106,441** | - | - | **4,704** | **1,131,145** |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | 135,503 | - | - | - | 135,503 |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | (272) | (272) |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | (68,500) | - | - | - | (68,500) |
| Ziada ya Kisheria | - | - | - | - | - | - | - |
| Tengo la Ziada ya Jumla | - | - | - | - | - | - | - |
| Mengineyo | - | - | - | - | - | - | - |
| **Salio la mwisho wa mwaka** | **20,000** | - | **1,173,444** | - | - | **4,432** | **1,197,876** |
| **Mwaka Uliopita 2020** | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa mwaka** | **20,000** | - | **944,473** | - | - | **4,630** | **969,103** |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | 95,844 | - | - | - | 95,844 |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | (932) | (932) |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | (48,000) | - | - | - | (48,000) |
| Ziada ya Kisheria | - | - | - | - | - | - | - |
| Tengo la Ziada ya Jumla | - | - | - | - | - | - | - |
| Mengineyo | - | - | - | - | - | - | - |
| **Salio la mwisho wa mwaka** | **20,000** | - | **992,317** | - | - | **3,698** | **1,016,015** |

## TAARIFA YA BENKI YA MABADILIKO YA MTAJI KWA KIPINDI KINACHOISHIA 30 JUNI 2021

(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | Mtaji wa Hisa | Malipo juu ya bei ya hisa | Mapato Yaliyobakizwa | Ziada ya Kisheria | Tengo la Ziada ya Jumla | Mengineyo (Uthamanishaji Amana za Kuuzwa) | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Mwaka wa sasa 2021** | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa mwaka** | **20,000** | - | **1,109,142** | - | - | **792** | **1,129,934** |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | 133,640 | - | - | - | 133,640 |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | (272) | (272) |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | (68,500) | - | - | - | (68,500) |
| Ziada ya Kisheria | - | - | - | - | - | - | - |
| Tengo la Ziada ya Jumla | - | - | - | - | - | - | - |
| Mengineyo | - | - | - | - | - | - | - |
| **Salio la mwisho wa mwaka** | **20,000** | - | **1,174,282** | - | - | **520** | **1,194,802** |
| **Mwaka Uliopita 2020** | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa mwaka** | **20,000** | - | **951,341** | - | - | **1,049** | **972,390** |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | 93,568 | - | - | - | 93,568 |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | (932) | (932) |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | (48,000) | - | - | - | (48,000) |
| Ziada ya Kisheria | - | - | - | - | - | - | - |
| Tengo la Ziada ya Jumla | - | - | - | - | - | - | - |
| Mengineyo | - | - | - | - | - | - | - |
| **Salio la mwisho wa mwaka** | **20,000** | - | **996,909** | - | - | **117** | **1,017,026** |

## BAADHI YA MAELEZO KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA JUNI 2021

**Katika kuandaa taarifa hizi za fedha, sera za uandaaji ni zile zilizotumika wakati wa uandaaji wa Taarifa za Fedha zilizokaguliwa za mwaka uliopita.**

| Jina na Cheo | Saini | Tarehe |
|---|---|---|
| Ruth Zaipuna<br>**Afisa Mtendaji Mkuu** | | 23/07/2021 |
| Juma Kimori<br>**Afisa Mkuu wa Fedha** | | 23/07/2021 |
| Benedicto Baragomwa<br>**Kaimu Mkaguzi Mkuu wa Ndani** | | 23/07/2021 |

Sisi, tuliotajwa hapo chini, wajumbe wa bodi ya wakurugenzi, tunathibitisha usahihi wa taarifa za hapo juu, tunatamka kwamba tumezitathmini taarifa hizi, na kwa uelewa na imani yetu kubwa zimeandaliwa kulingana na Viwango vya Kimataifa vya Uwasilishaji wa Taarifa za Fedha na matakwa ya Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha ya mwaka 2014, na zinaonesha hali halisi. Taarifa hizi za fedha zimekaguliwa na PricewaterhouseCoopers, Certified Public Accountants (T), na kupokea taarifa huru ya uhakiki wa ukaguzi.

| Jina na Cheo | Saini | Tarehe |
|---|---|---|
| Dr. Edwin P. Mhede<br>**Mwenyekiti wa Bodi** | | 23/07/2021 |
| Leonard Mususa<br>**Mkurugenzi** | | 23/07/2021 |

www.nmbbank.co.tz

216379602

## MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Tumuunge mkono Samia kupata chanjo ya corona

**HATIMAYE** Tanzania imeingia rasmi katika orodha ya mataifa duniani yaliyoanza kuchukua hatua ya kuwapa chanjo raia wake kuwakinga dhidi ya maambukizi ya ugonjwa wa Covid-19 unaosababishwa na virusi vya corona.

Jana, Samia Suluhu Hassan, aliwaongoza viongozi mbalimbali wa serikali, vyombo vya ulinzi na usalama na dini kupata chanjo hiyo, huku akitaja vigezo sita vilivyomfanya achanje.

Amesema hawezi kuhatarisha maisha yake, huku akijua anaongoza kundi kubwa la watu wanaomtegemea akiwa kama Rais, Amiri Jeshi Mkuu , mama, bibi, mke na mchungaji wa Watanzania.

Rais Samia alichoma chanjo aina ya Johnson & Johnson kwenye bega la kushoto saa 5:56 asubuhi Ikulu jijini Dar es Salaam, mbele ya viongozi mbalimbali wa serikali, huku tukio hilo likirushwa mubashara na vyombo mbalimbali vya habari.

Rais alisema Tanzania haiwezi kupuuza chanjo hiyo kwa kuwa hatuishi peke yetu, tunaishi na mataifa mengine hivyo hatuwezi kuishi kwa kujitenga na dunia inavyoenda, na kwamba haoni hatari ya kuchanja ilihali wanasayansi wa nje na ndani ya nchi wameshajiridhisha kuwa chanjo hiyo ni salama.

Tukio hilo sasa limefungua milango kwa Watanzania kuitumia fursa hiyo kuchanjwa, lengo likiwa ni kujilinda dhidi ya gonjwa hilo hatari, ambalo hadi sasa limeua mamilioni ya watu duniani na wengine wakiugua.

Aidha, gonjwa hilo limeathiri uchumi wa kila taifa, kutokana na shughuli za uzalishaji zikiwamo za viwandani kusimama au kupungua kwa kiwango kikubwa.

Sababu alizozieleza Rais Samia hapo juu kwamba ndizo zilizomsukuma achukue uamuzi wa kuchanja unamshawishi kila Mtanzania mwenye akili timamu na mzalendo kwa nchi yake kuelewa na kumuunga mkono.

Kumuunga mkono maana yake ni kukubali kwenda kupata chanjo hiyo katika vituo vya huduma za afya ambavyo mamlaka husika zitavitolea maelekezo.

Tunawahimiza na kuwasisitiza wananchi wote wabadili mitazamo yao kwa kukubali kupewa chanjo hiyo kwa lengo la kujilinda na kuwalinda wengine, huku pia wakiendelea kuchukua hatua za tahadhari dhidi ya maambukizi ya corona.

Tunasema hivyo kwa kuwa kuna baadhi ya watu wamekuwa wakitoa kauli za upotoshaji kuhusu chanzo za Covid-19 kwamba zina madhara kwa binadamu, hivyo kuwajaza hofu ya kuchanjwa.


Maelezo yanayoendelea kutolewa na wataalamu wa afya, yakiwamo yaliyotolewa naja wakati wa hafla ya uzinduzi wa chanjo hiyo yanadhihirisha bila kuacha shaka yoyote kuhusu usalama, ubora na umuhimu wa chanjo.

Ushauri wetu ni kwamba wananchi wawapuuze wale wote wanaotoa kauli za kuwapotosha kwa kuwa madhara ya corona yanaonekana katika maeneo kadhaa ya nchi.

Kadhalika, tunawahimiza kuzingatia wito wa Rais Samia wa kuwataka Watanzania watakaochanja wasijiachie kwa sababu wapo watu ambao hawajachanja.

Tunatarajia kuona shughuli za kutoa elimu ya corona na uhamasishaji wananchi kuchanja zikifanyika kwa kasi kubwa kupitia uratibu wa Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto. Itakuwa vyema kama viongozi wa dini nao wataelimisha waumini wao na kuwahimiza kupata chanjo.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com



## Muungwana Lazima Nilonge



Na Mashaka Mgeta

# Hakika Rais Samia yu 'Mchungaji Mwema' kwa vitendo, jamani tufuate aliyonena

**ALIPOKUWA** anazindua Mpango wa Chanjo ya Uviko 19 kwa Watanzania jana, Rais Samia Suluhu, amezungumzia mambo kadhaa yanayouaminisha umma kuhusu usalama uliopo kwenye chanjo hiyo.

Kauli ya Rais Samia, imekuja kutokana na kauli za baadhi ya watu, wanaoonyesha wasiwasi juu ya usalama wa chanjo hiyo, pengine kutokana na ama ukosefu au upungufu wa taarifa sahihi, walizo nazo hasa zinazotokana na kuenezwa kupitia mitandao ya kijamii.

Ni uzinduzi uliofanyika Ikulu ya Magogoni, jijini Dar es Salaam, Rais Samia akiweka wazi kwamba ana majukumu makuu yanayomkabili akiwa mama wa familia, mke, mlezi wa wajukuu.

Pia kiserikali ana wasifu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, akiwa na dhamana ya Amiri Jeshi Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi na Usalama.

Anajitambulisha kuwa na watoto na wajukuu anaowapenda sana, kama vile nao wanavyompenda na kumtegemea katika maisha yao. Ameyasema hayo huku 'lugha ya picha' ikionyesha jinsi Rais Samia anamaanisha kuhusu jambo hilo.

Upande mwingine, Rais Samia akasema anayatambua majukumu yake katika ngazi hizo, ikiwamo ya urais ambayo inamfanya kuwa mfano wa mchungaji anayewaongoza Watanzania, hivyo hawezi kuruhusu jambo lisilokuwa na tija liwafikie Watanzania.

Hotuba fupi ya Rais Samia kuhusu chanjo hiyo, imebeba ujumbe mzito unaopaswa kuwatoa hofu wananchi, badala yake wanapaswa kuunga mkono ili Tanzania iwe sehemu ya dunia inayolenga kudhibiti kasi ya maambukizi ya virusi vya corona.

Rais Samia akijitaja kuwa 'Mchungaji' wa Watanzania, nami ninawiwa kumtaja kuwa 'Mchungaji Mwema'. Kwanini? Niseme, anatimiza vyema wajibu wake katika kutambua 'kiu' ya watu anaowachunga, kisha akawaonea huruma wasiendelee kuteseka katika kadhia inayowakabili. Hapa inamaanisha madhara ya Uviko 19.

Ni wazi kwamba, Watanzania wengi wameguswa kwa namna tofauti kutokana na athari za Uviko 19. Lakini, kwa walioguswa moja kwa moja, wanatambua umuhimu wa kulidhibiti janga hilo. Udhibiti wa Uviko 19 ni miongoni mwa 'kiu' ya Watanzania ambayo Rais Samia aliye 'Mchungaji Mwema' ameitambua.

Utambuzi huo ndio unamsukuma Rais Samia, kuwaonea huruma Watanzania kwa kadhia zinazotokana na athari za Uviko 19, na hivyo kuruhusu matumizi ya chanjo hiyo, huku akiongoza uzinduzi wake uliofanyika Ikulu ya Magogoni jijini Dar es Salaam jana.

Hiyo inachukua nafasi kuidhihirishia dunia kwamba, chanjo hiyo haina madhara pasipo shaka yoyote. Rais Samia kachanjwa hadharani, huku akiungwa mkono na watu mashuhuri, wakiwamo viongozi wakuu wa dini, wakuu wa vyombo vya ulinzi na usalama, viongozi waandamizi, wa kiserikali hadi ngazi ya wilaya, wasanii na engine wenye mapenzi mema.

Kwa namna yoyote ile, Watanzania wanapaswa kuondokana na taarifa potofu, badala yake wazipate na kuzitumia taarifa sahihi zitakazowawezesha kufanya uamuzi sahihi kwa maisha yao.

Taarifa sahihi ni zinazotoka kwenye vyanzo sahihi, kama zilivyotolewa kwenye hotuba ya Rais Samia kuhusu ukweli wa chanjo yenye kudhibiti maambukizi ya Uviko 19.

Kwa mukhtadha huo, Rais Samia ametimiza wajibu wake akiwa Rais na Amiri Jeshi Mkuu; ametimiza wajibu wake akiwa mama wa familia;. ametimiza wajibu wake akiwa mlezi wa wajukuu; ametimiza wajibu wake akiwa mke; na ametimiza wajibu wake kama Mchungaji aliyeshika fimbo mkononi, akiwaongoza Watanzania.

Ni hiari kwa kila Mtanzania kutumia akili na utashi kufanya uamuzi sahihi katika kushiriki mpango wa kupata chanjo ya Uviko 19, na kwa namna iwayo yote, uamuzi sahihi ni kushiriki chanjo hiyo pasipo hofu ama hisia hasi.

Wakati hamasa ikiwa katika kushiriki chanjo hiyo, Watanzania wanapaswa kuendelea kuchukua hatua zote zinazoshauriwa na watalaamu katia kudhibiti maambukizi ya Uviko 19, ikiwamo kuvaa barakoa, kunawa mikono kwa maji tiririka, kutumia vitakasa mikono na kadhalika. Kwa pamoja tutashinda dhidi ya Uviko 19!

■ **Mwandishi ni Katibu Tawala wa Wilaya ya Handeni mkoani Tanga na anapatikana kwa simu: 0754691540 au barua pepe: mgeta2000@yahoo.com.**

# Watoto kortini tuhuma kughushi saini ya baba

**Na Kulwa Mzee**

WATOTO watano wa familia moja, wamefikishwa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu kwa tuhuma za kughushi saini ya baba yao katika kuhamisha umiliki wa ardhi.

Washtakiwa hao walifikishwa mbele ya Hakimu Mkazi Mwandamizi, Joseph Lwambano, na kusomewa mashtaka na Wakili Neema Mushi.

Akisoma mashtaka hayo, Wakili Mushi aliwataja washtakiwa kuwa ni Saidi Athumani, Tufaa Athumani, Fatuma Athumani, Amal Athumani na Nimiit Athumani.

Washtakiwa wanadaiwa kula njama kutenda kosa Agosti mwaka 2016, Mtaa wa Lumumba wilayani Ilala.

Inadaiwa katika kipindi hicho, kwa nia ya kudanganya, walighushi saini ya Ally Athumani wakionyesha ilikuwa halali na ilitolewa na Ally Athumani wakati siyo kweli.

Wakili Mushi alidai katika kipindi hicho washtakiwa walighushi saini ya baba yao katika uhamisho wa umiliki wa ardhi wakionyesha hayo yalifanywa na Ally Athumani wakati siyo kweli.

Upande wa Jamhuri ulidai upelelezi wa kesi hiyo haujakamilika, hivyo kesi kuahirishwa hadi Agosti 11, mwaka huu kwa kutajwa.

Mahakama ilitoa masharti ya dhamana ambapo kila mshtakiwa alitakiwa kuwa na wadhamini wawili wa kuaminika, wanne wakifanikiwa kupata dhamana huku mshtakiwa wa kwanza aliyeshindwa kutimiza masharti ya kuwa na wadhamini wawili.

Katika hatua nyingine, mbele ya Hakimu Ritha Tarimo, mshtakiwa Frank Mahelela alisomewa mashtaka ya wizi akiwa mtumishi.

Inadaiwa kati ya Mei 28, mwaka 2019 na Septemba 30, 2019, maeneo ya Ofisi ya Kimataifa ya Wahamiaji iliyoko Masaki, akiwa mhasibu, aliiba Dola za Marekani 156,000 sawa na Sh. milioni 358.8, mali ya mwajiri wake, fedha zilizokuja kwenye umiliki wake kupitia ajira yake.

Mshtakiwa anadaiwa kughushi kadi ya mpigakura yenye jina la Airi Asa Salaam kwa kujifanya ilikuwa halali na ilitolewa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC).

Inadaiwa kuwa Mei 28, 2019, katika Benki ya Azania, Tawi la Masdo, kwa nia ya kudanganya, aliwasilisha kitambulisho hicho kwa Waida Abubakar ambaye ni mtoa huduma wa benki hiyo kwa kudai ni nyaraka halali wakati siyo kweli.

# Makundi hatarishi homa ya ini yatajwa

**Na Augusta Njoji, DODOMA**

WIZARA ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, imetaja makundi hatarishi saba kwenye maambukizi ya homa ya ini aina ya B na C nchini.

Makundi hayo ni pamoja na watumishi wa afya, wanaume wanaofanya ngono na wanaume wenzao, watu wanaojidunga dawa za kulevya, watu wenye wapenzi wengi na wenye magonjwa sugu ya ini na figo.

Wengine ni wazee kuanzia miaka 60 wenye kisukari na watu wanaosafiri kwenda kwenye nchi zenye maambukizi makubwa ya 'Hepatitis B'.

Kutokana na hali hiyo, wizara inakamilisha mwongozo wa matibabu ya homa hiyo ambao utatumikia nchi nzima na kupunguza gharama kwa wananchi wanaofuata huduma katika Hospitali ya Taifa Muhimbili, Dar es Salaam.

Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Dorothy Gwajima, alibainisha hayo jana kupitia tamko la maadhimisho ya Siku ya Homa ya Ini Duniani alilotoa kwa vyombo vya habari.

Katika tamko hilo, Dk. Gwajima alisema ugonjwa huo umetajwa kuwa hatari na unaua idadi kubwa ya watu pole pole.

Aidha, alisema utafiti mahususi ujulikanao kama 'THIS' unaoratibiwa na Ofisi ya Taifa ya Takwimu, unaonyesha kuwa maambukizi ya homa ya ini aina ya B ni asilimia nne miongoni mwa Watanzania wenye umri kati ya miaka 15-49 kwa mwaka 2017.

Hata hivyo, alisema takwimu kutoka Mpango wa Taifa wa Damu Salama (NBTS) zinaonyesha kuwa maambukizi ya ini aina ya B kwa wachangiaji damu kwa miaka mitatu mfululizo yanaongezeka. Mwaka 2018 kati ya wachangiaji damu 307,835 takribani watu 13,613 sawa na asilimia 4.4 walikuwa na maambukizi.

"Mwaka 2019, kati ya wachangiaji damu 258,779 takribani 14,123 sawa na asilimia 5.5 walikuwa na maambukizi na mwaka 2020 kati ya wachangiaji damu 263,119 takribani watu 15,923 sawa na asilimia 6.1 walikuwa na maambukizi," alisema.

Alitaja mikoa iliyokuwa na maambukizi makubwa ya homa ya ini kwa mwaka 2020 kwenye kundi la watu wanaochangia damu ni Mara asilimia 9.3, Geita asilimia 8.7, Morogoro asilimia 7.7, Rukwa asilimia 7.6 na Shinyanga ni asilimia 7.4.

Kwa upande wa homa ya ini inayosababishwa na virusi aina ya C, kwa mwaka 2019 maambukizi yalikuwa kati ya wachangiaji wa damu 258,779 takribani watu 5,344 sawa na asilimia 2.1 walikuwa na maambukizi huku mwaka 2020, kati ya wachangiaji damu 263,119, takribani watu 6,914 sawa asilimia 2.6 walikuwa na maambukizi.

"Mikoa iliyoongoza kwa maambukizi ya homa ya ini ya C kwa mwaka 2020, kwenye kundi la wachangiaji damu ni Mtwara asilimia 5.5, Ruvuma asilimia 4.6, Kilimanjaro na Geita asilimia 4.6 na Lindi asilimia 4.5," alisema.

Aliwahimiza wananchi kufanya uchunguzi wa homa hiyo na watakaobainika kuwa na maambukizi watapatiwa chanjo hiyo kwa gharama nafuu kwenye hospitali za serikali.

Waziri aliagiza hospitali binafsi na za mashirika ya kidini kushusha gharama za upimaji na utoaji wa chanjo ili kuwafikia wananchi wote.

Akitoa semina kwa waandishi kuhusu ugonjwa huo, Mratibu wa Homa ya Ini wa Wizara hiyo, Dk. Baraza Nzobo, alisema uchangiaji vitu vya ncha kali ikiwamo vitu vya kutoga masikio pia unasababisha maambukizi ya ugonjwa huo.


## FIRST HOUSING FINANCE (TANZANIA) LIMITED

1st Housing

### UONESHAJI WA TAARIFA ZA FEDHA KWA UMMA 30.06.2021

### IMETOLEWA CHINI YA KANUNI YA 7 NA YA 8 YA KANUNI ZA MABENKI NA TAASISI ZA FEDHA (UONESHAJI) YA MWAKA 2014

#### WARAKA MIZANIA KWA TAREHE 30.06.2021

*(Kiasi kwa shilingi elfu)*

| | | Robo Mwaka ya sasa 30th Jun. 2021 | Robo Mwaka iliyopita 31st Mar. 2021 |
|---|---|---|---|
| A. | MALI | | |
| 1 | Fedha Taslimu | 229 | 92 |
| 2 | Salio Katika Benki Kuu ya Tanzania | - | - |
| 3 | Uwekezaji Katika Amana za Serikali | 3,600,276 | 3,657,426 |
| 4 | Salio Katika Benki Nyingine na Taasisi za Fedha | 5,435,568 | 6,386,865 |
| 5 | Hundi na Miamala ya Kushughulikiwa | - | - |
| 6 | Miamala Baina ya Matawi | - | - |
| 7 | Bili Zilizoafikiwa | - | - |
| 8 | Dhima za Wateja Zilizokubalika | - | - |
| 9 | Mikopo Iliyotolewa kwa Benki Nyingine | - | - |
| 10 | Uwekezaji Katika Amana Nyingine | - | - |
| 11 | Mikopo Halisi Iliyopo | 9,029,473 | 7,961,296 |
| 12 | Mali Nyingine | 680,536 | 549,167 |
| 13 | Uwekezaji wa Hisa | 1,622,000 | 1,622,000 |
| 14 | Akaunti za udhamini | - | - |
| 15 | Mali Zisizohamishika, Mitambo na Vifaa | 545,353 | 587,637 |
| 16 | **JUMLA YA MALI** | **20,913,434** | **20,764,484** |
| | | | |
| B. | B. DHIMA | | |
| 17 | Amana za Benki nyingine na Taasisi za Fedha | - | - |
| 18 | Amana za Wateja | 420,471 | 418,073 |
| 19 | Dhamana ya Malipo kwa Fedha Taslimu | - | - |
| 20 | Amana Maalumu | - | - |
| 21 | Maagizo ya Malipo/Fedha za Kuhamisha | - | - |
| 22 | Hundi na Hawala za Kibenki Zilizotolewa | - | - |
| 23 | Limbiko la Kodi na Gharama Zitakazolipwa | 784,855 | 801,510 |
| 24 | Dhima la Tozo kwa Ajili ya Usuluhishi Baina ya Benki na Mteja | - | - |
| 25 | Miamala Isiyoshughulikiwa Baina ya Matawi | - | - |
| 26 | Mapato yaliyoingia ya Kipindi Kijacho na Tozo Nyingine Zitakazolipwa Baadae | 131,246 | 121,749 |
| 27 | Dhima Nyingine | 541,504 | 417,580 |
| 28 | Madeni | 1,010,685 | 1,010,274 |
| 29 | **JUMLA YA DHIMA** | **2,888,762** | **2,769,186** |
| 30 | **MALI/(DHIMA) HALISI** ***(16 kutoa 29)*** | **18,024,673** | **17,995,297** |
| | | | |
| C. | FEDHA ZA WANAHISA | | |
| 31 | Mtaji wa Hisa Uliolipwa | 21,800,000 | 21,800,000 |
| 32 | Malipo juu ya bei ya hisa | - | - |
| 33 | Akiba ya Mtaji | 95,831 | 95,831 |
| 34 | Mapato Yaliyobakizwa | (3,924,009) | (3,911,640) |
| 35 | Faida (Hasara) ya Kipindi Husika | 40,482 | 11,106 |
| 36 | Akaunti Nyingine za Mtaji | 12,369 | - |
| 37 | Stahiki ya Wenyehisa Chache | - | - |
| 38 | **JUMLA YA FEDHA ZA WANAHISA** | **18,024,673** | **17,995,297** |
| 39 | Dhima Zisizo Dhahiri | - | - |
| 40 | Mikopo Chechefu | 132,898 | 133,564 |
| 41 | Tengo kwa Ajili ya Mikopo Chechefu | 25,802 | 19,465 |
| 42 | Mali Nyingine Chechefu | - | - |
| | | | |
| D. | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA HALI YA KIFEDHA** | | |
| (i) | Uwiano wa Fedha za Wanahisa na Jumla ya Mali | 86.19% | 86.66% |
| (ii) | Uwiano wa Mikopo Chechefu na Jumla ya Mikopo Ghafi | 1.47% | 1.68% |
| (iii) | Uwiano wa Mikopo Ghafi na Jumla ya Amana | 2216.82% | 1957.04% |
| (iv) | Uwiano wa Mikopo Halisi na Jumla ya Mali Halisi | 43.18% | 38.34% |
| (v) | Uwiano wa Mali Zinazozalisha na Jumla ya Mali | 88.20% | 90.35% |
| (vi) | Ongezeko la Amana | 0.57% | 1.21% |
| (vii) | Ongezeko la Mali | 0.72% | 2.93% |

Katika kuanda taarifa hizi za fedha, sera za uandaaji ni zilizile zilizotumika wakati wa uandaaji wa Taarifa za Fedha zilizokaguliwa za mwaka uliopita (kama kulikua na mabadiliko katika sera za uandaaji taarifa za fedha katika kipindi cha robo mwaka ya/mwaka wa sasa, mabadiliko yaelezwe kwa mujibu wa IAS 34 na IAS 8).

| **Jina na Cheo :** | **Saini** | **Tarehe** |
|---|---|---|
| Sasa M. Chonza **(Ofisa Mtendaji Mkuu)** | **(Imesainiwa)** | **20.07.2021** |
| Amulike Kamwela **(Mkuu wa Fedha)** | **(Imesainiwa)** | **20.07.2021** |
| Ally Kimbulaga (Kaimu Mkaguzi Mkuu wa Ndani) | (Imesainiwa) | 20.07.2021 |

#### TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 30.06.2021

*(Kiasi kwa shilingi elfu)*

| | Maelezo | Robo ya Mwaka sasa | Robo ya mwaka Linganishi (Mwaka Uliopita) | Limbikizo la Mwaka wa sasa | Limbikizo la Mwaka Linganishi (Mwaka Uliopita) |
|---|---|---|---|---|---|
| | | 30th Jun. 2021 | 30th Jun. 2020 | 30th Jun. 2021 | 30th Jun. 2020 |
| 1 | Mapato ya Riba | 560,869 | 382,029 | 1,082,651 | 743,625 |
| 2 | Gharama za Riba | (30,987) | (6,602) | (59,543) | (14,228) |
| 3 | **Mapato Halisi ya Riba (1kutoa 2)** | **529,881** | **375,427** | **1,023,108** | **729,397** |
| 4 | Madeni Viza Yaliyofutwa | - | - | - | - |
| 5 | Punguzo/Ongezeko la tengo katika Mikopo | 3,235 | (204) | 12,806 | (461) |
| 6 | **Mapato Yasiyo ya Riba:** | **28,603** | **17,559** | **64,830** | **18,929** |
| | 6.1 Faida /(Hasara) Zitokanazo na Miamala ya Fedha za Kigeni | 57 | 156 | 83 | (924) |
| | 6.2 Ada na Kamisheni | 28,536 | 2,000 | 64,734 | 4,450 |
| | 6.3 Gawio | - | 10,333 | - | 10,333 |
| | 6.4 Mapato Mengine | 11 | 5,070 | 13 | 5,070 |
| 7 | **Gharama Zisizo za Riba:** | **(529,396)** | **(531,400)** | **(1,054,524)** | **(1,059,236)** |
| | 7.1 Mishahara na Mafao | (260,866) | (238,798) | (494,354) | (475,963) |
| | 7.2 Ada na Kamisheni | - | - | - | - |
| | 7.3 Gharama Nyingine | (268,530) | (292,601) | (560,170) | (583,273) |
| 8 | **Faida /(Hasara) ya Uendeshaji** | **32,323** | **(138,618)** | **46,219** | **(311,371)** |
| 9 | Tengo la Kodi ya Mapato | (2,947) | (1,033) | (5,737) | (1,033) |
| 10 | **Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato** | **29,376** | **(139,651)** | **40,482** | **(312,405)** |
| 11 | **Mapato Mengine Yaliyojumuishwa (bainisha)** | - | - | - | - |
| 12 | **Jumla ya Faida (Hasara) iliyojumuishwa kwa robo ya mwaka /mwaka** | **29,376** | **(139,651)** | **40,482** | **(312,405)** |
| 13 | Idadi ya Waajiriwa | 18 | 10 | 18 | 10 |
| 14 | Mapato kwa Hisa | 0.13 | (0.64) | 0.19 | (1.43) |
| 15 | Idadi ya Matawi | 1 | 1 | 1 | 1 |
| | | | | | |
| | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA UFANISI** | | | | |
| (i) | Uwiano wa Faida Kabla ya Kodi na Wastani wa Mali | 0.14% | -0.71% | 0.20% | -1.60% |
| (ii) | Uwiano wa Faida baada ya Kodi na Wastani wa Fedha za Wanahisa | 0.16% | -0.77% | 0.22% | -1.71% |
| (iii) | Uwiano wa Matumizi Yasiyo ya Riba na Mapato Ghafi | 94.79% | 135.22% | 96.93% | 135.22% |
| (iv) | Uwiano wa Mapato Halisi ya Riba na Wastani wa Mali Zinazozalisha | 2.85% | 2.14% | 5.50% | 4.26% |

#### TAARIFA YA MABADILIKO YA MTAJI KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 30.06.2021

*(Kiasi kwa shilingi elfu)*

| | Mtaji wa Hisa | Malipo juu ya bei ya hisa | Mapato Yaliyobakizwa | Ziada ya Kisheria | Tengo la Ziada ya Jumla | Mengineyo (Bainisha) | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Robo ya mwaka ya sasa (30.06.2021)** | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa robo ya mwaka (01.04.2021)** | **21,800,000** | - | **(3,900,534)** | - | - | **95,831** | **17,995,297** |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | 29,376 | - | - | - | 29,376 |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | (12,369) | 12,369 | - | - | - |
| Ziada ya Kisheria | - | - | - | - | - | - | - |
| Tengo la Ziada ya Jumla | - | - | - | - | - | - | - |
| Mengineyo | - | - | - | - | - | - | - |
| **Salio la mwisho wa robo ya mwaka (30.06.2021)** | **21,800,000** | - | **(3,883,528)** | **12,369** | - | **95,831** | **18,024,673** |
| | | | | | | | |
| **Robo ya mwaka iliyopita (31.03.2021)** | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa mwaka (01.01.2021)** | **21,800,000** | - | **(3,911,640)** | - | - | **95,831** | **17,984,191** |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | 11,106 | - | - | - | **11,106** |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Ziada ya Kisheria | - | - | - | - | - | - | - |
| Tengo la Ziada ya Jumla | - | - | - | - | - | - | - |
| Mengineyo | - | - | - | - | - | - | - |
| **Salio la mwisho wa robo ya mwaka (31.03.2021)** | **21,800,000** | - | **(3,900,534)** | - | - | **95,831** | **17,995,297** |

Sisi, tuliotajwa hapo chini, wajumbe wa bodi ya wakurugenzi, tunathibitisha usahihi wa taarifa za hapo juu, tunatamka kwamba tumezitathmini taarifa hizi, na kwa uelewa na imani yetu kubwa zimeandaliwa kulingana na Viwango vya Kimataifa vya Uwasilishaji wa Taarifa za Fedha na matakwa ya Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha ya mwaka 2006, na zinaonesha hali halisi).

| **Jina:** | **Saini** | **Tarehe** |
|---|---|---|
| Sanjay Suchak **Mwenyekiti** | (Imesainiwa) | 20.07.2021 |
| Charles Itembe **Mkurugenzi** | (Imesainiwa) | 20.07.2021 |

#### TAARIFA YA MTIRIRIKO WA FEDHA KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 30.06.2021

*(Kiasi kwa shilingi elfu)*

| | | Robo ya Mwaka sasa | Robo ya Mwaka iliyopita | Limbikizo la Mwaka wa sasa | Limbikizo la Mwaka Linganishi (Mwaka Uliopita) |
|---|---|---|---|---|---|
| | | 30th Jun. 2021 | 31st Mar. 2021 | 30th Jun. 2021 | 30th Jun. 2020 |
| I: | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uendeshaji:** | | | | |
| | Mapato/(Hasara) Halisi | **32,323** | **13,896** | **46,219** | **(311,371)** |
| | **Marekebisho kwa Ajili ya:** | - | - | - | - |
| | - Hasara Katika Mali | 132,394 | 77,389 | 133,007 | 261,534 |
| | - Badiliko Halisi Katika Mikopo | (1,068,177) | (1,707,160) | (2,775,950) | (1,169,151) |
| | - Faida/Hasara Kwenye Mauzo ya Mali | - | - | - | - |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Amana | 2,398 | 4,986 | 7,384 | - |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Amana za Muda Mfupi Zilizoafikiwa | 57,151 | (1,115,279) | (1,058,129) | - |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Dhima Nyingine | 111,029 | 573,233 | 687,051 | (39,287) |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Mali Nyingine | (131,369) | 36,690 | (94,679) | (86,103) |
| | - Kodi iliyolipwa | - | - | - | - |
| | - Mengineyo | 14,171 | 30,347 | 36,233 | (6,700) |
| | ***Fedha Halisi zilizotolewa (zilizotumika) kwa shughuli za uendeshaji*** | ***(850,081)*** | ***(2,085,899)*** | ***(3,018,864)*** | ***(1,351,079)*** |
| II: | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uwekezaji:** | | | | |
| | Gawio Lililopokewa | - | - | - | 9,301 |
| | Ununuzi wa Mali za Kudumu | (90,110) | (418,001) | (430,722) | (4,564) |
| | Mapato Kutokana na Mauzo ya Mali za Kudumu | - | - | - | - |
| | Ununuzi wa Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | - | - | - |
| | Mapato Kutokana na Mauzo ya Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | - | - | - |
| | Mengineyo (bainisha) | - | - | - | - |
| | ***Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Uwekezaji*** | ***(90,110)*** | ***(418,001)*** | ***(430,722)*** | ***4,737*** |
| III: | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Kifedha:** | | | | |
| | Ulipaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - | - | - |
| | Mapato Kutokana na Utoaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - | - | - |
| | Mapato Kutokana na Utoaji wa Mtaji wa Hisa | - | - | - | - |
| | Gawio Lililolipwa kwa Fedha Taslimu | - | - | - | - |
| | Mabadiliko Halisi Katika Madeni Mengine | 411 | (205) | 206 | - |
| | Mengineyo (bainisha) | (24,851) | (49,489) | (49,702) | (75,251) |
| | ***Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Kifedha*** | ***(24,440)*** | ***(49,695)*** | ***(49,496)*** | ***(75,251)*** |
| IV: | **Fedha Taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu:** | | | | |
| | **Ongezeko / Punguzo Halisi Katika Fedha taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu** | **(964,631)** | **(2,553,594)** | **(3,499,082)** | **(1,421,593)** |
| | Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwanzoni mwa Robo Mwaka | 6,386,957 | 8,921,408 | 8,921,408 | 14,965,937 |
| | Badiliko Halisi Katika Mikopo ya mabenki | 13,470 | 19,143 | 13,470 | (72,283) |
| | **Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwishoni mwa Robo Mwaka** | **5,435,797** | **6,386,957** | **5,435,797** | **13,472,060** |

#### MINIMUM DISCLOSURES OF CHARGES AND FEES

| S/No | ITEMS | CHARGES/FEES |
|---|---|---|
| 1 | Prime Lending Rate (PLR) | 16% p.a. |
| 2 | Maximum spread above PLR | 4% p.a. |
| 3 | Application Fee (Non-refundable) | TZS 200,000/- |
| 4 | Processing Fee | 1.5 % of the loan value |
| 5 | Facility Fee | 1.5 % of the loan value |
| 6 | Valuation Fee | Paid by the client as per the invoice |
| 7 | Legal Fee | Paid by the client to FHF account and FHF will pay law firm |
| 8 | Early Repayment | 5% of the amount to be prepaid |
| 9 | Annual Review Fee | NIL |
| 10 | Cheque returned Unpaid (Outward & Inward) | TZS 50,000/- |
| 11 | Loan Statement | TZS 20,000/- |



1st Housing
Homes within your reach

Unlike banks we aren't limited to options when it comes to Home Loans.

Being a dedicated mortgage provider, we have a variety of products on home loans which can be cherry picked for every individual.

THE MORTGAGE FINANCIAL INSTITUTION
Dar es Salaam
Plot No. 19, Barack Obama Drive | Postal Address 11990 | +255 22 2113456 |
info@firsthousing.co.tz | www.firsthousing.co.tz

216378301

# Nyoka asababisha Mwalimu Mkuu kuikimbia nyumba

**Na Halima Ikunji,** KALIUA

MWALIMU Mkuu wa Shule ya Sekondari ya Dk. John Magufuli katika Kata ya Kamsekwa, wilayani Kaliua mkoani Tabora, amekimbia nyumba aliyojengewa na shule kwa hofu ya kuwapo nyoka aina ya kobogo.

Mwenyekiti wa Serikali ya Kijiji cha Kamsekwa, Ramadhan Juma, alibainisha hayo mbele ya Mbunge wa Jimbo la Kaliua, Aloyce Kwezi, alipokuwa katika ziara ya kukagua utekelezaji miradi ya maendeleo wilayani humo.

Mwenyekiti huyo alimweleza mbunge na Kamati ya Mfuko wa Jimbo kuwa nyumba hiyo licha ya kukamilika tangu mwaka 2015 haikaliwi na mtu kwa sababu ya nyoka huyo aliyeko ndani.

Alisema licha ya mwenyewe kutomuona, lakini waliomuona walidai ni nyoka aina ya kobogo na tangu alipoonekana katika nyumba hiyo, Mwalimu Mkuu hakuingia tena.

Alisema walileta wazee wa kimila wakafanya tambiko baadaye akaja mchungaji kuombea nyumba hiyo, lakini wanaogopa kwenda kufungua mlango kujiridhisha kama bado yupo au alishaondoka.

Mwalimu Mkuu Leonard Assenga, alisema walimu na wanafunzi wana hofu kubwa na nyoka huyo na kushindwa kufundisha.

Hata hivyo, alisema hakuna madhara yaliyosababishwa na nyoka huyo, lakini ni hofu miongoni mwa walimu na wanafunzi na kuomba juhudi zifanyike ili kumwondoa na kumwezesha kurudi katika nyumba yake.

Kaka Mkuu wa shule hiyo, Joseph Jackson, alisema hawana raha na wanashindwa kusoma kwa amani kutokana na hofu.

Kwa upande wake mbunge wa jimbo hilo, Aloyce Kwezi, aliwataka kutafuta mtaalamu wa kukamata nyoka ili awasaidie kumwondoa kwa kuwa uwapo wake katika eneo hilo ni hatari na unawapa hofu walimu na wanafunzi.

Aliwataka viongozi wasitegemee maombi bali wawatafute wataalamu wa kukamata nyoka waje wamwondoe ili wanafunzi wasome kwa amani na utulivu.

"Shughulikieni suala hilo haraka iwezekanavyo ili maendeleo ya shule hiyo kitaaluma na miradi inayoendelea kutekelezwa isije kuathirika kutokana na hofu iliyopo," alisema.



Kaimu Meneja wa Benki ya Exim tawi la Shinyanga, Sarah Paul Tito (kulia) akieleza huduma zinazotolewa na benki hiyo, kwa Naibu Waziri wa Madini, Prof. Shukrani Manya (kushoto), katika maonyesho ya pili ya biashara na teknolojia ya madini mjini Shinyanga jana. Wengine ni Mkuu wa mkoa wa Shinyanga, Dk. Philemon Sengeti (wa tatu kushoto) na Mkuu wa mkoa wa Mara, Ally Hapi (wa pili kushoto). **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mwanamke auawa kikatili madai ya ugomvi wa mali

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

MKAZI wa Lunguya wilayani Njombe, Emma Mfikwa (43), ameuawa kikatili kwa kukatwa na vitu vyenye ncha kali kutokana na kile kinachodaiwa migogoro ya kifamilia iliyotokana na kugombania mali.

Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Njombe, Hamisi Issah, alitoa taarifa hiyo wakati alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kuwa tukio hilo lilitokea Julai 24, majira ya saa mbili asubuhi.

Alisema jeshi hilo linawashikilia watuhumiwa wanne wa familia moja ambao wametajwa kuhusika na tukio hilo.

Kamanda Issah alisema, awali mwanamke huyo aliolewa na mume wake ambaye kwasasa ni marehemu na kuamua kujenga nyumba kwenye kiwanja chao baada ya mumewe kufariki kitendo ambacho familia ya mume wa mwanamke huyo haikupenda na kutengeneza mgogoro mkubwa.

"Kesi ipo mahakamani inayohusiana na umiliki wa hiyo nyumba lakini haijafikia mwishoni mwanamke huyo ameuawa," alisema Issah.

Pia, alisema jambo la kushangaza katika tukio hilo miongoni mwa watuhumiwa waliokamatwa yupo mtoto wa marehemu ambaye amehusika katika tukio hilo la kikatili la mauaji.

Alisema jeshi hilo linaendelea na uchunguzi ili kuwasaka watuhumiwa wengine waliohusika na mauaji hayo ambao wataunganishwa na kupelekwa mahakamani baada ya upelelezi kukamilika.

"Napenda kuwaambia wana Njombe haki ya mwanamke ipo pale pale ya kuishi na kumiliki mali katika familia na hata ya kutofanyiwa ukatili wa aina yoyote," alisema Issah.

Katika hatua nyingine jeshi hilo linamtafuta mtu aliyehusika kumtupa mtoto majira ya usiku mwenye umri wa miezi tisa katika bonde la mto wa maji karibu na chuo cha maendeleo ya jamii mjini hapa na kusababisha kifo chake.

Alisema chanzo cha kifo cha mtoto huyo ni baridi kali licha kuwa aliokotwa akiwa amefunikwa nguo na inaonyesha kuwa mzazi wa mtoto huyu alimtelekeza akiamini kuwa watu watamkuta akiwa hai na kumchukua.


TANZANIA FOREST CONSERVATION GROUP

Tanzania Forest Conservation Group
Shirika la Kuhifadhi Misitu ya Asili Tanzania

**STATEMENT OF RECEIPTS AND EXPENDITURE FOR THE YEAR ENDED 31 DEC 2020**

This publication of the Statement of Receipts and Expenditure is made in accordance with regulation 13(a) of the Non-Government Organization Act (Amendments), Regulation 2018 which requires Non-Government Organizations receiving funds exceeding TZS 20 Million to publish bi annually the funds received and its expenditure.

| DETAILS | ACTUAL - TZS |
|---|---|
| **RECEIPTS** | |
| Opening fund balance | 1,935,771,321.00 |
| Disbursement from Donors | 4,528,004,561.00 |
| **TOTAL RECEIPTS FROM DONORS** | **6,463,775,882.00** |
| | |
| **PROGRAMMES EXPENDITURE** | |
| Participatory Forest Management | 1,054,774,100.00 |
| Research | 127,704,167.00 |
| Environmental Education | 223,046,125.00 |
| Community Development (Poverty reduction in rural communities) | 1,177,146,183.00 |
| Communication and Advocacy | 225,176,525.00 |
| **OTHER PROGRAMME EXPENDITURE** | |
| Institution Development and Resources Mobilization | 348,109,885.00 |
| Personnel | 1,602,378,392.00 |
| **TOTAL PROGRAMMES EXENDITURES** | **4,758,335,377.00** |
| **FUND BALANCE**** | **1,705,440,505.00** |

****Fund balance represents an obligation to conduct donor funded activities per contractual commitments made between donor/development partners and the organisation/recipient, where funds have not been transferred and such activities have not yet occurred.**

**Executive Director**
**Tanzania Forest Conservation Group**
**Plot 323, Msasani Village, Mwaikibaki Rd**
**P.O. Box. 23410, Dar es Salaam, Tanzania**

21637920Z

# Waziri azitaka kaya maskini kubadilika

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

NAIBU Waziri Ofisi ya Rais (Utumishi na Utawala Bora), Deogratius Ndejembi, amesema kaya maskini ambazo ni wanufaika wa Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) zinatakiwa kutumia fursa hiyo kuleta mabadiliko ya kimaendeleo.

Ndejembi ametoa maagizo hayo alipofanya ziara ya siku moja katika Wilaya ya Kibaha ambapo alikwenda Kijiji cha Mwanabwito kuona kaya zinazopokea fedha za TASAF.

Wanufaika hao walieleza kikwazo cha ucheleweshaji wa fedha ambapo alisema pamoja na hali hiyo, lakini bado wapo wanufaika wa muda mrefu ambao hawajaonyesha mabadiliko ya kimaendeleo kupitia fedha wanazowezeshwa na TASAF.

Alisema pamoja na juhudu za serikali kusaidia kaya maskini, lakini kuna baadhi yao hali zao zimeendelea kubaki kama zamani kwa kutokuwa na mabadiliko.

"Ni jukumu lenu kuamka kubadilika kimaendeleo, lazima tujitathmini tumefanya nini tangu tuanze kupata hizi fedha, ni miradi gani ya kujikwamua na umaskini tumeifanya tubadilike," alisema.

# Nyumba za wadaiwa sugu Pemba zafungwa

**Na Mwandishi Wetu,** PEMBA

MPAKA Juni mwaka huu, Ofisi ya Shirika la Nyumba Pemba linadai fedha shilingi 269,310,000 ambazo ni madeni ya kodi za wapangaji.

Nyumba hizo zinatumika kwa makazi pamoja na maduka ya biashara.

Akizungumza katika zoezi la kuzifunga nyumba za wadaiwa sugu, Kaimu Mkurugenzi wa Ofisi ya Shirika la Nyumba Pemba, Ali Mgau Kombo, alisema madeni ya baadhi ya wakazi hao ni mengi, hivyo wameamua kuzifunga kwa kuweka kufuli.

Alisema wapangaji wamekuwa wagumu kulipa licha ya kuwahamasisha, kuwaonya na hata kuwaita kwa barua.

Alieleza kuwa wamekuwa wakikataa na kupuuza wito wa shirika hilo kila wanapoitwa kwenda kulipa madeni wanayodaiwa, jambo ambalo limewafanya wachukue hatua ya kuzifunga nyumba hizo.

"Hatua hii ya kuzifungia nyumba, tunaamini kwamba tutaamsha ari na hamasa ya wakazi hao kulipa madeni kwa haraka pamoja na kulipa kodi kwa wakati, ili kuiletea nchi maendeleo," alisema.

# Wenye ulemavu walia kero huduma za afya

**Na Lilian Lugakingira,** MULEBA

WATU wenye ulemavu mbalimbali katika Mkoa wa Kagera wameiomba serikali kuwatengenezea vitambulisho maalumu ambavyo vitawasaidia kupata huduma haraka na bila usumbufu wanapokwenda kutibiwa katika vituo vya kutolea huduma.

Wakizungumza wakati wa tathmini ya mradi wa kuondoa vikwazo vya kiafya kwa watu wenye ulemavu unaofadhiliwa na Shirika la The Foundation For Civil Society, walisema baadhi yao wamekuwa wakifika hospitali na kurudishwa katika vijiji vyao, ili wapewe uthibitisho na serikali za vijiji kuwa wanastahili kutibiwa bure, bila kujali kuwa ni wagonjwa.

Aleckseda Masilingi, alisema kuwa kutokana na aina tofauti za ulemavu walionao, wengi wao hawana shughuli za kuwaingizia kipato, hali inayowafanya kushindwa kupata fedha za matibabu.

"Tunaishukuru serikali kwa kuliona hilo na kutuwekea utaratibu wa kutibiwa bure, lakini wakati mwingine tukienda hospitali wahusika wakiona umevaa vizuri wanakwambia wewe una uwezo uende ulete hela... kwa hiyo tunaomba angalau tupewe vitambulisho ambavyo vitaturahisishia kupata huduma bila usumbufu," alisema. Akizungumzia changamoto za kiafya kwa watu wenye ulemavu, Makamu Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Muleba, Muhaji Bushako, aliwataka viongozi na watendaji kuwakaribisha kwenye vikao vya vitongoji, vijiji na kata ili waeleze vikwazo vinavyowakabili vikiwamo vya kiafya, kwa lengo la kutafutiwa ufumbuzi wa kudumu.

"Watu wenye ulemavu viongozi wenu kuanzia ngazi za kitongoji wasikae tu kwa sababu wao ni viongozi, waende wawatafute wenyeviti wa vitongoji na vijiji, pia na uongozi wa kata ili wazungumze nao juu ya umuhimu wa kuwakaribisha katika vikao vyote, ili wawasilishe matatizo yanayowakabili," alisema.

Bushako alisema changamoto kuhusu matibabu bure kwa watu wenye ulemavu zitapungua maana miongozo iliyotolewa imeshapelekwa mpaka ngazi ya zahanati, vituo vya afya na hospitali, kwa hiyo ni rahisi kutetea na kufuatilia kama watu wanapatiwa haki zao.

Naye mratibu wa mradi huo wa kuondoa vikwazo vya kiafya kwa watu wenye ulemavu, Laurian Pankras, alisema baada ya serikali kudai kupeleka miongozo katika maeneo ya kutolea huduma za afya, wataunda kamati katika kila kata ambazo zitakuwa zikiwasiliana na kamati za afya za halmashauri, ili kubaini changamoto zinazowakabili watu wa kundi hilo.

Katibu wa Shirikisho la Vyama vya Watu wenye Ulemavu (SHIVYAWATA) mkoa wa Kagera, Sweetbert Mushanga, aliwataka watu wenye ulemavu kutokata tamaa na kuendelea kuwa wavumilivu wakati hatua zikichukuliwa kupunguza changamoto zinazowakabili, zikiwamo za matibabu.




Mkuu wa Kitengo cha Bima wa Benki ya NMB, Martine Massawe (katikati), akikabidhi mfano wa hundi ya zaidi ya Sh. milioni 400 kwa wafanyabiashara waliokuwa na bima walioungua katika Soko la Kuu la Kariakoo, Sajida Kagasheki na Emmanuel Kabadi (kushoto), jijini Dar es Salaam juzi. Kulia ni Meneja wa Bima wa Benki ya NMB, Adam Nsenga na (wapili kulia) ni Meneja wa Kampuni ya Reliance, Joel Mwakalebela. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Gekul ataka matumizi sahihi fursa zilizopo mtandaoni

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI imehimiza matumizi bora na salama ya mfumo wa mtandao kuhakikisha maudhui mtandaoni yanasalia kuwa yenye manufaa kwa watumiaji wote na kuhakikisha makosa ya uvunjifu wa sheria za mtandao yanapungua.

Aidha, watumiaji wamekumbushwa kutumia vema huduma hizo ili kuchagiza ukuaji wa uchumi na kuepuka matumizi ya mitandao yanayokiuka sheria za nchi, kanuni na maadili.

Naibu Waziri wa Habari, Sanaa, Utamaduni na Michezo, Pauline Gekul, alibainisha hayo jana alipotembelea Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania TCRA jijini Dar es Salaam.

Alisema matumizi sahihi na salama ya mitandao yatawezesha kufikiwa kwa malengo ya maendeleo kwa watumiaji binafsi na kuiwezesha serikali kuongeza tija katika maendeleo ya uchumi.

Katika ziara hiyo ambayo Naibu Waziri pia alipata fursa ya kujifunza namna mamlaka hiyo inavyofanya kazi, alitoa wito kwa vituo vya utangazaji wa redio na televisheni kuhakikisha vinarusha maudhui yanayozingatia maadili ya kitaifa badala ya kuweka kipaumbele urushaji maudhui yasiyofaa yanayoweza kubomoa maadili na utamaduni wa jamii.

"TCRA tunashirikiana nao kwa upande wa wizara yetu kuhakikisha kwamba maudhui ambayo yanapelekwa na vyombo vya habari kwa wananchi yanakuwa sahihi, lakini yanaangalia maadili ya Taifa letu. Nitoe tu rai kwa jamii, tunapotumia mitandao hii tuitumie kwa namna ya kujenga na si kubomoa," alisisitiza.

Naibu Waziri pia, alihimiza umuhimu wa umoja, mshikamano na maendeleo ya nchi.

Katika ziara hiyo, Gekul alipata fursa ya kupokea wasilisho juu ya utendaji kazi wa TCRA na kushauriana na Menejimenti ya TCRA juu ya masuala mtambuka yanayoangukia katika Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo ambapo Naibu Waziri alipokea maelezo na kupata ufafanuzi namna mamlaka hiyo inavyosimamia huduma za maudhui ya utangazaji na mtandaoni.

Mkurugenzi Mkuu wa TCRA, Dk. Jabiri Kuwe Bakari, alibainisha kuwa katika mitandao ya kijamii zimo fursa nyingi za maendeleo kwa ajili ya wananchi na Taifa na kuwatolea wito wananchi kuzitumia vilivyo fursa hizo ili kujinufaisha kiuchumi badala ya kutumia mitandao isivyopasa kinyume cha sheria za nchi.

# Machinga waeleza corona ilivyowaathiri

**Na Christina Haule,** MOROGORO

WAFANYABIASHARA wadogo maarufu wamachinga katika Manispaa ya Morogoro, wamesema wanakumbana na ugumu wa biashara na wengine kuelemewa na mikopo kwa sababu wateja wa bidhaa zao wameanza kupungua tangu kuibuka kwa wimbi la tatu la ugonjwa wa corona (UVICO-19).

Wakizungumza kwa nyakati tofauti wafanyabiashara hao akiwamo mfanyabiashara wa nguo za mitumba Mustapha Chande, alisema biashara zao huwa zinachangamka msimu huu wa kiangazi kuanzia Juni na kuendelea, lakini mwaka huu imekuwa tofauti, hali ambayo wanaihusisha na kuzuka kwa wimbi la tatu.

“Huwa ninakwenda kwenye magulio yaliyo ndani na nje ya Manispaa kwa ajili ya kuuza nguo za kike na za watoto, hali huwa nzuri katika msimu wa kiangazi, lakini msimu wa kiangazi wa mwaka huu hali ni tofauti na ilivyokuwa nyuma,” alisema.

Chande alisema amekuwa akifanya biashara kwa mauzo yasiyokuwa na faida kwa sababu ya kuuza mzigo mmoja katika magulio mawili au matatu tofauti na miezi mingine kama hiyo, hivyo kuwa na ugumu katika kurejesha mkopo aliyokopa.

Naye muuza madafu Manispaa ya Morogoro, Juma Mpili, alisema biashara yake imekuwa ngumu, kwani awali alikuwa akiuza kati ya 50 mpaka 60 kwa siku, lakini kwa sasa anauza kati ya 15 mpaka 25.

“Biashara imekuwa ngumu, ninazunguka kwa baiskeli nikiwa nimebeba mzigo wa madafu kutwa nzima, lakini naambulia kuuza kidogo mengi yanabaki. Biashara imezorota sana, huenda ni corona,” alisema Mpili.

Kwa upande wa kinababa na mamalishe wa Manispaa ya Morogoro na wauzaji wa mboga na matunda walisema wanakumbwa na changamoto ya ugumu wa biashara kutokana na ugonjwa huo.

Yasinta Salumu, anayefanya shughuli zake kwenye Soko la Kuu la Chifu Kingalu, alisema anakumbana na ugumu wa biashara yake ya chakula, na kwamba kwa sasa anapika kilo tano za mchele na bado zikabaki wakati awali alikuwa anapika mpaka kilo 10 kwa siku na wote ulikuwa unaisha.

Mwenyekiti wa Chama cha Wafanyabiashara Ndogo Mkoa wa Morogoro, Faustine Francis, aliwaasa wafanyabiashara hao kuzingatia elimu wanayopewa mara kwa mara juu ya kuepuka misongamano isiyo ya lazima licha ya kuwa wateja wamepungua kwenye masoko mengi.

Naye Msimamizi wa Miradi wa Shirika la Tanganyika la Kuhudumia Wakimbizi (TCRS) Mkoa wa Morogoro, Rehema Samweli, aliwataka wafanyabiashara hao kuongeza juhudi katika kazi na kukumbuka kujiwekea akiba ambayo wataitumia kipindi biashara zao zitakapokwama kama sasa.

Alisema TCRS itaendelea kuwapa elimu ya kumudu kufanya biashara kwa tija na kupambana na changamoto mbalimbali wanazokutana nazo.



Kaimu Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Sengerema, Donati Bunonosi (katikati), akikata utepe kupokea mchango wa madawati 90 kwa ajili ya shule za msingi za Kaningu, Nyashimba na Sotta pamoja na vyoo vipya nane kwa watoto wa kike wa shule ya sekondari Ngoma vyote vikiwa na thamani ya Sh. milioni 26 kutoka kampuni ya OreCorp Tanzania Ltd, katika hafla iliyofanyika wilayani humo, mkoani Mwanza. Kushoto ni Ofisa Uhusiano wa OreCorp, John Bwana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Maboresho mitaala elimu ya juu yatakiwa

**Na Romana Mallya**

KATIBU Mkuu Kiongozi na Katibu Mkuu wa Baraza la Mapinduzi Zanzibar, Mhandisi Zena Ahmed Said, amesema ni wakati mwafaka wa taasisi za elimu ya juu kuangalia ni namna gani mitaala yake inaboreshwa ili iendane na mahitaji ya sasa ya soko la ajira.

Aliyasema hayo jijini Dar es Salaam wakati akifungua Maonyesho ya 16 ya Elimu ya Juu Sayansi na Teknolojia yaliyoandaliwa na Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania (TCU) na kuhudhuriwa na taasisi za elimu ya juu 73.

Alisema Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia imeanza mjadala wa kuona namna ya kuboresha mitaala ya elimu msingi.

“Tume ya vyuo vikuu ina wajibu kisheria kusimamia ithibati na udhibiti wa ubora wa elimu ya juu na kuishauri serikali mwelekeo wa utolewaji wake.

“Nashauri msimamie, upitiaji na uboreshaji wa mitaala ili itoe wahitimu bora wenye kukidhi vigezo kitaifa na kimataifa, ninatoa wito kwa TCU kuongeza jitihada katika uthibiti wa ubora wa vyuo vikuu ili kuhakikisha vinafuata taratibu zilizojiwekea na kutoa elimu iliyokusudiwa,” alisema.

Pia aliwataka wajikite pia kwenye kusimamia masuala ya utafiti na ushauri katika vyuo vikuu.

Mhandisi Zena alivitaka vyuo vikuu viongeze ushirikiano na vyuo vya kati hata vya chini katika mfumo wa kukuza ujuzi na maarifa ikiwa ni pamoja na kujengea uwezo vyuo vya ufundi.

Alisema serikali imepanga kuimarisha mfumo mzima wa kuratibu shughuli za sayansi, teknolojia na ubunifu sambamba na kujenga uwezo wa rasilimali watu kwa kuyaimarisha mafunzo ya walimu katika eneo hilo.

Pia alizitaka taasisi za elimu ya juu kuendelea kufanya utafiti unaojikita katika kutatua matatizo ya jamii na kuwezesha kujikwamua kiuchumi na kuchangia pato la taifa.

“Taasisi za elimu ya juu na zile za utafiti zishirikiane kwa karibu na sekta binafsi hususan ya viwanda na ziweke utaratibu wa kuendeleza teknolojia zinazozalishwa nchini na kuhamaisha matumizi yake ili kuongeza kasi ya kijamii na kiuchumi,” alisema.

Katibu Mkuu TCU, Prof. Charles Kihampa, alisema lengo la maonyesho hayo ni kutoa fursa kwa taasisi mbalimbali za vyuo vikuu kuonyesha kazi wanazofanya vyuoni na kwa kwa wale wanaotaka kujiunga elimu ya juu kufanya uchaguzi sahihi.

Alisema kwa mwaka huu maonyesho hayo yamebebwa na kauli mbiu isemayo, “Kuendelea kukuza na kudumisha uchumi wa kati kupitia elimu ya juu, sayansi na teknolojia.”

Alisema kwa mwaka huu jumla ya taasisi za elimu ya juu 73 zimeshiriki maonyesho hayo ikilinganishwa na taasisi 67 za mwaka jana.

Mkuu wa Wilaya ya Ilala, Ng’wilaguzu Ludigija, akizungumza kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, alivipongeza vyuo nchini kwa kuzalisha wahitimu wenye elimu bora na kueleza kuwa maonyesho hayo ni fursa kwa vijana wanaotaka kupata elimu ndani na nje ya nchi.

Makamu Mwenyekiti wa Bodi ya TCU, Charles Mgone, alisema tume itabaki kuwa taasisi imara na dhabiti Tanzania kikanda na kimataifa kwa kuzalisha wahitimu wabunifu ambao wanakabiliana na matatizo la ajira.

Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. James Mdoe, aliwaeleza wanafunzi wa sekondari na wale wanaotarajia kujiunga na taasisi elimu ya juu, kuwa maonyesho hayo ni muhimu kwao hivyo wachangamkie fursa hiyo.

# Shule Sengerema zapewa msaada madawati, vyoo

**Na Mwandishi Wetu,** SENGEREMA

KAMPUNI ya uchimbaji madini ya OreCorp Tanzania Ltd, imepiga ‘jeki’ ya madawati 90 pamoja na vyoo vipya nane vya wanafunzi wa kike.

Msaada huo una thamani ya Sh. milioni 26, na imetolewa kwa shule nne za Wilaya ya Sengerema, mkoani Mwanza.

Shule zilizonufaika na msaada huo ni za msingi za Kaningu, Nyashimba na Sotta, ambazo zimepata madawati na sekondari ya Ngoma iliyopata vyoo vipya nane kwa ajili ya watoto wa kike.

Akipokea msaada huo kutoka kwa Ofisa Uhusiano wa OreCorp, John Bwana, Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Sengerema, Donati Bunonosi, aliishukuru kampuni hiyo na kusema:

“Mradi wa madini ya dhahabu wa Nyanzaga unaungwa mkono na wakazi wa wilaya hiyo pamoja na mkoa wa Mwanza, ambao wanakaribisha fursa ambazo uwekezaji huu mkubwa utaleta mkoani humo.”

Mssada huo, sehemu ya miradi wezeshi ya kijamii ya hivi karibuni iliyokamilishwa na kampuni hiyo tangu ilipochukua uongozi wa mradi huo mwaka 2015.

Aprili mwaka huu, kampuni ya OreCorp ilitoa shilingi milioni 45 kwa ajili ya ujenzi wa kituo cha polisi cha Ngoma. Miradi mingine iliyotekelezwa na kampuni hiyo ni ujenzi wa madarasa kwa ajili ya shule mbalimbali zilizopo wilayani humo, ujenzi wa mashimo ya vyoo, ukarabati na usambazaji wa maji ya visima.

Mingine ni ukarabati na uimarishwaji wa barabara za mitaa, kuongeza kina cha bwawa la Sotta, usambazaji wa vifaa vya ujenzi ikiwemo saruji, mabati na mchanga kwa ajili ya ujenzi wa zahanati na ofisi za halmashauri ya wilaya, na kukuza na kusambaza miche ya miti zaidi ya 11,000 kwenye maeneo ya shule na makazi ya wanajamii.

Mchango wa ujenzi wa vyoo na madawati uliungwa mkono na Mkurugenzi Mtendaji wa Wilaya ya Sengerema Desemba 2020, na ujenzi ulianza rasmi Juni 2021.

Meneja Mkuu wa OreCorp Tanzania, Damien Valente, alisema kuwa “OreCorp inajivunia kuendelea kutoa mchango kwa watoto ili kuwa na mazingira salama na tulivu ya kujifunzia na kuendeleza masomo yao.


Ukurasa 12

Mtafiti aanika Ziwa Victoria limejaa tani 150 za plastiki, nywele za saluni


Ukurasa 13

**MIAKA MITATU YA EWURA KATIKA VITA DHIDI YA ADUI WACHAKACHUAJI MAFUTA**

OFISINI KWA MWANAHABARI...

# Simulizi ‘msimamo’ na ‘uwazi’ zilivyo silaha kuishinda rushwa ngono kazini

## •Uamuzi menejimenti ni sheria tosha kumaliza

**Na Mary Geofrey**

**JUMAMOSI iliyopita, ilikuwa na sehemu ya kwanza ya simulizi ya rushwa ya ngono katika sehemu ya kazi, vyombo vya habari, endelea na simulizi halisi:**


Kinamama wanahabari wakiwa kazini. **PICHA: MTANDAO.**

LICHA ya sehemu muhimu kwa umma, vyumba vya habari vimo katika orodha ya kugubikwa na matukio ya ukatili kijinsia, wanawake.

Inafahamika, ukatili wa kijinsia unaangukia chochote kinachosababisha madhara ya mwili, kingono, kisaikolojia au mateso kwa wana jamii, kama kutishiwa maisha, kunyimwa uhuru hadharani au kwa kificho, kupigwa na madhara zaidi.

Karaha inaangukia mtu kushikwa maumbile, anataniwa, kuchekwa kulingana na maumbile katika hali ya kumdhalilisha.

Chama cha Wanahabari Wanawake Tanzania (TAMWA) chini ya mradi wa Wanawake katika Vyombo vya Habari, imeanzisha mpango mkakati kupunguza ukatili wa kijinsia katika vyombo hivyo.

**‘KILICHOMO SEBULENI’**

Utafiti wa Nipashe umeibua uhalisia wa matukio katika vyumba vya habari. Mwanahabari kutoka Radio Wapo, Mwanahamisi (jina la pili tunalo), anaeleza sakata alipoanza kazi ya uanahabari, alivyokutana na madhila ya kijinsia kutoka kwa mhariri anayemsimamia.

Anasimulia magumu ya kupigiwa simu usiku wa manane na mhariri aliyekuwa na jukumu kumpangia kazi, (jina tunalo) kumshawishi kimapenzi., akiendeleza simulizi:

“Ananiuliza maswali ya karaha tena anazungumza zaidi ya saa tatu akilazimisha nizungumze yale masuala ya mapenzi.”

Mwanahamisi anaendelea: “Nilipoacha kupokea simu ndipo tatizo lilipoanza kuwa kubwa, kwa sababu nilikuwa nikifika ofisini ananitukana mbele ya kikao cha waandishi wa habari wenzangu kwa madai kuwa namdharau na simu zake sipokei.

“Alikuwa hasemi mbele za watu kuwa ananishinikiza kuongea naye mambo ya mapenzi. Alikuwa anadai sikupokea simu wakati alitaka kunipa majukumu ya kazi.”

Mwanahamisi anakumbushaa nukuu za kufokewa: “...mwandishi wa habari unazimaje simu yako, unaachaje kupokea simu? Unajua nilitaka nikuambie nini? Unajua nilitaka nikupangie kazi gani? Kama huwezi kupokea simu huna sifa ya kuwa mwandishi wa habari!”

Anasimulia namna kero ilivyoendelea kumuumiza na baada ya bosi wake kuacha kutoa kazi zake, ilimuingiza Mwanahamisi katika mazingira magumu.

“Kwa sababu nilikuwa mdogo na nilihofia angenifukuza kazi kama ningemsemea kwa viongozi wakuu wa ofisi, niliendelea kuvumilia huku nikishikilia msimamo wangu kuwa sitaruhusu lengo lake litimie,”anasema.

Mwanahamisi anasema, ikabainika ni tabia yake kwa wanahabari wengi wanawake ofisini, huku kati yao ilifanikisha lengo, huku waliokataa walipitia ukatili mkubwa.

Anasema mwisho wa tabia hiyo ulifika baada ya wao kuanza kulalamika na ndipo walibaini wote walisumbuliwa.

“Bosi wetu, Mkurugenzi alisikia akatuita na kutuhoji mbele yake, kila mmoja alieleza alichofanyiwa na huo ndio ulikuwa mwisho wake wa kufanya kazi, kwani alifukuzwa,” anasimulia Mwanahamisi.

Mama huyo anasema, siyo wanawake wote wanaomudu kuvumilia kama yeye, maana wabishi wengi wameangukia kunyanyasika kimapenzi.

Flora (jina la pili tunalo) anayefanya kazi Radio EFM, naye ana simulizi kwamba kabla ya kuajiriwa aliko sasa, safari yake ilipitia chombo kimojwapo nako anakakutana na ukatili kijinsia kutoka kwa mhariri aliyemsimamia.

Anasimulia alipomkatalia uhusiano, alianza kukutana na visa vilivyomkarahisha ashindwe kufanyakazi zake kwa weledi.

Flora anasema, bosi huyo alijenga tabia ya kufika mapema na hata kama muda wa kuripoti haujapita, alichora mstari kwenye daftari ili mama huyo aonekane kachelewa.

Anasema, pia bosi huyo aliendа mbali kuanza kumkosoa wakati akifanya kipindi ‘mubashara’ kinyume na taratibu za kitaaluma.

“Nikiwa studio natangaza anaingia kudai nimekosea na kuacha mlango wazi ili tu anitoe kwenye lengo na kunifanya nionekane sijui kazi yangu,” anasema Flora, akidokeza kwamba, hakuweza kumripOti, akihofia kufukuzwa. Mkataba wake wa kazi ulipoisha aliengʉliwa.

“Nilishindwa kuendelea na ajira yangu kwa sababu nilionekana ni mchelewaji, sijui kutangaza na sipo makini katika utekelezaji wa majukumu yangu, hivi vyote vilisababishwa na yule bosi wangu,” anasema Flora.

Beatrice Munisi, mwanahabari wa kujitegemea, ana simulizi alivyotumikia gazeti moja, akikumbuka ukatili wa bosi wake. Naye anangukia sumulizi za awali: “Nilikuwa sijaajiriwa, nafanya kazi na kulipwa kulingana na kazi. Kwa hiyo, kwa sababu alikuwa hazitoi nilikuwa nakosa malipo.”

INAENDELEA UK.14

MAZINGIRA

ULIVYO UTAJIRI WA MAJI MWANZA...

# Mtafiti aanika Ziwa Victoria limejaa tani 150 za plastiki, nywele za saluni

- Samaki asilimia 20 wamemeza plastiki
- Wakubwa na wadogo wamezana balaa


**Na Anthony Gervas, Mwanza**

ZIWA Victoria ni moja ya vyanzo muhimu kiuchumi na biashara katika jiji la Mwanza. Pia, ni kituo nyeti cha uwekezaji katika Kanda ya Ziwa.

Unapotaja utalii, ziwa hilo ni kivutio kikubwa cha wageni wanaoingia jijini humo, penye mandhari ya kipekee kuanzia yanayotajwa kila siku; milima yenye miamba ya mawe makubwa, visiwa mbalimbali vinavyotumika kwa makazi ya watu na shughuli za uvuvi.

Humohumo ziwani, kuna utajiri mwingine unaobeba mazingira na uchumi. Hao ni samaki wa aina mbalimbali wakiwamo sangara na sato, wanyama kama kiboko na mamba, wenye sifa kuishi majini na nchi kavu.

Ziwa hilo hadi sasa linakabiliwa na uchafuzi mkubwa wa mazingira ndani ya ya maji, kutoka watumiaji wakuu walioko jirani na Ziwa.



Uchafu plastiki katika Ziwa Victoria, jijini Mwanza. **PICHA: ANTHONY GERVAS.**

**MWANAZUONI WA UDSM**

Mhadhiri Msaidizi wa Chuo Kikuu cha Dar-es salaam,(UDSM) Bahati Mayoma, anaeleza uchafuzi wa mazingira uliopo sasa kuwa mkubwa unaoweza kuhatarisha afya na maisha ya watu wanaotumia maji hayo au huduma zake, ikiwamo kupata magonjwa kama vile kansa, kwa kurejea utafiti uliofanywa.

Mayoma anayefanya utafiti, anataja kubaini kuwa chini ya ziwa hilo kumegubikwa na vipande vidogo vya chupa za plastiki zilizozama majini na kusambaa ziwani kote, hata zikatengeneza sakafu ya taka hizo, pamoja na nyavu za kuvua samaki, kama vile makokolo.

Mwanazuoni huyo, anasema utafiti wake wa uchafuzi wa mazingira ya ziwa hilo unaokadiriwa ifikapo mwaka 2050 kama hakuna hatua ya udhibiti, uzalishaji taka za plasitiki utaongezeka zaidi.

Anasema, utafiti unaonyesha hivi sasa kuwa taka za vipande vya plastiki vilivyozama na zilizosambaa chini ya maji ni zaidi ya tani 150, ambazo madhara yake ni makubwa kwa afya na maisha ya binadamu wanaotumia huduma ya maji hayo na viumbe vilivyomo kama samaki.

Mayoma anasimulia kuwa, nyavu za kuvulia samaki na makokolo zinazotelekezwa na wavuvi zinapokuwa chakavu baada ya kutumika, huzama chini ya maji na kuungana na taka za vipande vya chupa za plastiki na kutengeneza sakafu ya taka hatarishi kwa afya na maisha ya watu.

"Kuna taka za vipande vidogo vidogo vya plastiki vimezama chini ya ziwa victoria na kusambaa na zingine kuelea juu ya maji, nyavu za kuvulia samaki na makokolo zinazotelekezwa na wavuvi baada ya kuchakaa na kuzama chini, hivyo vyote vimegeuza chini ya ziwa (Victoria) kuwamo sakafu ya taka," anaeleza Mayoma.

Kiuchumi, inaelezwa zaidi ya watu milioni 30 wananufaika moja kwa moja na vyanzo vya maji, zikiwamo maziwa makuu.

Anasema, utafiti uliofanyika mwaka 2014 iligundua asilimia 95 katika Ziwa Victoria kuna taka za aina hizo na mwaka 2015 utafiti mwingine nao uligundua samaki waliomo wastani wa mmoja kati ya watano wanabainika kumeza vipande hivyo vya plastiki.

Mayoma anasema, ni uchafuzi wa mazingira unaosababishwa pia na wingi wa kazi Kanda ya Ziwa, akitahadharisha madhara ya plastiki huwa hayashi na zina uwezo wa kudumu miaka 100, iwapo ziatasambazwa ovyo.

Hadi sasa kuna mkakati kitaifa wa kupunguza matumizi yasiyokuwa endelevu katika bidhaa za plastiki. Ni hali inayotajwa kupunguza zaidi uchafuzi wa mazingira.

Nchini, utafiti unaonyesha bidhaa nyingi za plastiki na nyavu za kuvua samaki na makokolo hazielei juu ya maji Ziwa Victoria, bali zinazama.

Katika utafiti mwingine uliofanywa na mtaalamu huyo, umegundua samaki aina ya sangara kila siku wanameza samaki wadogo saba aina ya furu, ambao ni jamii ya sato na kusababisha upungufu wa samaki aina hiyo kwa watumiaji wake.

> "Kuna taka za vipande vidogo vidogo vya plastiki vimezama chini ya ziwa victoria na kusambaa na zingine kuelea juu ya maji, nyavu za kuvulia samaki na makokolo zinazotelekezwa na wavuvi baada ya kuchakaa na kuzama chini, hivyo vyote vimegeuza chini ya ziwa (Victoria) kuwamo sakafu ya taka," anaeleza Mayoma.

**MBINU MBADALA ZILIVYO**

Mtafiti Mayoma anataja mbinu mbadala au teknolojia inayoweza kutumika kupunguza uchafuzi wa mazingira ziwani humo au usambaaji wa taka hizo, ni pale wenye viwanda vikubwa na vidogo wanaofanya ubunifu wa kuzalisha upya bidhaa zingine za plastiki zinazotumika mbadala wa kuzitupa.

Anatoa mfano, viwanda vinavyozalisha chupa za maji na juisi za plastiki Kanda ya Ziwa ni vingi na vinatakiwa kuwa na ubunifu mbadala wa kutengeneza malighafi mpya pindi zinapomaliza matumizi ya awali, ili kuongeza uchumi na faida kwa umma.

Mbinu nyingine ni watoto kufundishwa usafi wa mazingira, waweze kuepuka utupaji ovyo wa taka, kupitia wadau wa mazingira wanaposhirikiana na serikali na taasisi za kiraia, wameshaanzisha kampeni ya usafi wa mazingira nchini.

Anataja njia nyingine ni kuelimisha wananchi kuhusu madhara ya utupaji ovyo taka na kusimamia sheria; miongozo ya kudhibiti hali uchafuzi huo; na Ziwa Victoria linategemewa kiuchumi, kibiashara kwa karibu hasa na majirani wa Afrika Mashariki wanaopakana nao.

Mayoma anasema Tanzania inajaribu kuzuia taka kuingizwa katika ziwa hilo kupitia mito, hali kadhalika kuna uchafuzi unaotokea kwa majirani wanaopakana na Ziwa Victoria.

Hadi sasa Tanzania inamiliki asilimia 51 ya Ziwa Victoria, katika ukanda wake ulioko katika Afirika Mashariki na kwamba jamii ndiyo kinara wa rekodi ya utupaji taka.

**UCHAFU NYWELE**

Hali kadhalika, wadau wa mazingira na uvuvi wanadai nywele bandia za wanawake maarufu rasta, au wigi zinapomaliza muda wa kutumika hutupwa ovyo katika maeneo mbalimbali kisha kusafirishwa na vyanzo vya maji hadi ziwani.

Nywele za kawada watu wanaponyolewa hupelekwa dampo au kutupwa kwenye vyanzo vya maji na baadaye husafirishwa na maji hadi ziwani humo, zinazodaiwa siyo rahisi kuoza, pia ni hatari kwa afya ya binadamu anayetumia huduma za maji hayo.

Mkazi Juvenali Matagili, anaitaka mamlaka ya usafi wa mazingira, kuhakikisha taratibu za kisheria zinafuatwa kudhibiti utupaji ovyo nywele za binadamu ziwani, ilhali ni vitu visivyooza kirahisi.

"Nywele zinazonyolewa kwa binadamu hutupwa ovyo kwenye vyanzo vya maji, kama vile kwenye mito ambazo haziwezi kuoza kwa miongo mingi, husambaa kisha kusafirishwa na maji hadi ziwani," anasema.

Mdau huyo wa uvuvi anakiri kuwapo zana za nyavu na makokolo kutumika vibaya katika uvuvi, pamoja na kutelekezwa na wavuvi majini, pale nyenzo hizo zinapochakaa.

MAZINGIRA

# MIAKA MITATU YA EWURA KATIKA VITA DHIDI YA ADUI WACHAKACHUAJI MAFUTA

## •Ushindi? Umepungua kutoka 80% hadi 4%



Kituo cha kujaza mafuta ya petroli.

**Na Augusta Njoji, DODOMA**

KWA muda mrefu kumekuwapo kilio cha uchakachuaji mafuta ya petroli, hivyo kuhatarisha vyombo vya moto, hususani magari.

Baada ya tatizo hilo kuwa sugu, Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), jicho la kiserikali katika eneo hilo iliamua kuingilia kati kwa kuchukulia hatua jambo hilo litowekwe kabisa.

Meneja wa Mawasiliano na Uhusiano wa EWURA, Titus Kaguo, anasema suala hilo limetatuliwa kwa kiasi kikubwa, baada ya EWURA kuja na programu ya kuweka vinasaba kwenye mafuta hayo, iliyowezesha kupunguza athari hizi kwa kiasi kikubwa.

Kaguo anasema, ni hatua iliyofanikisha kupunguza uchakachuaji mafuta kutoka asilimia 80 za mwaka 2017 hadi asilimia nne za mwaka jana.

Akizungumza na wadau wa Taasisi ya Maendeleo ya Viziwi Tanzania (TAWAVITA), Kauo anasema EWURA ilianzisha programu hiyo, mnamo Septemba mwaka 2010, ikiweka vinasaba kwenye mafuta yanayotumika nchini.

Katika mjumuiko huo akimwakilisha Mhandisi Godfrey Chibulunje, Kaimu Mkurugenzi wa EWURA, Kaguo, anasema lengo kuu la kuchukuliwa hatua hiyo ni baada ya kuona kuwa uchakachuaji na ukwepaji unafanywa na wajanja wachache, hali yenye athari kufikia mazingira ya ushindani na haki.

"Uchakachuaji wa mafuta ni changamoto kubwa hapa nchini, EWURA kwa kuliona hilo, imepambana na kufanikiwa kupunguza uchakachuaji kutoka asilimia 80 hadi kufikia asilimia nne mwaka 2020,"anasema.

Kagua anafafanua kuwa mbinu zilizotumika ni pamoja na mwaka 2010, Chuo Kikuu Cha Dar es Salaam (UDSM), kilifanya utafiti kuhusu matumizi ya vinasaba na kubaini kati ya mwaka 2010 hadi 2013 kulikuwapo ongezeko la mapato ya serikali kupitia kodi, ziada ya Sh. bilioni 468.50, manufaa yanayoendelea kupatikana.

**UCHAKACHUAJI MPYA**

Kaguo anaeleza kuwa pamoja na jitihada hizo za EWURA, bado ilibaini uchakachuaji mpya wa mafuta, ambao katika namna hiyo mpya unachangia kuipotezea mapato serikali.

Anasema, katika kupambana na uchakachuaji mafuta, wamebaini baadhi ya wafanyabiashara wasio waaminifu wanachanganya mafuta yaliyolipiwa kodi na yasiyolipiwa kodi.

"Moja ya jukumu la EWURA ni kudhibiti ubora na usalama na tija ya watoa huduma na uchakachuaji wa mafuta, ni changamoto kubwa nchini katika sekta ndogo ya mafuta," anafafanua.

"Kazi kubwa imefanyika ya kudhibiti uchakachuaji wa kuchanganya petroli au dizeli na mafuta ya taa, lakini sasa kumeibuka uchakachuaji wa kuchanganya mafuta yaliyolipiwa kodi na yasiyolipiwa," anabainisha Kaguo.

Mwana- mawasiliano huyo wa EWURA, anasema ni takribani nusu ya mafuta yanayoingizwa nchini ni mafuta yanayoenda nchi jirani, vilevile kuna mafuta yenye msamaha wa kodi na uwezekano wa mafuta ya magendo kuingia nchini.

"Vitendo vya kuingiza mafuta kwenye soko ambayo hayajalipiwa kodi pia vilikithiri. Mafuta hayo ni yale ya kwenda nchi jirani yaliyosamehewa kodi na ya magendo kutoka nchi jirani, hasa kwa mikoa ya Kanda ya Ziwa na Kanda ya Kaskazini,"anasema.

Kaguo anasema, ni hali iliyosababisha kuwapo ushindani usio sawa kwa wauzaji mafuta nchini, hata kuikosesha serikali mapato.

**HATUA ZILIZOCHUKULIWA**

Anasema mwaka 2007 EWURA ilianza kuchukua sampuli za mafuta kutoka maghala ya mafuta na vituo vyake kupima ubora uliopo, kwa ajili ya kukagua hali ya uchakachuaji na imeshachukua hatua za kisheria dhidi ya wahusika waliokosa.

Hata hivyo, Kaguo anakiri kwamba pamoja na hatua zilizochukuliwa, hazijaweza kumaliza tatizo la uchakachuaji, kwani wapo wafanyabiashara wasio waaminifu wanaitrumia mbinu za ziada na kisha wakakidhi viwango vya Shirika la Viwango Tazanznia (TBS).

"EWURA iliona suluhisho ilikuwa ni kutafuta teknolojia ambayo inaweza kung'amua uchakachuaji na uingizwaji wa mafuta ambayo hayajalipiwa kodi hata ukifanyika kwa kiwango kidogo, ndipo ikaonekana kuwa teknolojia sahihi ilikuwa kuweka vinasaba kwenye mafuta inayotumika na nchi mbalimbali duniani,"anaeleza

Hata hivyo, msemaji huyu wa wadhibiti na wasimamizi wa mafuta hayo, anasema teknolojia ya kuweka vinasaba imesaidia kwa kiasi kikubwa kudhibiti uingizaji mafuta hayo yasiyolipiwa kodi.

**HALI YA USHINDANI**

Pia, anasema matumizi ya teknolojia hiyo yamechangia kuleta ushindani sawa katika soko na mapato ya serikali yakaongezeka, kwani sasa kuna kiasi kikubwa cha mafuta kinacholipiwa kodi.

Kaguo anatoa mfano wa kiasi cha mafuta ya dizeli kinachotumika nchini na kulipiwa kodi, sasa kimeongezeka kutoka wastani wa lita milioni 80 kwa mwezi mwaka 2010 hadi kufikia ita milioni 184 kwa sasa.

Vilevile, kiasi cha mafuta ya petroli kinachotumika nchini na kulipiwa kodi kimeongezeka kutoka wa lita milioni 40 za mafuta kwa mwezi mwaka 2010 hadi lita milioni 136 kwa sasa.

**TEKNOLOJIA VINASABA**

Kaguo anaieleza teknolojia ya vinasaba, kwamba inahusisha kuweka kemikali maalumu kwenye mafuta, inayoweza kutofautisha nishati husika na mafuta, ambayo hayajawekewa kemikali husika.

Pia, anasema teknolojia hiyo inatakiwa kuwa na vifaa maalumu vya kupima na kung'amua kwa usahihi mkubwa mafuta yenye kiwango stahiki cha vinasaba, pia yale yamekosa au yana kiwango pungufu.

**UAGIZAJI MAFUTA**

Kuhusu namna EWURA ilivyookoa fedha kwa kushirikiana na Wizara ya Nishati na Madini, ni kwamba aliandaa Mfumo wa Uagizaji wa Pamoja (BPS) wa Mafuta nchini.

Kwa mujibu wa utafiti uliofanywa na UDSM Aprili 2014, ulibaini BPS imesaidia kupunguza gharama Sh. bilioni 121.57 kwa mwaka. Anafafanua ni kupungua gharama za usafirishaji kwa kiasi cha mabilioni kila mwaka.

Kaguo anaendelea: "Kupungua kwa gharama za demurrage kwa Sh. Bilioni 25.7, kupungua kwa gharama za uagizaji mafuta kutokana na maboresho ya mikataba kwa Sh.bilioni 13.95 kwa mwaka."

Anaweka bayana faida iliyopatikana kwa kutumia mfumo wa pamoja wa BPS kuwa ni kupatikana kwa taarifa sahihi za kiwango cha mafuta kinachoingizwa nchini na hivyo kuongeza mapato ya kodi ya serikali kwa kiwango cha asilimia 24 kwa mwaka 2012.

"Kuongeza ufanisi katika udhibiti wa bei za mafuta kwa kuwa na gharama halisi za mafuta yanayoingia nchini. Kurahisisha udhibiti wa ubora wa mafuta yanayoingizwa nchini chini ya mfumo huu,"anasema Kaguo.

Anasema EWURA itaendelea kusimamia taasisi na mfumo kwa ujumla, kutokana na kuwa EWURA ina utaalamu mpana zaidi na taarifa za mwenendo wa soko la mafuta ndani na nje ya nchi.

"Kutokana na ubora wa mfumo huu, taasisi nyingi za hapa nchini zimeitembelea EWURA kujifunza namna ya kuanzisha na kutekeleza mfumo wa uagizaji wa bidhaa kwa pamoja (mfano mbolea na Dawa, Bodi ya Sukari na ununuaji wa dawa za maji MSD)."anasema.




Polisi wa Usalama Barabarani, akikagua lori la kusafirisha mafuta. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**

AFYA

## WAKATI KUNA UZINDUZI WA CHANJO;

# Siasa za barakoa, kukubalika ziko hivi...

**Na Michael Eneza**

SUALA la kuvaa barakoa bado halijaanza kutambuliwa katika tafsiri ya lazima kwa wakazi wa jiji la Dar es Salaam na kwingineko nchini.

Wakati kuna tafsiri hiyo, jana hatua ya mapambano ilifika mbali kwa kutolewa chanjo rasmi, ikiongozwa na Rais Samia Suluhu Hassan.

Katika maeneo hayo, baadhi ya wakazi wanaanza tena kuchukua umakini tangu linaloitwa wimbi la tatu kuanza kwa kasi.

Kunatajwa muundo tofauti na vilivyotangulia, ingawa haieleweki sana. Kwa jumla, kumekuwapo mawimbi mawili, ikianzia mwezi Machi, halafu mwanzoni mwa mwaka huu.

Nchi za nje kuna wimbi la nne. La kwanza likiwa la mwishoni mwa mwaka 2019 huko Wuhan, China halafu likasambaa Ulaya, kasha Marekani Kakazini na Kusini, hadi Bara Asia, kulikowaka moto.

Katika ujumla, kumekuwapo mawimbi tofauti na historia za kuenea corona kati ya nchi moja na nyingine. Ndio namna imesikika nchini jana Rais Samia Suluhu katika uzinduzi, akitaja mikoa kadhaa kama Dar es Salaam, Kagera na Kilimanjaro, ilivyofikiwa.

Wimbi la kwanza limeitwa Covid-19 na ugonjwa ukifahamika kutokana na virusi vya corona, vikimaanisha, "kirusi mviringo chenye sura ya kupatwa jua, ambako seli za ncha ya kirusi hicho ni 'mkuki' unaolenga kokote mwilini mwa binadamu.|

Dawa na chanjo zilizotengenezwa zimeulenga muundo wa kirusi hicho; 'u-protini' wake na jinsi ya kuulemaza. Ni 'mkuki' wa kudhibiti ncha yake kuwa butu.

Rais Samia alipoingia madarakani, tayari wimbi la tatu duniani lilishaanza. Mawimbi hayo yana kawaida yanapogundulika eneo fulani, haichukua muda kufikia kwingine, hata unazuka ubishi kirusi hicho kilianzia wapi.

Septemba mwaka jana, Uingereza ilipambana nayo ikiita ni 'kirusi cha Afrika Kusini' huku wanaotajwa wakikanusha vikali.

Kirusi cha pili kilianza na mazingira tatanishi zaidi, kati ya Marekani na Uingereza, lakini kama ilivyokuwa cha Afrika Kusini au na Uingereza, haikuwa na nguvu sana, licha ya kutofautiana katika maeneo kadhaa na cha awali kutoka Wuhan, China.

Serikali ya China imekanusha uvumi na tafsiri, ila inabaki na kigugumizi kueleza amna kirusi cha mnyama kama popo, kilivyobadilika kuwa cha binadamu ikikiwa na kasi kubwa ya kuambukiza.

Hadi mwanzo wa mwezi huu, inakadiriwa takriban watu 400,000 wameshakufa nchini humo. Pia licha ya kuwa virusi vya awali na vya sasa kuleta maafa makubwa duniani, Afrika bado maafa yapo kiwango cha chini zaidi.

Maeneo mengi duniani, mtu kutoka nje ni kujiweka karibu na madhara ya corona na mara nyingine virusi vinapenya mianya kuzunguka barakoa, mathalani juu ya pua.

Ndiyo sababu za msingi za 'lockdown' (kufungia watu ndani wasitoke nje ila kwa dharura maalum) ambazo sasa kuna maeneo wanabishia au kuzikataa, barakoa, pia chanjo katika mazingira tofauti.

Wakati Rais Samia, jana alitoa vigezo kadhaa kukubali kuchanja dhidi ya madhara virusi corona, naye Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Dorothy Gwajima, alifafanua nafasi na umuhimu wa dawa hizo, akitumia utaalamu wake kwa kina.



Mhamasishaji Waziri Dk. Dorothy Gwajima, akiwa amevaa barakoa. **PICHA: MTANDAO.**

Yako majadiliano yaliyofika katika magazeti na mitandao ya kijamii kuhusu njama za kutengeneza barakoa na hata chanjo, na baadhi walitoa hoja za kutengenezwa virusi vya Covid-19, kwamba ni

mkakati wa kupunguza watu duniani.

Hata hivyo, ni kama darasa limeanza kuwa bayana, nchini Marekani, sehemu kubwa ya maambukizi mapya ni kwa waliokwepa chanjo, kwa visingizio kadhaa.

Tofauti kuu iliyopo sasa, ni chanjo zilizoandaliwa kirusi cha awali cha Covid-19, zimepungua uwezo kuzuia badilika cha tatu, ambacho kiligunduliwa nchini India kwa jina Delta (herufi D).

Israel inasema, chanjo yenye nguvu zaidi ya 'Pfizer/BioNTech' ya kampuni za Marekani na Ujerumani, ina uwezo wa asilimia 40 kuzuia maambukizi ya 'Delta.'

**USHUHUDA WA DK. MSHANA**

Kuna ushuhuda wa Dk. Rogate Mshana, Mkurugenzi Mstaafu wa Fedha katika makao makuu ya Fungamano la Makanisa ya Kilutheri, Geneva amepona hospitalini KCMC, akikiri kutovaa barakoa kulimponza.

Askofu Mkuu wa Jimbo Kuu Katoliki la Dar es Salaam, Jude Ruwaichi, mnamo mwezi Aprili, alitoa angalizo la kuwapo tatizo la kutovaa, licha ya kutolewa wito.

# Simulizi 'msimamo' na 'uwazi' zilivyo silaha kuishinda rushwa ngono

**INATOKA UK.11**

Anaeleza bosi alimuongezea adhabu, ya kumpangia kufanya kazi za mahakamani pekee na licha ya yeye kutii, kazi zake hazikutumiwa, hadi pale alipojisikia.

"Niliteseka sana kisaikolojia, pia kiuchumi niliyumba kiasi kwamba nilitamani kuacha kazi nifanye shughuli nyingine. Lakini, niliendelea kujipa moyo kwa kuendelea kuvumilia zaidi ya mwaka mmoja," anaseme Beatrice.

Baada ya mwaka mmoja, anasema bosi huyo alihamishwa kikazi kwenda kituo cha mbali na ndio ukawa mwanzo wa uhuru wake kufanya kazi kwa ufanisi kiuchumi na uhuru binafsi.

Katika kipindi chote cha mpito anataja 'alibebwa' na biashara ndogo aizofanya.

**WAHARIRI WANASEMAJE**

Mhariri, Isaac Kijoti, anakiri kuwapo mambo ya aina hiyo, akiwa na ushuhuda wa malalamiko na siyo taarifa rasmi.

"Kama yupo anayefika hatua ya kusema au kuripoti ngazi za utawala basi ujue huyo amefikia hatua ya kuacha kazi. Vinginevyo vitendo kama hivi haviripotiwi moja kwa moja," anasema Kijoti.

Anasema kukosekana uthubutu wa kuripoti mikasa uanchangiwa na kuhofia ajira, kwa maana wanaweza kufukuzwa kazi.

Pia, anasema kinamama wanashindwa kuripoti kwa sababu wahariri wana mamlaka makubwa kwenye chombo cha habari.

"Utaona kabisa aliyemshtaki ataendelea vipi kufanya naye kazi, ndio maana wanaamua kunyamaza na kuvumilia," anasema Kijoti.

Mhariri wa Habari wa gazeti la Majira, Stellah Arron, anakiri ukatili kijinsia kwenye vyumba vya habari hayaripotiwi, kwa sababu wanaofanyiwa wanahofia kupoteza ajira zao.

Pia anadokeza, pia kuwapo dhana wanawake kuripoti matukio hayo ni kujidhalilisha, hivyo wanaamua kubaki wakimya.

"Mfano ukiripoti mhariri fulani amekutaka kimapenzi, akachukuliwa hatua, ukienda ofisi nyingine kufanya kazi, yule bosi atamuambia bosi mwingine kuwa una tabia mbaya na huna uwezo wa kufanya kazi.

"Sasa integemea mapokezi ya huyo bosi mpya, lakini hasara inakuwa kwa mwandishi anaendelea kupitia ukatili," anasema Stellah.

Anasema katika kipindi chake cha kuwa mhariri anayewapa majukumu wanawake, amekutana na matukio hayo na amewasihi kuwapuuza wanaowafuata, waendelee kutekeleza majukumu yao.

Anashauri elimu utolewe kwenye vyombo vya habari kudhibiti matukio hayo.

**SERA/ MUONGOZO MCT**

Sera ya Jinsia Kwenye Vyombo vya Habari ya Baraza la Habari Tanzania (MCT), mwaka 2019, inataja baadhi ya unyanyasaji kazini uliokithiri kazini ni wa ngono, kinamama wanaishia kutishiwa, kufedheheshwa na kutukanwa.

Ni sera inayoanika namna ya kuukabili, ikiwamo kulifikisha suala kwa msimamizi wao au Idara Rasilimali Watu.

**TAMWA JE?**

Mkurugenzi wa Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake (TAMWA), Rose Reuben, anasema wanatekeleza mradi huo wakifahamu kuwapo tafiti zinazoonyesha zipo rushwa ya ngono katika vyumba vya habari.

"Wakati huo huo, wanahabari wameonekana kuwa kimya kuhusu matukio hayo, aidha kwa kuogopa kupoteza ajira zao au pengine wakichelea kuaibika," Reuben anasema.

Anasema ni hali inayoshusha utu, kudhalilisha waathirika, kuwapa msongo wa mawazo na kutojiamini kazini, huku matukio mengi hayaripotiwi.

Rose anakiri TAMWA inatambua Sheria ya Rushwa ya Ngono inayosimamiwa na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa(TAKUKURU).

"Tunataka wanahabari wapaze sauti zao, tuvunje ukimya, wayazungumze yanayowasibu na kuondoa kabisa ukatili wa kijinsia aina hii," anasema Rose.

Anarejea watafiti kimataifa, Barton A na Storm, (2014) walibaini asilimia 48 ya wanahabari wanawake waliohojiwa walikiri kukumbana na rushwa ya ngono ofisini na asilimia 83 kati ya hao, hawakuyaripoti matukio hayo.

Anaeleza haja ya waathirika kujengewa uwezo wa kukusanya vidhibiti vya uhakika vinavyosaidia vyombo kusimamia udhibiti ea mikasa hiyo, kupitia ushirikiano na serikali, taasisi za habari, pia jinsia.

**TAKUKURU**

TAKUKURU katika kudhibiti rushwa ya ngono kazini, ilisaidia kutafiti kwa lengo kuwezesha upatikanaji taarifa za kisayansi kusaidia kukabili vitendo hivyo katika taasisi za elimu ya juu nchini.

Kurejea Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa ya Mwaka 2007, TAKUKURU ina wajibu wa kuzuia rushwa katika taasisi za umma na binafsi kwa kufanya chambuzi za mifumo katika taasisi ili kubaini mianya ya rushwa na kisha kutoa ushauri wa namna bora ya udhibiti.

Aliyekuwa Mkurugenzi wa TAKUKURU, Brigedia Jenerali, John Mbungo, katika uzinduzi wa ripoti hiyo, Juni mwaka jana, alisema vita ya rushwa nchini, bado ya ngono ina malalamiko.

Anatoa sababu ya kuwapo huko kunachangiwa na sababu nyingi, ikiwamo matumizi mabaya ya madaraka; mikakati dhaifu ya kutekeleza sheria za rushwa ya ngono; uelewa duni; kutotambua kina na athari za tatizo rushwa ngono; na jamii kuionea aibu.

Hapo inatajwa zao lake ni waathiriwa wa rushwa ngono wanaendelea kuumia kimya kimya na wanaotenda wanaendelea na vitendo hivyo, bila kuchukuliwa hatua stahiki kisheria.

Mwisho



## HABARI DODOMA

## 'Walimu msiwe kikwazo elimu'

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

MAKAMU Mwenyekiti wa Halmashauri ya Chamwino, Keneth Yindi, amewataka walimu wakuu wa shule za sekondari na msingi kutokuwa kikwazo cha ufaulu kwa watoto walio katika madarasa ya mitihani ya taifa.

Yindi alitoa rai hiyo jana alipozungumza na watumishi wa idara mbalimbali kwenye kikao cha dharura cha maendeleo kilichofanyika Kata ya Buigiri wilayani Chamwino.

Akizungumza kwenye kikao hicho, alisema baadhi ya walimu wakuu hawana ushirikiano na wazazi, jambo linalosababisha kukwamisha ufaulu wa watoto kwenye wilaya hiyo.

"Ninasema haya mimi kama kiongozi wa halmashauri hii ya Chamwino, kuna baadhi ya walimu wakuu wa sekondari wanawafukuza wanafunzi kwa vigezo vya kukosa michango isiyokuwa na tija, hali ambayo inaweza kutupatia alama ya zero (sifuri)," alisema.

Yindi ambaye ni Diwani wa Buigiri, aliwataka wazazi kutoa ushirikiano kwa watoto wao kwa ufuatiliaji wa masomo badala ya kuwaachia walimu.

Alisema ushirikiano huo ukifanywa kati ya pande zote, halmashauri itapanda katika ufaulu na hatimaye kufanya vizuri kwenye sekta hiyo ya elimu.

Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) katika kata hiyo, Elisha Mtamwa, aliwaomba viongozi wa idara mbalimbali kushikamana kuleta maendeleo katika Sekta ya Elimu.

Mtamwa alisema suala la elimu siyo la upande mmoja wa wakuu wa walimu, bali linahitaji ushirikiano kuanzia ngazi ya familia hadi kwa wanasiasa.

Mmoja wa wazazi, Joyce Nyamanga, aliiomba serikali kutowafumbia walimu wakuu ambao wamekuwa wakikaidi maelekezo yanayotolewa na viongozi wa ngazi za kuu kuhusu suala la kuwafukuza wanafunzi shuleni.

Alisema bado kuna baadhi ya shule za sekondari wanafunzi wanaendelea kunyanyasika kwa kufukuzwa na walimu bila kujali athari zitakazojitokeza.

# RC aagiza uchunguzi vifo wanafunzi watatu

**Na Ibrahim Joseph,** MPWAPWA

MKUU wa Mkoa wa Dodoma ameliagiza Jeshi la Polisi mkoani humo kufanya uchunguzi wa kina kuhusu tukio la vifo vya wanafunzi watatu wa Shule ya Msingi Mbori wilayani Mpwapwa.

Wanafunzi hao walifariki dunia juzi baada ya kufukiwa na kifusi walipokwenda kuchota mchanga waliodaiwa kuagizwa na walimu wao. Miili yao ilizikwa jana.

Anthony Mtaka alisema jana kuwa polisi wanatakiwa kufanya uchunguzi wa kina kubaini ukweli wa madai ya kuwapo kwa uzembe wowote uliofanywa na walimu wanaodaiwa kuwatuma wanafunzi hao mchanga.

Alipiga marufuku shughuli za kuchimba mchanga eneo hilo, huku akiwataka wananchi kuwa watulivu wakati serikali ikichukua hatua kuhusu tukio hilo.

Juzi, Mkuu wa Wilaya ya Mpwapwa, Josephat Maganga, alisema katika tukio hilo wanafunzi wengine watano walijeruhiwa.

Maganga alisema tukio hilo lilitokea saa tatu asubuhi na limeacha maswali mengi ya kujiuliza.

Aliwataja wanafunzi waliofariki kuwa ni Rehema Alex aliyekuwa anasoma darasa la nne; Daudi Machea wa darasa la tano; na Ezla Lucas wa darasa la sita. Waliojeruhiwa ni: Arafa Athumani (10); Nelly Daudi (12); Wilsoni Amosi; Yunis Mussa (12); na Mwijuma Machimo (13).

"Kuna maswali ya kujiuliza walienda peke yao? Nani aliwatuma? Je, ilikuwa ni wakati wa vipindi vya darasani? Kuwatuma mchanga kwenye mto na kokoto tumepiga marufuku," alisema.

Alibainisha kuwa kazi za maendeleo kwa maelekezo ya serikali zimeachwa kwa wazazi ndiyo watakaa na kupanga wenyewe.

Alisema uchunguzi unafanyika na wote waliosababisha tukio hilo watachukuliwa hatua.

Wakizungumzia tukio hilo, Mkazi wa Mbori, Daudi Ngumbi, alisema wazazi wamekuwa wakitwa kwenye shughuli mbalimbali za maendeleo ya shule na wiki mbili zilizopita shule hiyo inasadikiwa kupokea fedha za mradi wa ujenzi vyoo.

"Kama kulikuwa na changamoto ya kutotosha vifaa vya ujenzi, wazazi tulipaswa kushirikishwa ili kukamilisha sehemu pungufu lakini kama kuna shughuli za aina hiyo, walimu walipaswa kwenda na wanafunzi kwa ajili ya uangalizi," alisema.

Mariam Isaya, mkazi mwingine wa eneo hilo, alisema wazazi wanaamini walimu ni walezi na wanapotoa majukumu, wajiridhishe usalama wa eneo ili yasitokee madhara ya aina hiyo.



Waziri wa Nishati, Dk. Medadi Kalemani akizungumza na wananchi wa Kijiji cha Machenje, wilayani Kongwa, mkoani Dodoma alipofanya ziara ya kutembelea eneo litakapojengwa mradi wa kupoza umeme. Kulia ni Mbunge wa jimbo hilo na Spika wa Bunge, Job Ndugai. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Ahadi ya Rais Samia kutekelezwa Kongwa

**Na Ibrahim Joseph,** KONGWA

SERIKALI inatarajia kuanza ujenzi wa mradi wa kituo cha kupooza umeme katika eneo la Kongwa ili kuongeza umeme kwenye miji iliyo jirani na eneo hilo.

Waziri wa Nishati, Dk. Medard Kalemani, aliyasema hayo wakati wa ziara yake juzi kukagua eneo litakapojengwa na kuwekwa mitambo katika Kijiji cha Machenje wilayani humo.

Dk. Kalemani alisema lengo la serikali ni kuongeza nguvu ya umeme kwenye miji iliyopo jirani na eneo hilo na ujenzi utagharimu zaidi ya Sh. bilioni 41.2 na unatarajiwa kuanza mwanzoni mwa Septemba mwaka huu.

Alisema serikali imesikia kilio cha wananchi kulalamika kuhusu tatizo la kukatika katika kwa umeme kwenye miji jirani iliyopo maeneo hayo, hivyo ujenzi huo utaondoa tatizo hilo. Aliyataja maeneo yatakayonufaika na mradi huo kuwa ni Wilaya ya Gairo, Kiteto, Mpwapwa na Kongwa ambayo kwa utaratibu wa Shirika la Umeme (TANESCO) yako Mkoa wa kiTANESCO Dodoma.

Alisema ili kutatua tatizo hilo kwa haraka, serikali itafunga kifaa kiitwacho AVR ambacho kimehamishwa kutoka mkoani Ruvuma na kupelekwa wilayani Kongwa kwenye mji mdogo wa Mbande.

Aliongeza kuwa serikali imeshaandaa eneo la ekari 130 kwa ajili ya ujenzi wa mradi huo na fedha kiasi cha Sh. milioni 36.4 zimetengwa kwa ajili ya kulipa fidia kwa wananchi waliochukuliwa maeneo yao.

Waziri huyo alisema katika kukabiliana na ongezeko la watu katika Mji wa Dodoma, TANESCO wameongeza umeme kutoka megawati 48 za awali hadi 448 na mwisho wa mwaka huu wanatarajia kuongeza megawati 200 ambazo zitafikisha jumla ya megawati 648.

Spika wa Bunge na Mbunge wa Kongwa, Job Ndugai, alisema wilaya hiyo inakabiliwa na tatizo la kukatika kwa umeme mara kwa mara kunakokwamisha shughuli za uzalishaji.

Ndugai alisema uwapo la tatizo hilo umesababisha wenye viwanda kushindwa kuzalisha kwa malengo yaliyokudiwa na kuwakosesha weyeji ajira.

"Na hapa niseme Mheshimiwa Waziri, siyo kwamba Kongwa hakuna wasichana wazuri wanaoweza kushinda mashindano ya urembo nchini, hapana!

"Inawezekana kukosekana kwa umeme kumechangia Kongwa kukosa taji la washindi wa Miss Tanzania," alisema.

Upatikanaji wa umeme wa uhakika wilayani Kongwa ni ahadi iliyotolewa na Rais Samia Suluhu Hassan hivi karibuni alipokuwa njiani kwa ziara ya kikazi mkoani Morogoro.





# Wastaafu wapewa mbinu matumizi ya mafao yao

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WASTAAFU mkoani Mbeya wameshauriwa kuzitumia fedha za mafao kuanzisha biashara zenye tija ikiwamo kufungua viwanda vidogo badala ya kuzitumia kuhonga, vitendo ambavyo vinadaiwa kuwafilisi na kugharimu maisha yao.

Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, alitoa ushauri huo juzi jijini Mbeya alipokuwa anafungua mafunzo maalum kwa watumishi wa umma wanaotarajiwa kustaafu ambayo yaliandaliwa na Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma (PSSSF).

Mafunzo hayo yalilenga kutoa elimu ya uwekezaji kwa wastaafu watarajiwa ambayo pia yalihudhuriwa na maofisa kutoka katika taasisi mbalimbali zikiwamo taasisi za kifedha pamoja na wataalamu wa elimu ya ujasiriamali.

Homera alisema baadhi ya wastaafu wamekuwa wakizitumia fedha za mafao kuhonga mabinti wadogo, hali ambayo inawasababishai kuibiwa fedha zao na wakati mwingine kuuawa na mabinti hao kwenye nyumba za kulala wageni.

"Nawaomba sana wazee wangu hizi fedha ni kwa ajili yako na familia yako, sasa kuna mabinti huko nje akijua umepata mafao anaanza kujipitisha akiwa amevaa sketi fupi ili uingiwe na tamaa na ukithubutu ndio umekwisha, anakufanya vya kukufanya halafu unapokoroma anahamisha fedha zao zote," alisema Homera na kuongeza:

"Lakini mama zangu nanyi jitahidini sana, wapo wengine wakishapata fedha wanatafuta kijana mdogo na unakuta asubuhi kijana anasalimia 'shikamoo' kumbe walilala wote, nawaomba sana hayo mambo yapo ila jiepusheni nayo."

Aliwataka kusikiliza vizuri maelezo ya uwekezaji wanayopewa na wataalamu ili wakawekeze fedha hizo kwa tija badala ya kuzitawanya kwenye vitu visivyokuwa na maana.

Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa PSSSF, Fortunatus Magambo, alisema wameandaa mafunzo hayo kwa ajili ya wastaafu watarajiwa nchi nzima ili kuwaandaa wasizitumie vibaya fedha zao za mafao na badala yake wawe wanazitumia kwenye maendeleo.

Alisema kwa kuanzia wanatoa mafunzo hayo katika mikoa 11, na kwamba Mbeya umekuwa mkoa wa tano ambako alisema watawafikia wastaafu watarajiwa 8,000 na kwamba zoezi hilo ni endelevu na litakuwa linafanyika kila mwaka.

Alisema ni jukumu la mfuko huo kushirikiana na serikali kuwaandaa wastaafu hao ili kuhakikisha wanakuwa na maisha mazuri, baada ya kustaafu kwa kuwa na miradi endelevu badala ya kuanzisha biashara ambazo hazina tija.

"Hawa watu wamelitumikia taifa kwa muda mrefu na kwa mafanikio makubwa, kwa hiyo lazima tuwaandae maana unakuta mtu anastaafu hajui cha kutumia fedha zake, anaishia kutapeliwa na kupata presha anakufa," alisema Magambo.

Baadhi ya wastaafu watarajiwa waliushukuru uongozi wa PSSSF kwa kuanzisha mafunzo hayo wakidai kuwa yatawasaidia kuzitumia fedha zao kwa usahihi ili ziwasaidie kwa muda mrefu.

Thomas Urembo ambaye ni mfanyakazi wa Chuo cha Ufundi Stadi (VETA) tawi la Mbeya, alisema amebakiza miezi minne kustaafu na hivyo akadai mafunzo hayo yamekuja muda mwafaka.

Alisema wanafundishwa vitu vingi vya ujasiriamali ili kila mmoja akachague mwenyewe kitu cha kwenda kufanya kulingana na fedha atakazokuwa amepata.



Naibu Spika, Dk. Tulia Ackson (kulia), akimkabidhi mmoja wa viongozi wa serikali za mitaa wa Jiji la Mbeya, vifaa kwa ajili ya ulinzi shirikishi ambavyo ni tochi 400, filimbi 400 na betri 800, vilivyotolewa na mdau wa maendeleo, Raphael Ndelwa (kushoto), jijini humo jana. **PICHA: NEBART MSOKWA**

## Wachimbaji walalamikia gharama kubwa za vibali

**Na Grace Mwakalinga,** CHUNYA

WACHIMBAJI wa madini katika Wilaya ya Chunya, wamelalamikia gharama kubwa ya upatikanaji wa vibali vya matumizi ya vilipuzi, wakidai hulazimika kufuata huduma hiyo jijini Dodoma na kuwagharimu fedha nyingi.

Kutokana na adha ya kusafiri hadi jijini Dodoma kufuata kibali kwa ajili ya matumizi ya vilipuzi maarufu kama baruti kwa ajili ya shughuli za uchimbaji wa madini wilayani Chunya, wameiomba serikali kuwasogezea huduma hiyo karibu.

Thomas Munis, alisema hutumia gharama hadi shilingi 240,000 kwa ajili ya kupata leseni ya vilipuzi, na kwamba hutumia muda hadi wa wiki mbili kupata kibali.

"Tunatumia gharama kubwa hadi kwenda ofisi za madini makao makuu Dodoma kupata kibali cha vilipuzi kwa ajili ya shughuli zetu za madini... licha ya kutumia fedha nyingi, pia tunatumia zaidi ya wiki moja, huku shughuli za uchimbaji zikisimama tunaomba msaada serikali itusaidia kusogeza huduma karibu," alisema Munis.

Mbunge wa Lupa, Masache Kasaka, alisema mara kadhaa amekuwa akizungumza na wachimbaji hao na kwamba kilio chao ni kusogeza huduma ya utoaji leseni ya vilipuzi wilayani humo.

Alisema amelifikisha suala hilo kwa Waziri wa Madini, Dotto Biteko, na kwamba kinachosubiriwa ni utekelezaji.

Aidha Mkuu wa Wilaya ya Chunya, Mayeka Simon, alieleza hatua zilizochukuliwa kuwa ni pamoja na kuandika mapendekezo kwa ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Mbeya ili kusogeza huduma hiyo karibu na wachimbaji.

# Wakulima pareto waonywa mawakala vishoka

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

WAKULIMA wa zao la pareto katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya wametahadharishwa kujiepusha na mawakala feki 'vishoka' ambao wananunua zao hilo kwa wakulima kisha kuliuza bila kujali ubora hivyo kusababisha kushuka thamani kiwandani.

Tahadhari hiyo ilitolewa jana na mratibu wa huduma za ugani kutoka Kampuni ya Pareto nchini (PCT), Michael Bishubo, wakati kampuni hiyo ilipotembelea baadhi ya miradi ya ujenzi wa shule, zahanati na daraja na kutoa msaada wa vitu mbalimbali katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya.

Bishubo alisema wapo baadhi ya watu 'vishoka' ambao wanawafuata wakulima shambani kisha kununua zao la pareto kwa Sh. 2,700 kwa kilo na kisha wao kwenda kuiuza kwa wakala bei hiyo hiyo.

"Vishoka wananunua bei hiyo hiyo na wao wanaenda kwa mawakala wetu kuuza bei hiyo kwa kilo sasa unajiuliza kuwa wanapata faida gani, lakini ukiangalia wanauza pareto ambayo haina ubora, ina mawe na takataka nyingine ambazo zinaongeza uzito kwenye mizani."

"Lakini kwa kuwa mawakala wetu wanalipwa kwa kamisheni wakishapekelewa kwenye vituo vyao wanachukua mzigo kama ulivyo bila kujua kuwa umechakachuliwa hali ambayo inaleta usumbufu kiwandani," alisema.

Akizungumzia msaada, alisema kampuni ya PCT ni sehemu ya jamii kwa kuwa inafanya kazi na watu, hivyo imeamua kushirikiana na wanakijiji katika ujenzi wa vyoo vya Shule ya Msingi Itaga, Zahati ya Pashungu na ujenzi wa daraja la Izumbwe Two kwa kutoa mifuko ya saruji, mabati na fedha tasilimu.

Mkurugenzi wa PCT, John Power, alisema kampuni hiyo itaendelea kushirikiana na jamii katika masuala mbalimbali ya maendeleo hususani katika maeneo zinakofanyika shughuli za kilimo cha pareto.

Power alisema kampuni yake iko tayari kuongeza bei ya pareto kutoka Sh. 2,700 hadi kufikia Sh. 3,000 ikiwa wakulima wataongeza thamani ya zao hilo kuzalisha lenye ubora na linalofuata hatua muhimu za kilimo hicho.

Diwani wa Itawa, Elia Mwampamba, alisema PCT imekuwa ikishirikiana na jamii katika maeneo yote wanayozalisha zao la pareto na kwamba wataendelea kushirikiana nao katika masuala mbalimbali.

Msaada huo utasaidia kukamilisha ujenzi wa vyoo vya shule ya msingi Itaga, Zahanati ya Pashungu na ujenzi wa daraja la Mzumbwe Two lililobomoka kutokana na mvua za msimu uliopita.



# Wauguzi, wakunga wamkwaza waziri

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto, Nassor Ahmed Mazrui, amesema bado haridhishwi na huduma zinazotolewa na baadhi ya wakunga na wauguzi katika hospitali za serikali.

Alisema baadhi yao wamekuwa na kauli zisizoridhisha kwa wagonjwa wanaofika hospitalini kupata huduma za afya hasa wajawazito wanaosubiri kujifungua.

Aliyasema hayo juzi mbele ya wauguzi na wakunga katika kongamano la kutathmini kazi za wataalamu wa fani hizo Zanzibar, lililofanyika katika ukumbi wa Sheikh Idrisa Abdulwakil, Kikwajuni mjini Unguja.

Mazrui alisema ameshapokea malalamiko mengi kutoka kwa wajawazito wanaofika kujifungua katika Hospitali ya Mnazimmoja na Mwembe Ladu kuwa hutolewa maneno ya kashfa na kejeli.

"Mimi mwenyewe nilifanya utafiti mdogo wa kuwahoji wajawazito kama wanapendelea kuzalishwa na wakunga wa kiume au wa kike. Nilishangazwa sana kuwasikia wakisema wanapenda kuzalishwa na wakunga wanaume kuliko wanawake kwa sababu wakunga wanawake huwanyanyasa na kuwatolea maneno ya kashfa lakini wa kiume huwahudumia vizuri huku wakiwabembeleza," alisema.

Waziri huyo alisema zipo kesi za udhalilishaji zinazofanywa na baadhi ya wakunga wakati wa kinamama wanapojifungua hasa kwa watoto wenye uzito mkubwa ambao huwavuta viungo vyao ili watoke haraka na kuwasababishia ulemavu. "Ninazo kesi hizo za watoto wachanga kusababishiwa ulemavu wa makusudi kwa kuwavuta mikono wakati wanapozaliwa na wengine kuvuja damu katika vitovu vyao kutokana na kuvutwa. Huu ni udhalilishaji," aliongeza.

Waziri Mazrui alitumia fursa hiyo kuwataka wahudumu na wakunga kutumia lugha nzuri na kuacha kutumia lugha zisizofaa kwa wajawazito wanaofika hospitalini kujifungua.

Alisisitiza kuwa ni lazima tathmini ifanyike juu ya njia bora ya kuokoa maisha ya watoto na si kuwasababishia vifo au ulemavu.

Waziri huyo aliwataka wauguzi na wakunga kufuata maadili na sheria za kazi zao katika kutekeleza majukumu yao ili kutoa huduma bora kwa wananchi wanaofuata matibabu. Alisema ni vyema kila muuguzi na mkunga kutathmini utendaji wake ili kwenda sambamba na maadili ya kazi yake na mafunzo aliyopewa chuoni.

Mazrui alisema ni lazima kila mwanajamii apewe huduma zinazostahiki anapofika hospitalini na kuacha kumtendea kinyume cha maadili ili kuepusha malalamiko kwa wananchi.

"Muuguzi anatakiwa kufanya kazi kwa moyo wa huruma na upendo na anatakiwa aipende kazi yake ili kuokoa maisha ya watu. Tuwe wauguzi bora. Rais wetu ni daktari, hivyo ni lazima na sisi twende kidaktari kwa manufaa ya wananchi," alisema waziri.

Nao wauguzi na wakunga walioshiriki kongamano hilo, walisema watayafanyia kazi maelezo aliyoyatoa waziri lakini wakaomba kutatuliwa changamoto zinazowabili na kupewa nafasi ya kujieleza pale wanapotuhumiwa kufanya makosa na si kuchukuliwa hatua za kusimamishwa kazi bila kusikilizwa.

Kongamano hilo pia lilihudhuriwa na viongozi mbalimbali wa hospitali binafsi pamoja na walimu mbalimbali wa vyuo vikuu nchini.

## Kampuni kujenga nyumba za makazi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

KUTOKANA na mwingiliano mkubwa wa uhusiano wa kindugu kati ya Oman na Zanzibar, kampuni ya Muriya yenye makao makuu yake Oman inakusudia kujenga majengo ya makazi ambayo yatawawezesha wananchi na wafanyabiashara kutoka Zanzibar kuishi na kufanya shughuli zao wanapokuwa huko.

Meneja wa kampuni hiyo, Ghiziane El Gouchi, alisema hayo jana alipozungumza na waandishi wa habari katika Hoteli ya Verde akiutambulisha mradi huo Zanzibar.

Alisema hizo ni fursa zinazopatikana na kampuni hiyo ambazo zitasaidia shughuli za kiuchumi na uwekezaji kwa wafanyabiashara wa Zanzibar wanapokuwa Omna kwa shughuli za kibiashara.

Kampuni ya Muriya, alisema imekamilisha mradi wa maendeleo ya majengo ya makazi katika miji ya Jebel Sifah na Hawana Salala ambayo yamezinduliwa yakiwa miongoni mwa sehemu za kivutio kwa wageni.

Alisema kuwapo kwa nyumba za makazi katika miji hiyo inatoa fursa kwa wageni katika nchi mbalimbali kuishi Oman na kufanya shughuli za kibiashara bila matatizo.

"Ndiyo maana hizi fursa tumezileta Tanzania ikiwamo Zanzibar kwa kuzingatia uhusiano wa kindugu uliopo na mwingiliano wa wananchi wa pande mbili za kutembeleana mara kwa mara na kufanya biashara," alisema.

El Gouchi alisema bayana kwamba serikali ya Oman nia yake ni kufungua milango ya fursa za uwekezaji wa aina mbalimbali zikiwamo biashara na utalii.

"Oman kuna wananchi wengi kutoka Tanzania hasa Zanzibar, hivyo mradi huu utakuwa nafuu kwao kununua nyumba kwa ajili ya makazi au biashara," alisema.




Meneja wa Kampuni ya Muriya Estate ya Oman, Ghiziane El Gouchi (kushoto), akizungumza na waandishi wa habari jijini Zanzibar jana, wakati akitambulisha mradi wa ujenzi wa nyumba za makazi ambazo zitajengwa Oman, kwa ajili ya kuwasaidia wananchi mbalimbali ikiwamo Wazanzibari ambao wengi wao wapo nchini humo. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

## Masoud aahidi kuirejeshea hadhi Zanzibar

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MAKAMU wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, Masoud Othman Masoud, amesema ofisi yake iko tayari kushirikiana na Ofisi ya Meya wa Jiji la Zanzibar ili kuirudishia Zanzibar hadhi yake.

Aliyasema hayo jana alipokutana na Meya wa Jiji, Mahmoud Mohamed Mussa, pamoja na ujumbe wake uliofika ofisini kwake, Migombani mjini Unguja.

Othman alisema watu kutoka maeneo mbalimbali yakiwamo ya Afrika ya Magharibi walikuwa wakija Zanzibar kwa lengo la kujifunza namna ya kupanga mji, lakini kwa bahati mbaya sana kwa sasa Zanzibar imepoteza sifa hiyo. "Tuko tayari na tutaungana nanyi si tu katika kuweka mazingira ya Jiji la Zanzibar kuwa safi bali tutatoa msaada zaidi hata kuirudisha Zanzibar katika uzuri na haiba yake," alisema.

Naye Meya wa Jiji la Zanzibar, Mahmoud Mohamed, alimshukuru Makamu wa Kwanza kwa nasaha zake pamoja na kuahidi kutumia vyema fursa ya ushirikiano kutoka katika ofisi ya Makamu wa Kwanza ili kufikia malengo ya Rais wa Zanzibar, Dk. Husein Ali Mwinyi, ya kuufanya mji wa Zanzibar kuwa safi kwa kiwango kinachotakiwa.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, Dk. Saada Mkuya, alisema ujio wa meya huyo umeonyesha mustakbali mwema kuelekea katika ushirikiano na idara zake jambo ambalo litaifanya Zanzibar kuwapo katika mwenokano bora.

Mkuya aliwataka watendaji wa masuala ya mazingira na mabaraza ya miji kukaa pamoja na kuandaa mpango utakaowawezesha kupata fedha wa kutafuta nyenzo za kufanyia kazi ili mji kuwa katika hali ya usafi.

Akizungumza na watendaji hao pamoja na ujumbe wa watendaji wa baraza la jiji juu ya kutafuta namna bora ya kuimarisha usafi wa mji, alisema mpango huo uhusishe zaidi upatikanaji wa vitendea kazi pamoja na kuwajengea uwezo kitaaluma.

Alisema kwa sasa kuna umuhimu wa wadau hao kufanya kazi kwa pamoja ili kuona maagizo ya viongozi juu ya kuweka mazingira safi katika maeneo yote ya miji yanaimarika hivyo katika kufikia hatua hiyo kunahitajika mipango mbalimbali ikiwamo fedha na vitendea kazi stahiki kwa ajili ya kuimarisha eneo kuu la kutupia taka.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI INDUSTIAL AREA, PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 0782253676

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA WILAYA**
**KINONDONI**

**SHAURI LA MIRATHI NA. 143 LA 2021**

**Maombi ya barua ya usimamizi wa mirathi ya marehemu MMUNI...................MAREHEMU**

**NA**

**ANASTASIA VALENT MMUNI...........................MWOMBAJI**
**FARAJA ALOIS KONRAD MMUNI**

**TAARIFA YA KAWAIDA**
**(Kanuni ya 75)**

Watu wote wanaodai kuwa na haki ya marehemu aliyetajwa hapo juu wanafahamishwa kufika na kuangalia shauri hili katika jalada kama wanaona inafaa kabla ya kutolewa kwa uthibitisho wa barua ya usimamizi wa mirathi kwa mwombaji hapo juu.
Mapingamizi yoyote kuhusu maombi haya yawe yameandikishwa mnamo au kabla ya tarehe 19 Mwezi wa 8 mwaka 2021.

**Hati hii imetolewa tarehe 16 Mwezi wa 7 Mwaka 2021.**

HAKIMU MKAZI
MAHAKAMA YA WILAYA
KINONDONI
RESIDENT MAGISTRATE KINONDONI DISTRICT COURT DAR ES SALAAM

116377502

---

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**BONIPHACE ANYABWILE KAMBAGA** ANATANGAZA KUPOTEA KWA KADI YAKE YA GARI YENYE NAMBA ZA USAJILI **T 222 DMU – TOYOTA ALPHARD.** CHASSIS NAMBA **MNH100018486.** ENGINE NAMBA 1MZ1505311. YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI. TAARIFA YA POLISI: **DAR/MSI/RB/371257/2021.**

116377702

---

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**NGUSSA SANANGA MAKUNDE** Anatangaza kupotelewa na kadi ya Bajaji yenye namba za usajili **MC.664 CHJ.** Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo cha polisi kilichopo jirani yake.Taarifa ya jeshi la polisi, **KAH/RB/TR/4752/2021.**

116379802

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

## HATI YA KIAPO

Mimi **SAA MBWANA ZUMO wa S.L.P TANGA,** nikiwa na akili timamu nimefika mbele ya Hakimu/Wakili na kutamka yafuatayo:-

1. Kwamba mimi ni mwanafunzi ambaye nimemaliza Elimu yangu ya Sekondari mnamo 2007, katika shule ya Sekondari Japan-Tanga.
2. Kwamba baada ya kumaliza nilipewa cheti cha taaluma cha kidato cha Nne ambacho kina namba ya Mtahiniwa S.01323/0043.
3. Kwamba CHETI hicho kimepotea nimefanya jitihada kukitafuta bila ya mafanikio.
4. Kwamba kwa kiapo hiki ifahamike kwa mtu/taasisi yeyote kuwa cheti change kimepotea.
5. Kwamba nawasilisha taarifa hii ya upotevu kwenye mamlaka ya Jeshi la Polisi nikiomba hati ya upotevu wake Loss Report **TAN/RB/461639/2020.**

**UTHIBITISHO:**
Ninathibitisha kuwa yote niliyotamka hapo juu ni kweli tupu kadri nijuavyo kwa sheria ya viapo.

Leo hii tarehe 17 Juni, 2020
**MBELE YA...Jovine Bishanga**
**CHEO...Hakimu Mkazi**
RESIDENT MAGISTRATE

116378602

---

**SHERIA YA UMILIKI WA ARDHI YA MWAKA 1999**
**(SURA YA 113)**

**KUHAMISHA KWA BARUA YA TOLEO YA KUMILIKI ARDHI**

**MMILIKI ALIYEANDIKISHWA :HAMADI KULELE**

**KWENDA KWA :MICHAEL MASOTA**

**ARDHI:KIWANJA NA(4) KWA SASA NI NAMBA 434 KITALU J ENEO LA MBAGALA MANISPAA YA TEMEKE JIJINI DAR ES SALAAM**

Taarifa inatolewa kwamba **AFISA ARDHI MTEULE** anakusudia kuhamisha **BARUA YA TOLEO TAJWA YA KUMILIKI ARDHI** kwenda kwa **MICHAEL MASOTA** aliyewasilisha barua ya toleo pamoja na mkataba wa manunuzi kwamba ameuziwa kiwanja hicho,ikiwa kwa jina la **HAMADI KULELE. NINAKUSUDIA KUTOA** hati miliki **IWAPO HAKUNA PINGAMIZI LITAKALOTOLEWA KWA MUDA WA SIKU 30 TANGU TAREHE YA TAARIFA HII ITAKAPOTANGAZWA KATIKA GAZETI.**

116378002

---

## MNADA WA HADHARA

Kwa idhini tuliyopewa na **TUJIJENGE TANZANIA LTD**, MM Auctionees & Debt Collectors Co. Ltd tutauza kwa mnada wa hadhara Mali za wadaiwa Sugu kama ilivyotangazwa kwenye gazeti

| Mthamini/ Mdaiwa | Dhamana | Mahali Ilipo | Tarehe ya mnada |
|---|---|---|---|
| Waven Esron Mrikaria/Marco Esrom Mrikaria | Kiwanja/Nyumba haijaisha | Mtaa wa Ndofe - Igoma | 13/08/2021 |
| Julieth Sifuel Kowelo | Kiwanja/Nyumba haijaisha | Mtaa wa Majengo Nyegezi | 14/08/2021 |

**Masharti ya mnada**
Minada itafanyika mahali dhamana zilipo kuanzia saa nne asubuhi.
Mteja atalipa 25% siku ya mnada, 75% atalipa ndani ya siku 14 akishindwa kulipa 25% hairudishwi. Gharama za kubadili umiliki ni juu ya mnunuzi.

**Mawasiliano piga:-**
**MM Auctioneers –**
**0710784784456/0768990064**

116379002

---

## MNADA WA HADHARA

Kwa idhini tuliyopewa na **TUJIJENGE TANZANIA LTD, Dalali tajwa hapo chini** tutauza kwa mnada wa hadhara Mali za mdaiwa Sugu Ismail Abdallah Magari kama ilivyotangazwa kwenye gazeti;-

| Mdaiwa/ mdhamini | Dalali | Aina ya Mali | Tarehe ya mnada - Mahali |
|---|---|---|---|
| Ismail Abdallah Magari | MM AUCTIONEER & DEBT COLLECTOR | Toyota Coaster T 915 BXN | 12.08.2021 Mwanza Yard |
| Ismail Abdallah Magari | MM AUCTIONEER AND DEBT COLLECTOR | Toyota Coaster T 628 DRU | 12/08/2021 Mwanza Yard |

Minada yote itafanyika mahali dhamana zilipo kuanzia saa nne asubuhi. Mteja atalipa 25% siku ya mnada, 75% atalipa ndani ya siku 14 akishindwa kulipa 25% hairudishwi. Gharama za kubadili umiliki ni juu ya mnunuzi.

**Mawasiliano piga:**
**MM A/MART:-**
**0710784784456/0768990064**

116379002

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA**
**WILAYA YA MOROGORO**
**LILILOPO MOROGORO**
**MAOMBI NO 45 YA 2021**

**ABRAHAMU TERRY MJEMA ..........................MWOMBAJI**

**DHIDI YA**

**BENEDICT JOSEPH**
**PETER REUBENI RITE ..........................WAJIBU MAOMBI**

**WITO/KUITWA SHAURINI KWA**

**PETER REUBENI RITE**

Popote ulipo unaarifiwa ufike katika Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya ya Morogoro tarehe 23/08/2021 mbele ya M wenyekiti E. Mogasa wewe mwenyewe binafsi au utume muwakilishi wako bila kukosa ambapo maombi yamepangwa kutajwa. Endapo hautahudhuria maombi yatatajwa na kusikilizwa upande mmoja dhidi yako na kutolewa uamuzi.
Imetolewa kwa mkono wangu na muhuri wa Baraza leo tarehe 27 mwezi Julai 2021.

MWENYEKITI
BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA (W)
MOROGORO.

116379802

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA WILAYA**
**KINONDONI**

**SHAURI LA MIRATHI NA. 142 LA 2021**

**Maombi ya barua ya usimamizi wa mirathi ya ASSUMPTA CHINGUWILE...................MAREHEMU**

**NA**

**FARAJA ALOIS KONRAD MMUNI**
**ALLICE CHINGUWILE.......................................WAOMBAJI**

**TAARIFA YA KAWAIDA**
**(Kanuni ya 75)**

Watu wote wanaodai kuwa na haki ya marehemu aliyetajwa hapo juu wanafahamishwa kufika na kuangalia shauri hili katika jalada kama wanaona inafaa kabla ya kutolewa kwa uthibitisho wa barua ya usimamizi wa mirathi kwa mwombaji hapo juu.
Mapingamizi yoyote kuhusu maombi haya yawe yameandikishwa mnamo au kabla ya tarehe 05 Mwezi wa 08 mwaka 2021.
**Hati hii imetolewa tarehe 27 Mwezi wa 07 Mwaka 2021.**

HAKIMU MKAZI
MAHAKAMA YA WILAYA
KINONDONI
RESIDENT MAGISTRATE KINONDONI DISTRICT COURT DAR ES SALAAM

116377602

---

**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

## HATI YA KIAPO

Mimi **RAMADHANI ALMASI JUMA** WA S.L.P 178 TANGA NIKIWA MTU MZIMA NA AKILI ZANGU TIMAMU NAAPA NA KUTHIBITISHA MBELE YA HAKIMU MAHAKAMANI KAMA IFUATAVYO

1. KWAMBA MIMI RAMADHANI ALMASI JUMA NI MMILIKI WA GARI YENYE NAMBA T .243 BJG
2. KWAMBA KADI YA GARI HILO IMEPOTEA NA NIMEITAFUTA PASIPO MAFANIKIO YA KUIPATA TENA NIMEFIKA POLISI NA KUTOA TAARIFA TNG/RB/636/2021
3. KWAMBA KWA KIAPO HIKI NADHIBITISHA KUWA MIMI NI MMILIKI HALALI WA GARI NAMBA T .243 BJG ABAYO KADI YAKE IMEPOTEA

**UTHIBITISHO**
MIMI RAMADHANI AL MASI JUMA NATHIBITISHA KUWA YOTE NILIYO SEMA HAPA JUU KUANZIA AYA YA 1-3 NI KWELI TUPU KWA JINSI NIJUAVYO NA KWA MUJIBU WA SHERIA YA VIAPO (THE OATH AND STATUTORY DECLARATION ACT.CAP.34 R; E 2002

Imethibitishwa hapo Tanga
sahihi ya muapaji

116380502

---

## IMARA BRAKE LININGS TABATA DAMPO

**MALI MPYA IMEWASILI.**

**Gundi (Bostik) kwa Sh. 130,000/- Kwa ujazo wa lita 5.**

**Wasiliana nasi kwa simu namba 0783 277 909; 0714 475 898.**

116367002

---

***NJOO UTANGAZE BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU SANA***

**Kwa Habari Motomoto**

usikose Gazeti lako

la Nipashe kila siku

Tupigie

0782253676

Nipashe
MWANGA WA JAMII

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji
THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

HABARI KITAIFA

# 'Samaki waliozagaa Bahari ya Hindi hawakufa kwa sumu'

**Na Elizabeth Zaya**

UCHUNGUZI umebaini vifo vya samaki vilivyotokea katika ufukwe wa Bahari ya Hindi Julai 21, mwaka huu jijini Dar es Salaam, havikutokana na sumu.

Kwa mujibu wa taarifa ya matokeo ya uchunguzi wa vifo vya samaki hao iliyotolewa jana na Wizara ya Mifugo na Uvuvi, walikufa kwa kukosa hewa.

"Julai 21, mwaka huu, kulikuwa na tukio la vifo vya samaki ambao walionekana wakiwa wamezagaa katika ufukwe uliopo kati ya hospitali ya Ocean Road na Aghakhan, Dar es Salaam."

"Pamoja na hatua zilizochukuliwa za kuzuia wananchi kuchukua samaki hao kama kitoweo na kuzuia uingizaji wake katika soko la Magogoni Feri, sampuli za samaki hao zilichukuliwa kwa ajili ya uchunguzi wa kimaabara na kilogramu 156 zilibaki kuteketezwa na Ofisa Uvuvi Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam ili kubaini chanzo cha vifo vya samaki hao."

Taarifa ya uchunguzi huo kwa vyombo vya habari ilitolewa na Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano wa Wizara hiyo, Edward Kondela.

"Uchunguzi ulifanyika katika maeneo makuu matatu. Moja ni katika utambuzi wa aina za samaki waliokufa, ukubwa wao, aina ya vyakula ndani ya matumbo na muonekano wa hali ya nje ya samaki ambao ulifanyika kwenye maabara ya Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi Tanzania (TAFIRI)," alisema Kondela katika taarifa yake hiyo.

"Uchunguzi wa pili ulikuwa ni wa maji kuangalia vimelea vyenye sumu ambao ulifanywa kwenye Maabara ya Taifa ya Uvuvi, Dar es Salaam na uchunguzi wa tatu ulikuwa kuangalia viuatilifu, sumu zitokanazo na mimea na kemikali nyingine za viwandani ambao ulifanyika katika Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali."

Alisema uchuguzi huo ulihusisha aina tisa za samaki ikiwamo kui, mkizi, janja, tambanji, chaa, kuku bahari, kolekole pandu, kaa, kambamiti na kambakochi.

Alisema samaki jamii ya kui ilichukua sehemu kubwa ya samaki hao kwa asilimia 36 ikifuatiwa na jamii ya mkizi iliyokuwa na asilimia 29 ambao hupatikana kwenye kina kifupi cha maji na kwamba wengi wa samaki hao walikuwa wachanga. Alisema uchunguzi umebaini kwamba sehemu kubwa ya matumbo ya samaki hayakuwa na chakula, japokuwa samaki aina ya kui, mkizi na tambanji ndio walikutwa na dagaa, kaa na uduvi katika matumbo yao.

"Samaki waliochunguzwa walikuwa na hali nzuri, ngozi haikutatuka na ilikuwa na rangi angavu, huku macho yao yalionekana meusi na angavu, na mapezi yalikuwa angavu bila utelezi, walikuwa na nyama imara na hakukuwa na harufu mbaya," alisema Kondela.

"Hali hii inaondoa uwezekano kuwa vifo hivi vinaweza kuwa vimetokana na sumu au vilipuzi. Hata hivyo, samaki wengi walionekana kuwa na midomo wazi kuashiria kuwa walikosa hewa au walikufa wakitafuta hewa. Uchunguzi wa sampuli za maji yaliyochukuliwa katika eneo haukubaini vimeamaji vinavyohusishwa na sumu."

"Uchunguzi wa matumbo ya samaki haukubaini uwapo wa vimeamaji hivi hali inayoondoa uwezekano wa kuwa samaki hao walikufa kutokana na sumu itokanayo na vimeamaji hivyo."

Pia, alisema kwamba uchunguzi wa kitaalamu kuhusu uwapo wa viuatilifu, sumu zitokanazo na mimea na kemikali nyingine za viwandani uliofanywa na Mkemia Mkuu wa Serikali umeonyesha kuwa hakukuwa na sumu katika samaki hao na hivyo kuhitimisha kuwa vifo vya samaki hao havikutokana na uwapo wa sumu ya aina yoyote ile kwenye maji eneo la tukio.

# CUF yataka usawa zuio mikusanyiko

**Na Romana Mallya**

CHAMA cha Wananchi (CUF), kimesema kwa kuwa mikutano ya hadhara imezuiliwa kwa sababu ya janga la corona, serikali ihakikishe inazingatia usawa katika utekelezaji wa zuio hilo.

Mkurugenzi wa Habari, Uenezi na Uhusiano na Umma wa CUF, Mhandisi Mohamed Ngulangwa, aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam wakati akizungumza na waandishi wa habari.

Alisema CUF inakubaliana na mpango wote wa serikali wa kupambana na corona na huo ndio msimamo wa chama hicho tangu janga hilo liingie nchini mwaka jana. Mhandisi Ngulangwa alisema wanaunga mkono kutumika kwa njia zote za kitaalam ikiwa ni pamoja na kuzuia mikusanyiko isiyo ya lazima.

"Mwenyekiti wa Taifa CUF, Prof. Ibrahimu Lipumba, alijitokeza kupata chanjo dhidi ya corona ikiwa ni kuonyesha kwamba anapambana kuhakikisha taratibu na kanuni zinazotumika," alisema.

Hata hivyo, alisema janga la corona lisitumike kukandamiza demokrasia nchini kwa kuzuia mikusanyiko kwa wapinzani na kuacha inayohusu CCM inayoendelea.

"Hii ni kuishangaza jamii popote duniani. Je, virusi vya corona vinabagua aina ya mikusanyiko? Tunasisitiza haya yafanyike haraka," alisema.

Mhandisi Ngulangwa alimuomba Rais Samia Suluhu Hassan, akutane na viongozi wa siasa ili kuzungumzia muhktakabali wa taifa kisiasa na kidemokrasia na kueleza kuwa kikao hicho ni muhimu kwa wakati huu. Pia wamemwomba Rais Samia kuliagiza Jeshi la Polisi liache kitu walichokiita uonevu kwa viongozi wa upinzani na wanaharakati wengine wanaotumia uhuru wa kikatiba na kisheria katika kuendesha harakati zao.

Kadhalika alisema wale wote wanaoshikiliwa magerezani kwa sababu za kisiasa ama zinazotokana na Uchaguzi Mkuu mwaka 2020 au baada, Rais aingilie kati ili haki itendeke ikiwezekana waachiwe.


Air Tanzania
The Wings of Kilimanjaro

## EXCITING CAREER OPPORTUNITY

Air Tanzania Company Limited (ATCL) is implementing its five years Corporate Strategic Plan (2017/2018-2020-2021) which includes the network expansion in local, regional and international destinations as well as improvement of its internal operations and human capital management. Therefore, applications are invited from qualified Tanzanians to fill the position of Senior Human Resources Officer in Human Resources and Administration Unit.

1. **POSITION: Senior Human Resource Officer (Counselling & Employees Welfare) 1 (ATCL HQ)**

2. **REPORTING LINE: Head of Human Resource and Administration**

3. **QUALIFICATIONS:**
   The following are qualifications for aspired candidates: -
   - Must have Bachelor Degree in Human Resources Management/Public Administration/Political Science and Public administration or Degree in Commerce/Business Administration Majoring in Human Resource Management or its equivalent from recognized University/Institution.
   - Must have a formal training in counselling at least to certificate level
   - Must have at least 5 years' experience in service as Human Resource Officer in a competitive business environment.
   - Must have a proven background in provision of counselling services in a multicultural and multidisciplinary business environment

4. **COMPETENCIES:**
   - High levels of empathy
   - Mental health, counseling methods and techniques.
   - Organizational and time-management skills
   - Excellent communication, interpersonal and facilitation skills
   - Critical thinking
   - Problem-solving and flexibility
   - Strong ethical standards

5. **DUTIES AND RESPONSIBILITIES.**

   The holder of the position will perform the following duties and responsibilities:
   - Develop and oversee implementation of cost-effective staff engagement, team building and change management strategies;
   - Develop, oversee and monitor the implementation of the work-life balance guidelines
   - To oversee the implementation of leadership development programmes
   - Develop and oversee implementation of strategies that will attract employees to open up about their mental health
   - Coordinate interdepartmental and intradepartmental communication strategies
   - Listen to employees' concerns, seeking ways to address them
   - Initiate and implement interdepartmental, departmental, sections and units stress management activities that will also to promote team work
   - Plan, implement and manage the overall Talent Acquisition Strategy
   - Prepare periodic reports
   - Perform any other official duties that may be assigned by supervisor

6. **TERMS AND CONDITIONS:**
   Five 5) years contract with remuneration and fringe benefits as per ATCL Scales and Incentive Scheme

7. **MODE OF APPLICATION FOR ALL APPLICANTS:**
   Interested applicants must submit a dully signed letter for consideration of the application attached with the following:
   i. A detailed curriculum vitae (CV),
   ii. Certified copies of all certificates (including secondary school), other relevant certificates, **Applicants who have studied outside Tanzania should have their certificates approved by relevant authorities Tanzania Commission for University (TCU) or National Examination Council- NECTA)**
   iii. Two recent passport size photographs
   iv. Name and address of at least two reputable referees;
   v. Applicant's reliable contact address, email address and telephone number.

**Note: Misrepresentation of qualifications or any other information on application shall warrant legal consequences**

8. **CLOSING DATES:**

Applicants should consider the following closing dates for each post as follows:

**Within Fourteen (14) days from the first date of this announcement**

The application letters should be directed to the following address: -

**Managing Director and CEO,**
**Air Tanzania Company Limited,**
**P.O. Box 543,**
**DAR ES SALAAM**

216380002

HABARI MICHEZO

# FERNANDES: UNITED IMEJIPANGA KUSHINDA MATAJI

**MANCHESTER, England**



MANCHESTER United imeimarika na ipo tayari kushinda mataji, kwa mujibu wa kiungo, Bruno Fernandes.

Mashetani wekundu hao walishika nafasi ya pili kwenye Ligi Kuu, wakiwa wamemaliza kwenye nne bora mfululizo kwa mara ya kwanza tangu mwaka 2013, lakini walifungwa kwenye fainali ya Ligi ya Europa na Villarreal.


Ole Gunnar Solskjaer amekiimarisha kikosi chake kueleka kuanza kwa msimu mpya, akipata huduma ya Jadon Sancho kutoka Borussia Dortmund na kukubali uhamisho wa Raphael Varane kutoka Real Madrid.

Na sasa Fernandes, ambaye alifunga mabao 18 na kutoa pasi za mwisho 12 kwenye Ligi msimu uliopita, anaamini United inaweza kuwa bora zaidi.

"Kwa kawaida mara zote nafikiri tuna nafasi ya kushinda chochote tunachokitaka, au pale tunapojaribu kushinda, kwa sababu nafikiri msimu uliopita hatukuwa na bahati na hatukushinda mataji," alisema Fernandes, ambaye aliongoza kwa kutengeneza nafasi nyingi 95 kwenye Ligi Kuu msimu wa 2020-21.

"Tulifuzu kucheza fainali ya Ligi ya Europa, lakini bahati mbaya hatukushinda. Lakini bado tukiwa na usajili au bila usajili, Manchester United mara zote ni mpinzani mgumu, tutajaribu kushinda kila mashindano tutakayoingia."

Fernandes alifunga mabao 28 kwa United katika mashindano yote, ikiwa ni idadi kubwa zaidi kwa kiungo kwenye msimu mmoja wa Ligi Kuu England, akiizima ile ya Frank Lampard aliyofunga mabao 27 kwa Chelsea msimu wa 2009-10.



# MAN CITY itachezesha vijana Ngao ya Jamii

**MANCHESTER, England**

PEP Guardiola amesema Manchester City inaweza kuchezesha kikosi cha wachezaji wasio na uzoefu kwenye mechi ya Ngao ya Jamiii, ili wakubwa wapate muda wa kupumzika kutokana na uchovu wa msimu uliopita na michuano ya Euro 2020.

Man City ilianza maandalizi ya msimu mpya kwa ushindi wa 2-0 dhidi ya Preston North End, Jumanne.

Guardiola aliwapanga Joao Cancelo, Nathan Ake, Ruben Dias na Benjamin Mendy kwenye safu ya ulinzi pamoja na golikipa chipukizi wa Marekani, Zack Steffen, huku Fernandinho na Riyad Mahrez walikuwa wachezaji pekee kutoka kikosi cha kwanza.

City ilitwaa taji la Ligi Kuu kutoka Liverpool msimu uliopita pia wakishinda kombe la EFL na kufika fainali ya Ligi ya mabingwa Ulaya, ambako walifungwa na Chelsea.

Huku wachezaji wake wengi wakiwa wameshiriki michuano ya Ulaya, Guardiola anaona kwamba ni muda wa kuwapumzisha nyota wake wakubwa.

Jumamosi watacheza na Barnsley kwenye uwanja wao wa akademi ukiwa ni mchezo wa mwisho kabla ya mechi ya Ngao ya Jamii dhidi ya Leicester City kwenye dimba la Wembley, Agosti 7.

Akizungumza kupitia tovuti rasmi ya klabu hiyo baada ya ushindi dhidi ya Preston, Guardiola alisema: "Tunatakiwa kuzoea kuwa na wachezaji watatu au wanne wa kikosi cha kwanza, kila wiki na wachezaji wengi watarudi kuendelea kucheza na sisi."

# Allegri alikataa kuinoa Real Madrid

**TURIN, Italia**

KOCHA Massimiliano Allegri amebainisha kwamba, alikataa nafasi ya kuinoa Real Madrid ili aweze kurudi kwa mara ya pili kuifundisha Juventus.

Allegri aliteuliwa kuwa kocha wa Bianconeri hao Mei, mwaka huu baada ya Andrea Pirio kufungashiwa virago vyake baada ya msimu mbaya, akimaliza nafasi ya nne kwenye Ligi Kuu ya Italia, Serie A.

Allegri aliwaoongoza miamba hao wa Turin kushinda taji la Ligi Kuu la Serie A mara tano mfululizo, mataji manne ya Coppa Italia na mara mbili kutinga fainali ya Ligi ya mabingwa Ulaya.

Allegri mwenye umri wa miaka 53, Jumanne alibainisha kuwa angeweza kuchukua nafasi ya kuinoa Madrid kabla ya Carlo Ancelotti kuchaguliwa kama kocha mkuu.

"Natakiwa kuishukuru Real Madrid na rais kwa nafasi waliyonipa mimi (kuwa kocha wa Real Madrid). Halafu nilifikiria kuhusu hilo na nikachagua Juventus," alisema Allegri wakati akizungumza na waandishi wa habari.

"Ilikuwa nafasi ya mapenzi kwa klabu na kwa hakika nilifurahia nafasi ya kuinoa klabu."

Inter Milan ilitwaa taji la Ligi Kuu msimu wa 2020-21 na kumaliza umwamba wa Juventus wa kulitwaa taji hilo mara tisa mfululizo.



HABARI MICHEZO



# KOUNDE

## KUSAINI MIAKA MITANO CHELSEA

**LONDON, England**

CHELSEA imefikia makubaliano ya kumpa mkataba wa miaka mitano mlinzi wa kati wa Sevilla, Jules Kounde katika dili ambalo litamhusisha Kurt Zouma.

Kounde amekuwa kwenye rada za klabu nyingi kubwa, zikiwemo Real Madrid na Manchester United, tangu aliposhinda taji la Ligi ya Europa akiwa na Sevilla mwaka 2020.

Kwa mujibu wa Daily Mail, Chelsea wana nafasi kubwa ya kumsajili Kounde na atasaini mkataba wa miaka mitano hapo Stamford Bridge.

Iliripotiwa Jumanne kwamba, mazungumzo ya Chelsea na Kounde yameshafikia makubaliano na nyota huyo mwenye umri wa miaka 22 atasaini wakati wowote.

Mwandishi wa Sky Sport Italia na habari za usajili, Fabrizio Romano, sasa amebainisha kuwa Chelsea itampa mkataba wa miaka mitano Kounde utakaomuweka hapo hadi mwaka 2026.

Imeripotiwa kuwa katika mpango huo, Chelsea watamtoa pia mlinzi wake wa kati, Zouma.

Zouma hakuwa na nafasi ya kudumu katika kikosi cha Chelsea chini ya kocha, Thomas Tuchel katikati ya msimu uliopita, wakati awali alikuwa chaguo la kwanza chini ya kocha, Frank Lampard kabla ya Krismas.

## LIVERPOOL KUTOA PAUNI MIL 30 KWA TRAORE



**LIVERPOOL, England**

LIVERPOOL inafikiria kutoa kiasi cha pauni milioni 30 kwa Wolves ili kumsajili winga wake, Adama Traore wakati wekundu hao wakiwa kwenye harakati za kuimarisha kikosi chao kuelekea msimu wa 2021/22.

Mohamed Salah, Sadio Mane na Roberto Firmino wamebakiwa kuwa ndio nyota watatu muhimu wa mbele pale Anfield lakini Liverpool walipata huduma ya Diogo Jota kutoka Wolves kipindi cha majira ya joto kilichopita na sasa wanajaribu kumleta Traore ili kuimarisha ushindani.

Wolves wanajiandaa kumuuza Traore kipindi hiki cha majira ya joto, huku mtandao wa 90 uliripoti mwezi uliopita kwamba, mauzo ya mchezaji huyo ni kwa ajili ya kutafuta fedha za kusajili wachezaji wapya chini ya kocha mpya, Bruno Lage.

Golikipa Rui Patricio tayari ameondoka na nafasi yake imechukuliwa na Jose Sa, huku Ruben Neves yupo tayari kuuzwa kama Wolves watapata fedha wanayohitaji ya pauni milioni 30.

Traore pia yupo tayari kuondoka, licha ya kufikia makubaliano ya kusaini mkataba mpya Novemba mwaka jana.

Liverpool awali walikuwa wanahusishwa na Traore mwaka 2020 wakati Wolves walipoweka wazi kwamba thamani ya winga huyo wa Hispania ni kati ya pauni milioni 60 na milioni 80.

## MAN UNITED KUWAUZA POGBA, LINGARD

**MANCHESTER, England**

MANCHESTER inatarajia kuwauza baadhi ya wachezaji ili kujiimarisha msimu huu huku ikijiandaa kutumia pauni milioni 75 hadi 100, kwa mujibu Daily Mail.

Katika mpango huo United inataka kumuuza Pogba kwa pauni milioni 50 na Lingard kwa pauni milioni 30 na mauzo hayo kutumika kumsajili kiungo na kupata saini ya beki Kieran Trippier.

Tayari uhamisho wa Jodon Sancho akitokea Borussia Dortmund kwa pauni milioni 73 umekamilika wiki iliyopita.

Na hivi karibuni United itatangaza kukamilisha usajili wa beki wa Real Madrid Raphael, Varane kwa pauni milioni 42.

Kiungo mpya na beki wa kulia wa Athletico Madrid, Trippier anatarajiwa kusajiliwa na United wiki kadhaa zijazo, lakini usajili huo utategemea kwa kiasi kikubwa iwapo Pogba na Lingard wataruhusiwa kuondoka.



# UNITED BANK FOR AFRICA (TANZANIA) LIMITED

UBA

## UONESHAJI WA TAARIFA ZA FEDHA KWA UMMA 30.06.2021

Imetolewa chini ya kanuni ya 32 kifungu namba 3 ya kanuni za Mabenki na Taasisi za Fedha (Uoneshaji) ya Mwaka 2006

### WARAKA MIZANIA KWA TAREHE 30 JUNI 2021

(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | Robo Mwaka ya 30-Jun-21 | Robo Mwaka ya 31-Mar-21 |
|---|---|---|---|
| | **A. MALI** | | |
| 1 | Fedha Taslimu | 4,260 | 4,929 |
| 2 | Salio Katika Benki Kuu ya Tanzania | 8,476 | 6,458 |
| 3 | Uwekezaji Katika Amana za Serikali | 28,070 | 29,966 |
| 4 | Salio Katika Benki Nyingine na Taasisi za Fedha | 5,967 | 4,285 |
| 5 | Hundi na Miamala ya Kushughulikiwa | 0 | 0 |
| 6 | Miamala Baina ya Matawi | - | - |
| 7 | Bili Zilizoafikiwa | - | - |
| 8 | Dhima za Wateja Zilizokubalika | - | - |
| 9 | Mikopo Iliyotolewa kwa Benki Nyingine | 46,300 | 32,006 |
| 10 | Uwekezaji Katika Amana Nyingine | - | - |
| 11 | Mikopo Halisi Iliyopo | 71,445 | 67,846 |
| 12 | Mali Nyingine | 10,271 | 7,615 |
| 13 | Uwekezaji wa Hisa | - | - |
| 14 | Akaunti za udhamini | - | - |
| 15 | Mali Zisizohamishika, Mitambo na Vifaa | 1,853 | 1,334 |
| **16** | **JUMLA YA MALI** | **176,642** | **154,439** |
| | **B. DHIMA** | | |
| 17 | Amana za Benki nyingine na Taasisi za Fedha | 48,196 | 36,970 |
| 18 | Amana za Wateja | 85,136 | 75,781 |
| 19 | Dhamana ya Malipo kwa Fedha Taslimu | - | - |
| 20 | Amana Maalumu | 8,263 | 9,020 |
| 21 | Maagizo ya Malipo/Fedha za Kuhamisha | - | - |
| 22 | Hundi na Hawala za Kibenki Zilizotolewa | - | - |
| 23 | Limbiko la Kodi na Gharama Zitakazolipwa | 1,314 | 917 |
| 24 | Dhima la Tozo kwa Ajili ya Usuluhishi Baina ya Benki na Mteja | - | - |
| 25 | Miamala Isiyoshughulikiwa Baina ya Matawi | - | - |
| 26 | Mapato yaliyoingia ya Kipindi Kijacho na Tozo Nyingine Zitakazolipwa Baadae | 1,814 | 2,829 |
| 27 | Dhima Nyingine | 4,811 | 3,725 |
| 28 | Madeni | - | - |
| **29** | **JUMLA YA DHIMA** | **149,535** | **129,242** |
| **30** | **MALI/(DHIMA) HALISI** *(16 kutoa 29)* | **27,108** | **25,197** |
| | **C. FEDHA ZA WANAHISA** | | |
| 31 | Mtaji wa Hisa Uliolipwa | 31,420 | 31,420 |
| 32 | Akiba ya Mtaji | 29,104 | 29,104 |
| 33 | Mapato Yaliyobakizwa | (37,053) | (37,053) |
| 34 | Faida (Hasara) ya Kipindi Husika | 3,636 | 1,727 |
| 35 | Akaunti Nyingine za Mtaji | - | - |
| 36 | Stahiki ya Wenyehisa Chache | - | - |
| **37** | **JUMLA YA FEDHA ZA WANAHISA** | **27,107** | **25,197** |
| 38 | Dhima Zisizo Dhahiri | 951,915 | 869,874 |
| 39 | Mikopo Chechefu | 4,029 | 3,873 |
| 40 | Tengo kwa Ajili ya Mikopo Chechefu | 354 | 390 |
| 41 | Mali Nyingine Chechefu | - | - |
| | **D. BAADHI YA VIASHIRIO VYA HALI YA KIFEDHA** | | |
| (i) | Uwiano wa Fedha za Wanahisa na Jumla ya Mali | 15% | 16% |
| (ii) | Uwiano wa Mikopo Chechefu na Jumla ya Mikopo Ghafi | 5.60% | 6.19% |
| (iii) | Uwiano wa Mikopo Ghafi na Jumla ya Amana | 77% | 74% |
| (iv) | Uwiano wa Mikopo Halisi na Jumla ya Mali Halisi | 40% | 44% |
| (v) | Uwiano wa Mali Zinazozalisha na Jumla ya Mali | 83% | 84% |
| (vi) | Ongezeko la Amana | 10% | -25% |
| (vii) | Ongezeko la Mali | 14% | -10% |

### TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KWA ROBO MWAKA ULIOISHIA 30 JUNI 2021

(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | Robo ya Mwaka sasa 30-Jun-21 | Robo ya Mwaka linganishi 31-Mar-21 | Limbikizo la Mwaka wa sasa 30-Jun-21 | Limbikizo la Mwaka linganishi 30-Jun-20 |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Mapato ya Riba | 3,109 | 2,803 | 5,912 | 7,853 |
| 2 | Gharama za Riba | (1,040) | (765) | (1,805) | (2,855) |
| **3** | **Mapato Halisi ya Riba (1 kutoa 2)** | **2,069** | **2,038** | **4,107** | **4,998** |
| 4 | Madeni Viza Yaliyofutwa | - | - | - | - |
| 5 | Punguzo/Ongezeko la tengo katika Mikopo | - | - | - | - |
| **6** | **Mapato Yasiyo ya Riba**: | **3,664** | **3,068** | **6,732** | **4,962** |
| | 6.1 Faida /(Hasara) Zitokanazo na Miamala ya Fedha za Kigeni | 257 | 312 | 569 | 597 |
| | 6.2 Ada na Kamisheni | 3,355 | 2,719 | 6,073 | 4,329 |
| | 6.3 Gawio | - | - | - | - |
| | 6.4 Mapato Mengine | 52 | 38 | 90 | 36 |
| **7** | **Gharama Zisizo za Riba:** | **(3,796)** | **(3,352)** | **(7,148)** | **(6,979)** |
| | 7.1 Mishahara na Mafao | (1,615) | (1,615) | (3,231) | (3,379) |
| | 7.2 Ada na Kamisheni | (413) | (305) | (718) | (301) |
| | 7.3 Gharama Nyingine | (1,768) | (1,431) | (3,199) | (3,299) |
| **8** | **Faida /(Hasara) ya Uendeshaji** | **1,937** | **1,754** | **3,692** | **2,981** |
| 9 | Tengo la Kodi ya Mapato | (28) | (28) | (55) | (36) |
| 10 | **Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato** | **1,910** | **1,727** | **3,636** | **2,945** |
| 11 | **Mapato Mengine Yaliyojumuishwa (bainisha)** | - | - | - | - |
| **12** | **Jumla ya Faida (Hasara) iliyojumuishwa kwa mwaka** | **1,910** | **1,727** | **3,636** | **2,945** |
| 13 | Idadi ya Waajiriwa | 121 | 114 | 121 | 117 |
| 14 | Mapato kwa Hisa | 304 | 275 | 579 | 469 |
| **15** | **Idadi ya Matawi** | 6 | 5 | 6 | 4 |
| | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA UFANISI** | | | | |
| | (i) Uwiano wa Faida Kabla ya Kodi na Wastani wa Mali | 1.15% | 1.06% | 2.20% | 0.97% |
| | (ii) Uwiano wa Faida baada ya Kodi na Wastani wa Fedha za Wanahisa | 7.30% | 7.10% | 13.90% | 8.77% |
| | (iii) Uwiano wa Matumizi Yasiyo ya Riba na Mapato Ghafi | 56.04% | 57.09% | 56.53% | 49.71% |
| | (iv) Uwiano wa Mapato Halisi ya Riba na Wastani wa Mali Zinazozalisha | 1.50% | 1.50% | 2.98% | 1.45% |

### TAARIFA YA MTIRIRIKO WA FEDHA KWA ROBO/MWAKA ULIOISHIA 30 JUNI 2021

(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | Robo ya Mwaka ya sasa 30-Jun-21 | Robo ya Mwaka linganishi 31-Mar-21 | Limbikizo la Mwaka wa sasa 30-Jun-21 | Limbikizo la Mwaka linganishi 30-Jun-20 |
|---|---|---|---|---|
| **I: Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uendeshaji:** | | | | |
| Mapato/(Hasara) Halisi | **1,910** | **1,754** | **3,636** | **2,945** |
| Marekebisho kwa Ajili ya: | | | | |
| - Hasara Katika Mali | 276 | 133 | 276 | 256 |
| - Badiliko Halisi Katika Mikopo | (3,599) | (11,883) | (3,599) | (7,785) |
| - Faida/Hasara Kwenye Mauzo ya Mali | - | - | - | - |
| - Mabadiliko Halisi Katika Amana | 19,825 | (15,361) | 19,825 | (38,761) |
| - Mabadiliko Halisi Katika Amana za Muda Mfupi Zilizoafikiwa | 1,896 | (5,960) | 1,896 | 10,701 |
| - Mabadiliko Halisi Katika Dhima Nyingine | 1,086 | 117 | 1,086 | (540) |
| -Mabadiliko Halisi Katika Mali Nyingine | (2,657) | (1,657) | (2,657) | 1,342 |
| - Kodi Iliyolipwa | - | (28) | - | - |
| -Mengineyo (bainisha) | - | - | - | - |
| *Fedha Halisi zilizotolewa (zilizotumika) kwa shughuli za uendeshaji* | **18,737** | **(32,885)** | **20,464** | **(31,842)** |
| **II. Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uwekezaji:** | | | | |
| Gawio Lililopokewa | - | - | - | - |
| Ununuzi wa Mali za Kudumu | (661) | (51) | (661) | (225) |
| Mapato Kutokana na Mauzo ya Mali za Kudumu | - | - | - | - |
| Ununuzi wa Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | - | - | - |
| Mapato Kutokana na Mauzo ya Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | - | - | - |
| Mengineyo (bainisha) | - | - | - | - |
| *Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Uwekezaji* | **(661)** | **(51)** | **(661)** | **(225)** |
| ***III. Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Kifedha:*** | | | | |
| Ulipaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - | - | - |
| Mapato Kutokana na Utoaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - | - | - |
| Mapato Kutokana na Utoaji wa Mtaji wa Hisa | - | - | - | - |
| Gawio Lililolipwa kwa Fedha Taslimu | - | - | - | - |
| Mabadiliko Halisi Katika Madeni Mengine | - | - | - | 29,916 |
| Mengineyo (bainisha) | - | - | - | - |
| ***Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Kifedha*** | **-** | **-** | **-** | **29,916** |
| IV. Fedha Taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu: | | | | |
| Ongezeko / Punguzo Halisi Katika Fedha taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu | **18,076** | **(32,936)** | **19,803** | **(2,151)** |
| Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwanzoni mwa Robo Mwaka | 86,138 | 119,074 | 119,074 | 107,794 |
| Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwishoni mwa Robo Mwaka | **104,214** | **86,138** | **138,877** | **105,644** |

### TAARIFA YA MABADILIKO YA MTAJI KWA KIPINDI KINACHOISHIA 30 JUNI 2021

(Kiasi kwa shilingi millioni)

| | Mtaji wa Hisa | Malipo juu ya bei ya hisa | Mapato yaliyobakizwa | Ziada ya Kisheria | Tengo la ziada ya jumla | Mengineyo | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Mwaka wa sasa 2021** | | | | | | | |
| Salio la mwanzo wa mwaka | 31,420 | 29,104 | (37,053) | - | - | - | 23,471 |
| Faida/(Hasara) Halisi baada ya kodi ya mapato | - | - | 3,636 | - | - | - | 3,636 |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Ziada ya kisheria | - | - | - | - | - | - | - |
| Tengo la ziada ya jumla | - | - | - | - | - | - | - |
| Mengineyo | - | - | - | - | - | - | - |
| Share issued | | | - | | - | | |
| **Salio la mwisho wa mwaka** | **31,420** | **29,104** | **(33,417)** | **-** | **-** | **-** | **27,107** |
| **Mwaka uliopita 2020** | | | | | | | |
| Salio la mwanzo wa mwaka | 31,420 | 29,104 | (40,498) | - | - | - | 20,026 |
| Faida/(Hasara) Halisi baada ya kodi ya mapato | - | - | 3,445 | - | - | - | 3,445 |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Ziada ya kisheria | - | - | - | - | - | - | - |
| Tengo la ziada ya jumla | - | - | - | - | - | - | - |
| Mengineyo | - | - | - | - | - | - | - |
| Share issued | - | - | - | - | - | - | - |
| **Salio la mwisho wa mwaka** | **31,420** | **29,104** | **(37,053)** | **-** | **-** | **-** | **23,471** |

| | ***Jina na Cheo*** | ***Saini*** | ***Tarehe*** |
|---|---|---|---|
| 1 | Kingsley Ulinfun<br>**Mkurugenzi Mtendaji** | ***Imesainiwa*** | *29th July 2021* |
| 2 | Chomete Hussein<br>**Mkuu wa Fedha** | ***Imesainiwa*** | *29th July 2021* |
| 3 | Joseph Ringa<br>**Mkaguzi Mkuu wa Ndani** | ***Imesainiwa*** | *29th July 2021* |

Katika kuanda taarifa za hizi za fedha, sera za uandaaji ni zilizile zilizotumika wakati wa uandaaji wa Taarifa za Fedha zilizokaguliwa za mwaka uliopita (kama kulikua na mabadiliko katika sera za uandaaji taarifa za fedha katika kipindi cha robo mwaka ya/mwaka wa sasa, mabadiliko yaelezwe kwa mujibu wa IAS 34 na IAS 8).

| | ***Jina na Cheo*** | ***Saini*** | ***Tarehe*** |
|---|---|---|---|
| 1 | Amb.Tuvako Manongi<br>**Mkurugenzi** | ***Imesainiwa*** | *29th July 2021* |
| 2 | Oliver Alawuba<br>**Mkurugenzi** | ***Imesainiwa*** | *29th July 2021* |

United Bank for Africa (T) Ltd is a subsidiary of United Bank for Africa Plc, a leading Pan African bank offering universal banking to more than 13 million customers in over 1000 branches and outlets in Africa , USA and Europe .

**East & South Africa**
- Tanzania
- Kenya
- Congo DRC
- Mozambique
- Uganda
- Zambia

**Central Africa**
- Cameroon
- Gabon
- Tchad
- Congo Brazzaville

**West Africa**
- Ghana,
- Benin
- Burkina Faso,
- Cote D'Ivoire (CDI)
- Liberia
- Sierra Leone
- Senegal
- Mali
- Guinea

**Europe**
- UK
- France

**USA**
- New York

216380702

# SIMBA SC YAIFANYIA KAZI RIPOTI YA GOMES

**Na Saada Akida**

UONGOZI wa Simba umesema baada ya mapumziko ya wiki mbili kwa wachezaji wao wanatarajia kurejea kwa kishindo kwa kusajili kikosi imara 'Unbeaten' kuelekea msimu ujao wa Ligi Kuu Tanzania Bara na michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

Akizungumza na gazeti hili jijini Dar es Salaam jana, Makamu Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa Simba, Salim Abdallah, 'Try Again' alisema wanaendelea vizuri na mipango yao ya maboresho ya kikosi ikiwamo kusajili wachezaji wenye uwezo mkubwa.

Alisema viongozi wana uhakika na wachokifanya, ikiwamo kuwa makini katika usajili wao kuhakikisha msimu ujao wanakuwa na kikosi imara zaidi.

"Kila kitu kinaenda vizuri, Wanasimba wanatakiwa kutulia na kusubiri waone kazi yetu inayofanywa na viongozi wao, baada ya kupokea ripoti ya Kocha Gomes (Didier) na kufanyia kazi mapendekezo yake ikiwamo usajili wa wachezaji wenye kiwango kizuri na kuwa na kikosi imara ambacho ni 'Unbeaten'," alisema Try Again.

"Tumejipanga vizuri katika usajili wetu, mashabiki, wanachama na wapenzi wa Simba wanatakiwa kuwa watulivu kwa sababu wanafanya maboresho kwenye mapungufu yao kulingana na mahitaji."

Alisema watafanya marekebisho madogo kulingana na mahitaji ya benchi la ufundi kuelekea katika mipango yao ya msimu ujao wa Ligi Kuu pamoja na kutaka kufanya vizuri na kutawala soka la Afrika.



Wakazi wa Temeke Dar es Salaam wakicheza mchezo wa drafti katika eneo la kituo cha mabasi Temeke Mwisho hivi karibuni. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## 'Katapila' adai hajachuja kwenye dansi

**Na Sabato Kasika**

MWIMBAJI mkongwe wa muziki wa dansi Rogart Hegga 'Katapila' amesema, bado yuko vizuri kwenye muziki huo ingawa baadhi ya watu wamekuwa wakidhani kuwa amepotea.

'Katapila' amesema, kutosikika kwake kama zamani kunatokana na muziki wa dansi kukosa nafasi ya kutosha kwenye baadhi ya vyombo vya habari hali ambayo inasababisha wanamuziki wengi kutosikika.

"Bado niko imara nikiwa na bendi ya Sayari inayoongozwa na Badi Bakule, ingawa sisikiki kama zamani kutokana na dansi kukosa nafasi kwenye baadhi ya vyombo vya habari," amesema 'Katapila'.

Mwanamuziki huyo aliyepitia bendi mbalimbali zikiwamo za Twanga Pepeta, Mchinga Sound, TOT -Plus, Extra Bongo na Ruvu Stars, amesema anaamini bado muziki wa dansi una nguvu.

"Ninaamini watu wa dansi, wanajua niko wapi, lakini tatizo ni kukosa nafasi ya kutosha kwenye vyombo vya habari ambayo ingesaidia kutufanya wanamuziki wote kutamba kama zamani," amesema.

Amesema, yeye Badi Bakule ni miongoni mwa waimbaji waliotamba katika muziki wa dansi, lakini sasa hawasikiki, lakini wanaamini mashabiki wanaofika kwenye maonyesho ya bendi ya Sayari wanajua kile kinachofanywa huko.

'Katapila' amesema, ingawa muziki umekosa nafasi ya kusikika kwenye baadhi ya vyombo vya habari, anaamini ipo siku utarudi katika chati kama zamani, na kuwataka mashabiki waendelee kuvumilia.

.

## Yanga SC yaahidi kisasi Ngao ya Jamii

**Na Adam Fungamwango**

BAADA ya kuchapwa bao 1-0 kwenye mechi ya fainali ya Kombe la FA dhidi ya Simba, klabu ya Yanga imewaahidi wanachama na mashabiki wake kuwa italipiza kisasi kwenye mechi ya ufunguzi wa msimu mpya wa Ligi Kuu Tanzania Bara 2021/22.

Nahodha wa timu hiyo, Bakari Mwamnyeto, amesema kuwa baada ya kupoteza mechi ya fainali dhidi ya Simba na kumalizika kwa msimu bila kupata ubingwa, wanajipanga vema kwa msimu ujao ili kulipiza kisasi cha kufungwa kwenye Uwanja wa Lake Tanganyika na kulikosa kombe la FA.

"Tunashukuru Mungu ligi imeisha salama. Lakini tunajipanga vizuri kwa msimu utakaoanza. Tuko vizuri, tunawaahidi wanachama na mashabiki wa Yanga kuwa hatutowaangusha kwenye mechi ya Ngao ya Jamii," alisema nahodha huyo.

Simba na Yanga zitafungua msimu mpya wa Ligi Kuu 2021/22 kwenye mechi ya Ngao ya Jamii.

"Tutalipiza kisasi na pia tutachukua ubingwa. Hata msimu huu lengo letu lilikuwa ni hilo, lakini ilishindikana, kwa hiyo tunajipanga tena kwa msimu ujao," alisema Mwamnyeto ambaye alisajiliwa kabla ya msimu huu, akitokea Coastal Union.

Kwenye Ligi ya Mabingwa, Mwamnyeto alisema kuwa watajipanga vema ili kufanya vizuri kwenye michuano hiyo pia.

"Hata kwenye mechi za kimataifa, pia tunakwenda kujiandaa kisawasawa ili kuiwakilisha vizuri nchi na naamini tutafanya vema," alisema.

Yanga imemaliza msimu huu ikiwa na Kombe la Mapinduzi pekee ililolitwaa Zanzibar Janauri 13, mwaka huu, baada ya kuichapa Simba kwa mikwaju 4-3 ya penalti, zikitoka suluhu bila kufungana dakika 90 za mchezo.

## Coastal Union kuwaongezea mikataba nyota wake

**Na Saada Akida**

KATIBU Mkuu wa Coastal Union, Rashid Mgweno, amesema wamejipanga na kuwaongezea mikataba baadhi ya wachezaji wao wa kikosi cha kwanza kwa kuhofia yaliyotokea msimu uliopita.

Akizungumza na gazeti hili, Mgweno alisema kuondoka kwa wachezaji saba msimu uliopita huku wakiwa huru imewapa fundisho na sasa wako katika mchakato wa kuwaongezea mikataba nyota wao akiwamo Hance Masoud na wengine.

Alisema mbali na nyota hao tayari kamati ya usajili imeingia kazini kwa ajili ya kufanya mazungumzo na wachezaji wapya kwa lengo la kuimarisha kikosi cha timu hiyo kwa ajili ya msimu ujao wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

"Ni kweli msimu ulioisha hatukuwa na kikosi imara, hasa baada ya wachezaji wetu wengi kuondoka bure kasoro, Bakari Mwamnyeto, hatukufanya vizuri, lakini tumepata bahati ya kubaki kwenye Ligi Kuu," alisema Mgweno.

Aliongeza; "Na sasa hatutaki kurudia makosa yaliyopita tunawaongeza mikataba wachezaji ambao ni hitaji la kocha wetu, Mgunda (Juma), pamoja na kuanza mazungumzo na wachezaji wapya."

Michezo
Alhamisi Julai 29, 2021
Nipashe



## Man City kutoa pauni Mil. 75 kwa Grealish

HABARI UK. 22



Mchezaji wa Zambia, Ireen Lungu (chini), akiwania mpira dhidi ya Andressa wa Brazil katika mchezo wa michuano ya Soka la Wanawake Olimpiki baina ya timu hizo juzi, mjini Saitama, Japan. Brazil ilishinda 1-0 na kutinga Robo Fainali. **PICHA: MTANDAO**

# SIMBA, MANARA WAACHANA RASMI

●●● Klabu yamshukuru kwa kazi aliyoifanya, huku nafasi yake ikipewa mwandishi wa habari...

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Simba imetangaza kuachana na Mkuu wa Idara ya Habari na Mawasiliano ya Klabu hiyo, Haji Manara, baada ya kutotaka kuendelea kuhudumu klabu hiyo, na hapo hapo imemteua Ezekiel Kamwaga kuwa Kaimu Mkuu wa idara hiyo kwa muda wa miezi miwili.

Kwa mujibu ya taarifa iliyotolewa na klabu hiyo jana, ikitoka kwenye Bodi ya Wakurugenzi imesema kuwa imeridhia matakwa ya Manara kutoendelea kuhudumu katika nafasi hiyo kama Msemaji wa Klabu, hivyo imemshuruku na kumtakia kila la kheri katika shughuli zake.

Taarifa hiyo iliyochapishwa kwenye mtandao rasmi wa klabu hiyo, ilisema inamshukuru kwa maneno aliyoyatumia kuwaaga Wanasimba katika kundi la viongozi wa Simba (Simba HQ) na kwa kazi kubwa aliyoifanya kwenye klabu hiyo kwa kipindi chote alichoshika nafasi hiyo.

Katika taarifa hiyo, pia klabu hiyo imemteua Kamwaga kuwa kaimu kwa kipindi cha miezi miwili, ambacho atashiriki maboresho ya muundo na utendaji wa idara hiyo.

Ilisema kuwa kaimu huyo ni mwandishi wa habari mwenye uzoefu wa zaidi ya miaka 15 kwenye tasnia ya habari, akifanya kazi kwenye vyombo vya habari vya ndani na kimataifa.

Pia, ilisema kuwa mkuu huyo anaijua vizuri klabu ya Simba na historia yake, kwani ameshawahi kuitumikia katika nafasi ya Msemaji na Kaimu Katibu Mkuu wa Simba.

Vile vile, taarifa hiyo ilisema mara baada ya maboresho ya Idara ya Habari na Mawasiliano, pamoja na idara zingine klabu itatangaza fursa mbalimbali za ajira katika kipindi cha wiki chache zijazo.

Manara aliteuliwa na klabu hiyo kuwa msemaji wa klabu 2015, akichukua nafasi ya Asha Muhaji aliyefariki mwaka 2020, na kuhudumu kwa miaka sita.

Kamwaga alishawahi kuwa Katibu Mkuu wa klabu hiyo 2014, kazi ambayo aliihudumu kwa muda wa miezi sita tu, chini ya aliyekuwa Mwenyekiti wa wakati huo, Ismail Aden Rage.

Ikumbukwe Kamwaga alichaguliwa kuwa Kaimu Katibu Mkuu akichukua nafasi ya Mwanasheria Evodius Mtawala, akitoka kuwa Ofisa Habari wa klabu hiyo, na baada ya kuteuliwa, ndipo marehemu Muhaji naye akateuliwa kuchukua nafasi ya Kamwaga.

## Yanga kukamilisha usajili wiki mbili

**Na Saada Akida**

UONGOZI wa Yanga sasa umeelekeza nguvu zake katika kuimarisha kikosi na wanatarajia ndani ya wiki mbili watakuwa wamekamilisha usajili wa kikosi cha timu hiyo, kuelekea msimu ujao wa Ligi Kuu Tanzania Bara na michuano ya kimataifa.

Akizungumza na gazeti hili jana, Mshauri wa Yanga, Senzo Mazingiza alisema baada ya kurejea kutoka Kigoma walikuwa na kikao viongozi wote wa kamati ya utendaji kwa lengo la kukamilisha usajili wa wachezaji wapya.

Alisema uongozi umejipanga vizuri na ndani ya wiki ijayo kikosi cha Yanga kitakuwa imara kulingana na kukamilisha usajili wa wachezaji wapya na kuungana na wenzao kurejea kambini mapema.

"Uongozi umejipanga vizuri, ndani ya siku hizi chache tutakamilisha usajili wa wachezaji wapya, zoezi la usajili linaendelea ili kuhakikisha nyota wapya wanakuwa sehemu ya kikosi kuelekea michuano ya Kagame," alisema mshauri huyo.

Alisema wako makini katika usajili wa ndani na nje, kulingana na mahitaji yao kuelekea msimu ujao kwa kufanya vizuri katika michezo ya Ligi Kuu na michuano ya kimataifa.

"Muda ni mchache tunatakiwa, kukamilisha usajili mapema kabla ya Agosti 15, tuna kazi ya kufanya na tuko makini hadi wiki ijayo tukamilishe usajili kwa asilimia kubwa," alisema Senzo.

Alisema kuwa na kikosi imara kwa msimu ujao kulingana na jinsi ya mapendekezo ya benchi lao la ufundi chini ya kocha wao Nesreddine Nabi kwa ajili kuboresha kikosi chao kulingana na mahitaji ya msimu ujao.

Mshauri huyo alisema wanatarajia wachezaji wapya kuanza kuonekana katika michuano ya Kombe la Kagame itakayoanza kutimua vumbi Agosti Mosi mwaka huu jijini Dar es Salaam.

Katika michuano hiyo Yanga imethibitisha kushiriki ikiwa ni miongoni mwa timu za nchi sita ambazo zitacheza michuano hiyo huku ikiwa imepangwa kundi C ambalo kuna Yanga, Nyasa Big Bullets (Malawi) na Express FC (Uganda).

Kundi B kuna AZAM FC (Tanzania), Atlabara (Sudan Kusini), Tusker (Kenya) na Kundi A kutakuwa na KCCA (Uganda), Le Messanger Ngozi FC (Burundi) na KMKM FC (Zanzibar)

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042
9 770856 541002 >